ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tatu – Tarehe 26 Machi, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Nam. 8 ya mwaka 1983 na Kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo hapa Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na Kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maoni ya upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 58

Wasichana Wanaotoroshwa na Kutelekezwa

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Hivi sasa kumezuka wimbi la wanaume wasiowaaminifu kuwahadaa wasichana ambao bado wapo kwenye uangalizi wa wazee wao na kuwaleta Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Baadhi yao huwapa ujauzito na kutelekezwa hasa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ambako mara kadhaa Serikali ya Wilaya imepata kazi ya kuwarejesha makwao baadhi yao.

(a) Kwa kuwa suala hili linaongezeka badala ya kupungua, wizara yako ina mpango gani kuliondoa?

(b) Kwa kuwa baadhi ya vijana waliofanya vitendo hivyo wamewahi kukamatwa, Je, hatua gani zilichukuliwa dhidi yao?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 58 lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa hadi sasa Mkoa wa Kaskazini Unguja haujapokea kesi za wanaume wasiowaaminifu wanaowadanganya watoto waliochini ya uangalizi wa wazee wao.

Kilichojitokeza na ambacho kinaendelea kuleta usumbufu katika Mkoa wa Kaskazini ni wimbi la wasichana wanaoshawishiwa na wanaume wasio waaminifu kuja Zanzibar kutoka Tanzania Bara, kwa sababu za kutaka kuwaoa/kuwapatia kazi katika Hoteli za Kitalii na mara tu wanapofika nao Zanzibar huwakimbia na hatimae kufika katika Afisi za Wakuu wa Wilaya kwa kuomba msaada.

Mhe. Spika, naomba kutoa majibu kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imejipanga kikamilifu kudhibiti vitendo viovu vinavyoathiri mila na silka za Wazanzibari. Tunaomba kwa Waheshimiwa na wananchi wote kutoa taarifa mapema kwa vyombo vya sheria mara tu wanapoona tukio lolote lenye uovu wanaoufanya au wanaofanyiwa vijana wetu.

(b) Hakuna kijana yeyote aliyekamatwa kutokana na kosa la kufanya vitendo hivyo lakini jumla ya wasichana wane (4) wamefika katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya Kaskazini “A” kuomba kusaidiwa baada ya kutelekezwa na wenyeji wao. Afisi ya Mkuu wa Wilaya imewasafirisha kuwarejesha kwao.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali maja la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Waziri ametwambia kwamba hakuna kesi ya mwanamme inayosemekana labda amekamatwa au anawaleta wasichana kwa ajili ya kitu fulani. Mhe. Spika, taarifa sahihi ambazo tunazipokea katika vyombo vya

habari hasa mawio kwa upande wetu huu wa Mkoa wa Kaskazini tunaye ndugu Mirando ni mzuri sana wa kufuatilia mambo mbali mbali yanayotokezea.

Hivyo mheshimiwa inasemekana kwamba kuna baadhi ya akina mama wanaotoka Tanzania Bara wanaoishi hapa Zanzibar huwaleta watoto kwa kutafuta ajira au mambo mengine machafu na baada ya kufika hapa wasichana wale kwa bahati mbaya kama hawakuelewana huwa wanawatoroka na kuwaacha wanasumbuka. Hivyo, mheshimiwa taarifa hii anayo na kama anayo anatoa wito gani kwa serikali na wananchi wanaohusika na mambo kama hayo ili wasiendelee nayo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, suala ameliondoa kwa akina baba na sasa amelipeleka kwa akina mama. Mhe. Spika, mimi naijua kesi moja imewahi kutokea lakini haikuweka Kaskazini ilitokea Kusini kwamba kuna mama mmoja alikuwa anachukua wasichana kutoka Bara na kuwaleta hapa kwa kutaka kuwafanyisha kazi ambazo si halali. Mhe. Spika, serikali imechukua hatua juu ya suala hilo na imelirekebisha. Kwa hivyo, na huku kama wako watu kama hao ni vizuri serikali ikajuilishwa na bila shaka itachukua hatua ya kulirekebisha.

Nam. 89

Eneo la Wazi Baina ya Starehe Club na Tembo Hotel

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu - Aliuliza:-

Serikali kwa nia njema kabisa imetenga baadhi ya maeneo wazi kuwa ni sehemu za kupumzika. Lakini pamoja na nia hiyo nzuri, eneo la wazi baina ya Starehe Club na Tembo Hotel, inatumiwa vibaya na watu, vijana na magenge ya wahuni na vibaka kwa kuvuta bangi na madawa ya kulevya, kinyuma na malengo na shabaha ya sehemu hiyo.

Mhe. Waziri, kwa kuwa matumizi ya eneo hilo hayaendani na malengo ya serikali; na kwa kuwa hali hiyo haipendezi na inatia hofu kwa wakaazi wa Mji Mkongwe na hata kwa watalii wanaozunguka na kutembelea maeneo ya Forodhani.

Je, serikali haioni kuwa ni vyema ikalitoa eneo hilo kwa mwekezaji ili litumike vizuri na kuzalisha mapato kwa faida ya nchi, kuliko kuendelea katika hali ya sasa inayotia hasara kwa taifa?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 89 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba eneo baina ya Starehe Club na Tembo Hotel linatumika vibaya na watu, vijana na magenge ya wahuni na vibaka kwa kuvuta bangi na madawa ya kulevya kinyume na malengo na shabaha ya sehemu hiyo.

Mhe. Spika, wizara yangu pamoja na malengo ya serikali yaliopo itashauriana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kuona namna bora na ya haraka ya kutumia eneo hilo kwa maslahi ya nchi yetu.

Nam. 28

Ujenzi wa Minara katika Maeneo ya Makaazi

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Hivi sasa kumezuka wimbi la Kampuni za Simu za Mkononi kujenga minara yao ya mawasiliano katika maeneo ya makaazi ya watu mijini na vijijini Unguja na Pemba kwa lengo la kurahisisha mawasiliano.

(a) Je, Mhe. Waziri, katika ujenzi wa minara hiyo wizara yako inashirikishwa kiasi gain?

(b) Je, kitaalamu hakuna madhara ya kiafya wanayoweza kupata watu wanaoishi katika maeneo ya jirani na minara hiyo?

(c) Kama yapo madhara, kwa nini minara iruhusiwe katika maeneo hayo na nani atawajibika kwa afya za watu hao?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye kifungu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

a) Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu inashirikishwa ipasavyo katika suala la ujenzi wa minara, kwani hilo wizara yangu imeunda Kamati ya Kitaifa inayosimamia Ujenzi na Utumiaji wa Minara ya Mawasiliano Zanzibar. Kamati hiyo huarifiwa kabla ya hatua zozote za ujenzi wa minara kuanza, baada ya kuarifiwa kamati hiyo hufanya ukaguzi maalum katika eneo husika kwa lengo la

kuangalia eneo hilo linaloombwa. Baada ya ukaguzi huo kamati hukaa na kufanya tathmini ya eneo hilo na na kupendekeza kwa mamlaka husika ili kutoa ruhusa ya ujenzi au kutoruhusu kulingana na uhalisia wa eneo husika. Kamati hiyo imeshirikisha taasisi zifuatazo:-

(i) Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi
(ii) Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ
(iii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) – Zanzibar
(iv) Idara ya Mazingira Zanzibar
(v) Idara ya Anga Zanzibar
(vi) Idara ya Ardhi na Mipango Mji Zanzibar.

b). Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) limefanya utafiti juu ya athari za mionzi ya minara ya simu na utafiti huo unaonesha kwamba mionzi inatokana na minara ya simu haina athari yoyote kwa binaadamu. Vile vile Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) imethibitisha hilo kutokana na utafiti wake uliofanywa mwaka 2009. Hivyo, mpaka sasa wizara yangu haijapata utafiti wowote wa kitaalamu unaonesha kuwepo kwa madhara ya kiafya yanayosababishwa na kuwepo kwa minara katika maeneo ya makaazi ya watu.

c). Wizara yangu kupitia Kamati hiyo ya Kitaifa ya Minara inaweka mlango wazi kwa kupokea ushauri wowote wa kitaalamu na kwa yeyote atakayegundua madhara ya aina yoyote yanayotokana na minara. Kamati hiyo ipo tayari kupokea taarifa hiyo wakati wowote na wizara yangu ina ahidi kuchukua hatua zinazofaa kwa kushirikiana na taasisi nyengine kama vile *TCRA* na taasisi zinazohusiana na masuala ya afya.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wizara inahusika na waandaji wa mpango mzima wa ujenzi wa minara lakini hivi sasa kuna maeneo ambayo yamekuwa ni kero kwa wananchi kwani minara hiyo imejengwa bila ya wananchi kushauriwa katika maeneo hayo.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa unasema unasikiliza mashauri mbali mbali na uko tayari kufuatilia mambo ambayo yanahusiana na hayo je, kama watu hao watajitokeza wakija katika wizara yako uko tayari kuwasaidia vipi?

b) Kwa kuwa hivi sasa katika teknolojia mpya zinazoendelea minara ni sehemu ambayo inatizamiwa kuondoka kabisa hivi sasa watu wanatumiwa *satellite*. Hivyo wanampango gani wa kuwahamasisha wawekezaji hivi sasa kutumia *satellite* badala ya minara?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwamba wizara yangu tayari ina kamati ambayo inashughulikia masuala haya na kwa ushauri wa Mhe. Mwakilishi iwapo kutatokea tatizo hilo basi kama nilivyosema milango iko wazi waje katika taasisi zetu pamoja na wizara yetu watapata ufumbuzi ambao unafaa.

Mhe. Spika, suala la kutumia satellite ni jema na nafikiria watu wote wanakwenda huko kwa hivyo na sisi tunategemea hali ya uchumi itakavyoturuhusu tunategemea kuelekea huko.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana aliyoyatoa. Lakini suala hili linapitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi lakini naomba nilielekeze kwenye kiti chako zaidi. Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba ilifanyika semina hapa ndani ya Baraza ya *TCRA* na ilihudhuriwa pia na Naibu Waziri Mhe. Dk. Mauwa Daftari na katika semina hiyo paliahidiwa kwamba patafanyika semina nyengine ama ile sheria ya *TCRA* kuwasilishwa hapa Zanzibar kwa ajili ya kuthibitishwa kwa sababu *TCRA* tayari ipo hapa Zanzibar na inafanyakazi. Kwa hivyo, sijui ufuatiliaji wa sheria ile kuletwa hapa Barazani na kuthibitishwa umefikia wapi.

Mhe. Spika, jambo la pili itakumbukwa pia kupitia kiti chako kwamba walikuja hawa Kampuni ya *ZANTEL* kuja kutufanyia semina na mwisho wa semina wewe mwenyewe ulikubaliana nao kwa ahadi kwamba watatufanyia semina ya siku tatu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nilisikia kipindi fulani kwamba mualiko huo wa semina wa siku tatu uliletwa lakini kutokana na Baraza kuwa na ratiba nyengine haukuweza kufanyika, ilikuwa wameleta kwa ajili ya Hotel ya Ocean Paradise kwa ajili ya kufanya hiyo semina. Mhe. Spika, baada ya hapo ile semina haikufuatiliwa tena hadi hivi sasa. Sijui ile ahadi imefikia wapi ya kufanyiwa semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili wakaweza nao kufaidika kutokana na haya mambo ya minara na teknolojia kwa sababu masuala haya yanarudia kila siku na hiyo ahadi ilishatolewa? Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri hebu jibu hilo suala la sheria ile inayohusu *TCRA* kuweza kuletwa hapa kwa ajili ya kuthibitishwa kama unayo taarifa, hili

jengine ni la Baraza ambalo mawasiliano zaidi yatafanywa na *ZANTEL* ili kuona semina hiyo inafanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri hapa nafikiri alichotaka ni kutukumbusha tu kwamba hii sheria lini italetwa. Mhe. Spika, nataka kumwambia kwamba kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano basi tutafanya mawasiliano ya karibu kuona hii sheria lini italetwa na mara tu baada ya kupata taarifa hiyo tutaiwasilisha Barazani.

Mhe. Said Khelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wanashirikishwa katika ujenzi wa minara Bumbwini umejengwa mnara huu ni muda mrefu sana haujatumika hivyo kuna sababu zipi mpaka sasa hivi ikawa haujatumika?

b) Kuna wafanyakazi wawili wameajiriwa hapo lakini hadi sasa si chini ya miezi 11 hawajalipwa. Je, Mhe. Naibu Waziri atachukua hatua gani kuhusu watu hao?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, suala la mnara wa Bumbwini nafikiri unatumika isipokuwa suala la pili ambalo la wafanyakazi wake ambao wameajiriwa na hawajalipwa hili naahidi kulifuatilia na si muda mrefu tutapata ufafanuzi kwa nini hawajalipwa.

Nam. 27

Matengenezo ya Barabara za Kusini Pemba

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Hivi sasa tayari kazi za ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba zilizofadhiliwa na Serikali ya Norway imeanza kwa ujenzi wa Barabara ya Mtambile – Mwambe na hatua ya kwanza ya uwekaji wa kifusi umekamilika. Lakini ziko dalili za kuchelewa kwa kazi hiyo kutokana na upungufu uliopo wa vifaa.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba upungufu huo unaweza kucheleweshe kukamilika kwa kwa kazi hiyo?

(b) Kazi ya uwekaji wa lami ya majaribio kwa kilomita moja imekwama. Je, ni sababu gani iliyokwamisha kazi hiyo?

(c) Baadhi ya wanachi katika baadhi ya maeneo wanadai fidia ya nyumba na vipando vyao vilivyoathika kwa ujenzi huo. Je ni kiasi gani cha za fidia kinachohitajika kuwalipa watu hao?

Mhe. Naibu Waziri Mawasiliano na Uchukuzi:- Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa ni kweli hivi sasa tayari kazi za ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba zile zinazofadhiliwa na Serikali ya Norway zimeanza kwa ujenzi wa Barabara ya Mtambile–Mwambe na hatua ya kwanza ya uwekaji wa kifusi umekamilika.

Mhe. Spika, baada ya maendeleo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavo:-

a) Ni kweli kuwa upungufu wa vifaa vya ujenzi unaweza kucheleweshe kukamililika kwa kazi hiyo, lakini hatua mbali mbali zimeshachukuliwa za ununuzi wa zana mpya za kuzitengenezea zana kongwe. Hivi sasa vipuri hivyo vimeshafika kisiwani Pemba na matengenezo ya barabara hiyo yanaendelea vizuri. Ni mategemeo yetu kwamba kazi hii itakamilika kwa wakati.

b) Mhe. Spika, kazi ya uwekaji wa lami ya majaribio ilisitishwa kwa vile lami iliyoletwa awamu ya kwanza haikuwa katika kiwango kinachotakiwa, hivyo iliamriwa irejeshwe kwa kampuni husika na badala yake iletwe nyengine, hatua ambayo ilifanyika na lami nyengine imeshawasili Kisiwani Pemba.

c) Kwa sasa hatuna fidia ya nyumba iliyolipwa kwani kuna mabadiliko yamefanywa ili kupunguza uvunjaji wa majumba isipokuwa pale tu ambapo ni lazima. Kazi ya kutathmini malipo ya mazao hivi sasa iko katika Wizara ya Kilimo na mara tu badala ya kukamilika basi watalipwa fidia hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa tena nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b), (c) na (d).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba lami iliyoletwa ilikuwa haifai, ni kweli lami ambayo sasa hivi imeletwa nimeishuhudia lakini lami hiyo haina hata lebo kwamba ni ya nchi

gani. Mhe. Spika, nataka nijue ni kampuni gani iliyopewa kazi hiyo na lami hiyo ni kutoka nchi gain?

b) Kwa kuwa nyumba nne zimeathirika na hazifai tena kwa makaazi ya wanadamu ni lini hatma ya wananchi wale?

c) Kwa kuwa Baraza hili limeshuhudia matendo ambayo serikali ilifanywa na Kampuni ya Prismo kwa barabara ya Mfenesini-Dunga na hatimae kampuni kukimbia. Kwa kuwa mimi ni mkaazi wa Mwambe kuna dalili zinaonekana hivyo. Je, lini wizara yake itaipeleka Kamati ya Mawasiliano kwenda kushuhudia udhaifu huo?

d) Kwa kuwa teknolojia ya ujenzi wa barabara ile sasa wanatumia vyuma na vyuma ambavyo viko Mwambe ni vyuma zaidi ya nane, basi hata hivyo vyuma vinashindwa kununuliwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, suala alilouliza kwamba lami inatoka wapi au nchi gani. Mhe. Spika, kwa kuwa sikujiandaa na hilo nitamtafutia kujua hiyo lami inatoka nchi gani na mengineyo.

Mhe. Spika, kuhusu nyumba ambazo ziko katika hali mbaya. Mhe. Spika, tumesema kwamba nyumba zile ambazo tu zitalazimika kuvunjwa ndizo ambazo zitavunjwa na zile ambazo ziko katika hali mbaya nafikiria kigezo cha hali mbaya watathmini wetu watakapokwenda pale ndio watakaona kama hii inastahiki na hii haistahiki.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Kampuni ya Prismo na ujenzi wa barabara hii aliyoisema yeye haihusiani na ninachotaka kumuhakikishia kwamba kama nilivyojibu suala la msingi ni kwamba mimi mwenyewe binafsi nimetembelea Pemba katika eneo ambalo analizungumza Mhe. Mwakilishi na wakati tulipokwenda tulizungumza na wajenzi moja kwa moja na taarifa ambazo wametupa sisi kama wizara tumeridhika nazo kwamba tatizo kubwa kama nilivyosema mwanzo ni kuwa vyombo vyetu vya ujenzi ni vibovu. Mhe. Spika, kitu ambacho kinasababisha wakati mwengine kuchelewa kwa kazi zetu.

Mhe. Spika, kwa maelezo ya ziada kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe hivi sasa tuna ujenzi wa barabara ya Kinazini Bububu, lakini ujenzi wa barabara hii unasaidiwa na wenzetu wale ambao wapo kwa kuazima zana zile za ujenzi ndio tunafanikiwa vizuri, lakini kama ingekuwa sio wao basi kuitoa ile lami ya juu na kufanya *grading* upya ingetuchukua muda mrefu. Kwa hivyo, kwa upande wa Jimbo la Kiwani kama nilivyosema kwamba tayari zana zimeshanunuliwa

mpya kwa hivyo nataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi aondowe wasi wasi huo kwamba barabara yake itakamilika tena kwa wakati.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri mimi naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mradi wa barabara sita za Kusini Pemba tulielezwa kama unatarajiwa kukamilika katika miaka mitatu mpaka hapa tulipo kama sikosei mwaka mmoja umeshamaliza. Mhe. Spika, tukifanya tathmini ni kwamba hatujapata hata *one third* ya ule mradi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri atatuhakikishia vipi kwamba miaka miwili hii iliyobakia ataweza kuzikamilisha barabara zote sita.

Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba tumetoa ahadi kuwa barabara hizo zingejengwa katika miaka mitatu, yaani kukamilika kwake. Kutokana na hali halisi iliyopo bado imani hiyo tunayo kwamba tutamaliza kwa wakati, kwani kati ya barabara hizi sita ambazo zinajengwa kwa ufadhili wa *NORAD* tayari barabara tatu za Mgagadu – Kiwani, Mtambile – Mwambe pamoja na Mzingani – Wambaa zimeshaanza ile hatua ya awali.

Kwa hivyo, tunategemea kwamba tutakamilisha kazi hiyo haraka iwezekanavyo na pale ambapo patatokea kazi imezorota basi sisi kama wizara hatutosita kwenda kuona nini tatizo na kama linatokana na wizara basi tutahakikisha kuwa tatizo hilo linaondoka mara moja, hasa kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha yuko makini sana kuona jambo lolote linalohusiana na mambo ya barabara basi anakuwa ni msimamizi mzuri.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, miongoni mwa barabara hizi sita ni barabara ya Mtambile – Kangani, na barabara hii imeanza kubomolewa kwa nia ya kujengwa, lakini mwenendo wa ujengaji wa barabara hii unavunja moyo sana. hivi sasa mvua inaponyesha sikwambii kwenda kwa gari hata kutembea kwa miguu ni tatizo.

Sasa sijui Mhe. Waziri atawahakikishia nini wananchi wanaokaa katika maeneo haya ili kuepukana na balaa wakati wa mvua za masika zitakapoanza kuhakikisha kwamba ile sehemu iliyobomolewa inatengenezwa ili iweze kupitika wakati huu wa mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba wakati wa masika katika barabara ambazo ni za kifusi zinakuwa na matatizo kupitika. Kwa hivyo, wizara yangu itahakikisha kuona kwamba maeneo yale yote ambayo yanaonekana yana matatizo makubwa na yanaweza kusababisha usumbufu na magari kutokupita, basi yanafanyiwa kazi

haraka ili kuona usumbufu huo haupatikani na wananchi wende na shughuli zao kama kawaida.

Nam. 54

Wanafunzi Kuacha Mitihani

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Pamoja na matokeo mazuri ya mitihani ya Darasa la Saba na Darasa la Kumi na Mbili 2009, kuna tatizo kubwa la wanafunzi wasiofanya mitihani yao. Kwa mfano, wanafunzi wapatao 1,672 wa Darasa la Saba na wanafunzi 1,397 wa Darasa la Kumi, hawakujitokeza kufanya mitihani.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako imefanya utafiti kujua sababu zilizowafanya wanafunzi hao wasifike vituoni kufanya mitihani yao?

(b) Je, ni maeneo yepi ambayo tatizo hilo lipo zaidi kuliko maeneo mengine?

(c) Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi kama hao ili waweze kurudi skuli na kufanya mitihani yao?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la Mhe. Mjumbe Nam. 54, kwanza napenda niweke wazi suala ambalo limejitokeza jana kuhusu Skuli ya Ukongoroni kuwa iko Wilaya ya Kusini.

Mhe. Spika, Skuli ya Ukongoroni, Michamvi pamoja na Charawe ziko Wilaya ya Kati, lakini zinapata huduma ya kielimu kutoka Wilaya ya Kusini hivyo ndio maana ikaelezwa kuwa iko Wilaya ya Kusini.

Baada ya maelezo hayo machache, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 54 lenye sehemu (a) ,(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wanafunzi 1,672 wa darasa la saba na wanafunzi 1,397 wa Kidato cha Pili wa mwaka 2009 wa skuli mbali mbali hawakufanya mitihani hiyo.

a) Wizara haijafanya utafiti rasmi wa kuelewa kujua sababau za wao kutofanya mitihani hiyo. Hata hivyo, taarifa zilizoelezwa na Walimu Wakuu zimeonyesha kuwa baadhi ya wanafunzi hao

hawafanyi mitihani kutokana na ama ugonjwa au utoro wa muda mrefu. Wanafunzi ambao huwa ni wagonjwa, huiarifu wizara na huomba kurejea masomo mara tu wanapopata nafuu au kurudi kufanya mitihani kwa mwaka unaofuata.

b) Wanafunzi wengi wasiofanya mitihani hasa kutokana na utoro wanatokea katika Skuli za Mkoa Mjini/Magharibi hasa katika skuli zenye wanafunzi wengi kama vile Skuli ya Haile Sellasie, Mwembeladu na Mwanakwerekwe "A".

c) Baadhi ya wanafunzi wasiofanya mitihani kwa sabaabu za ugonjwa, wanaruhusiwa kurudia masomo au kufanya mitihani katika mwaka unaofuata baada ya kuthibitishwa na daktari. Baadhi ya wanafunzi ambao hawakufanya mtihani wao kwa sababu za utoro, hujiunga na madarasa ya elimu mbadala au masomo ya kujiendeleza.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sna Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri maswali ya nyongeza yenye kifungu a, b na c.

(a) Mhe. Spika, hivi ni kweli utoro na maradhi yanaweza kufikia kiwango hiki cha watoto karibu elfu nne kwa mwaka huu?

(b) Ikiwa hivyo sivyo, Mhe. Waziri anaweza kukubaliana na mimi kwamba michango mbali mbali inapelekea kurudisha nyuma watoto ikiwemo ile ya kuchangia kufanya mitihani?

(c) Ni hatua gani atachukua za kuona watoto hawa nao wanapata haki yao ya kupata elimu ili waweze kuwa na maisha mazuri siku za usoni?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi aliuliza kwamba ni kweli utoro na maradhi ndio sababu tosha? Kama nilivyojibu katika kipengele (a) wizara haijafanya utafiti rasmi wa kuonesha sababu halisi ya wao kutofanya mitihani. Lakini tumesema kwamba taarifa tunazozipata kutoka kwa walimu wakuu zinaonesha kwamba utoro na maradhi ndio ambayo yanasababisha watoto hao wasifanye mitihani.

Lakini swali lake la (b) Mhe. Spika, sikubaliani naye kwamba michango ndio sababu ya kwamba watoto hawa wasiende kufanya mitihani.

Na (c) Mhe. Spika, wizara yangu inachukua hatua mbali mbali za kuona kwamba vijana hawa wanarudia skuli ikiwemo kushirikiana na jamii pamoja na

kamati za skuli kuona kwamba vijana wote ambao wametoroka skuli basi wanarejea na kuna madarasa maalum ambayo tumeyaandaa kwa shughuli hiyo, kama vile elimu mbadala kama nilivyozungumza katika kipengele (c). lakini pia ni kwamba wanafunzi hao wanapatiwa fursa wakiwa wagonjwa kurejea tena skuli ama kufanya mitihani.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza mimi napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri kutokana na majibu yake hii iliyotajwa hapa ni asilimia ngapi ya wanafunzi wote ambao wamefanya mtihani?

Lakini pili kwa sababu kuna mtiririko katika skuli wa kitaalamu unaoitwa *drop out* na hii inaripotiwa kwamba ni utoro. Lakini mimi nakumbuka Mhe. Spika, kwamba wanafunzi wanapofanya mitihani huwa wanasajiliwa. Kwa hivyo, ina maana utoro huu unatokea ule mwaka wa mwisho tu, idadi hii ni ule utoro wa mwaka wa mwisho wa masomo. Kwa sababu kama ingekuwa ni mwaka mwengine ingekuwa hawakuripotiwa kwa sababu wasingesajiliwa kama ni wafanya mitihani.

Kwa hivyo, ina maana utoro huu unatokea ule mwaka wa mwisho wa kufanya mitihani. Sasa hebu atueleze Mhe. Naibu Waziri au waziri mwenyewe ni kitu gani hasa kinachofanya zaidi ya sababu zile zinazotajwa kuhusiana na tukio lote la utoro kama huu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru, nilikuwa na hamu ya kujibu kwa sababu sijawahi kujibu swali toka mkutano huu ulivyoanza na hasa akiuliza Mhe. Rashid Seif hupenda nimjibu mimi.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yote na maelezo. Naomba nitoe nyongeza kidogo tu. Kwanza suala la kupambana na utoro si jukumu la Wizara ya Elimu peke yake, suala la kupambana na utoro ni la jamii kwa ujumla. Hivi karibuni nimeanza ziara mimi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba sehemu zote za mikutano nimehimiza sana suala zima la kamati za skuli kusimamia nidhamu, na moja katika jambo ambalo nimelizungumza kwa nguvu zangu zote ni suala la utoro. Mheshimiwa anauliza ni asilimia ngapi?

Asilimia ya utoro sasa hivi kwa upande wa darasa la saba ni asilimia 7.4 hivi na darasa la kumi ni asilimia hiyo hiyo 9. Lakini pia asifikirie kwamba utoro ule uko kwenye madara ya saba tu na kumi, Mhe. Spika, hata darasa la kwanza utoro upon a la pili. Lakini kipindi hiki tunajuwa utoro upo kwa sababu kama alivyosema yeye mwenyewe tunafanya *registration,* tunapofanya *registration* huwa wanaingia Januari pale, Febuari wengine wanaanza ku-*drop* pale.

Ikiwa ni maradhi na ikiwa *one third* ya kipindi ambacho alikuwa darasani, *two third* hakupata basi taratibu zetu zinaruhusu mwanafunzi yule arejee mwaka mzima. Lakini ikiwa amesoma *two third* na amebakisha *one third* basi mwanafunzi yule huwa anaruhusiwa kuja kufanya ule mtihani tu kwenye darasa la kumi. Lakini kwenye darasa la saba ni *basic education* haina tatizo hata kama atatoroka mwaka mzima basi tuna wajibu sisi kumpatia taaluma ile.

Sababu za kimsingi Mhe. Spika, ziko nyingi amezieleza Mhe. Naibu Waziri wangu, lakini inawezekana matatizo mengine ni *low awareness* katika baadhi ya maeneo, lakini pengine na harakati nyingi katika maeneo. Kasema Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake la wizara kwamba maeneo ya *Haile Sellasie,* Mwembeladu na Mwanakwerekwe ndio umekithiri utoro ule. Ni kweli, mimi nashangaa wakati mwengine kwanini maeneo haya ya mjini. Lakini kilichojitokeza ni kwamba watoto wanaondoka majumbani matokeo yake hawafiki skuli wanajishughulisha na kazi nyengine za kuhangaika hangaika.

Sasa hili ni jukumu ambalo sote wenyeviti wa kamati, masheha, wawakilishi, wabunge na sisi Wizara ya Elimu basi tusaidiane katika kuhakikisha kwamba suala hili tunapambana nalo kwa sote.

Mhe. Spika: Swali hili limechukua muda hivyo tuendelee.

Nam. 17

Mpango wa Kupambana na Kuondosha Malaria

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Kwa muda sasa tangu Zanzibar uanzishwe mpango wa kupambana na Malaria, tumekuwa tukipewa taarifa za mafanikio ya kutokomezwa kwa ugonjwa huo na taarifa hizo zinaeleza kwamba kiwango cha ugonjwa huo kilichopo Zanzibar ni chini ya asilimia 3 (3%). Lakini wananchi wanaona bado ugonjwa upo kutokana na kusumbuliwa na homa.

(a) Mhe.Waziri ni upi ukweli wa hoja ya serikali inayodai kutokuwepo kwa ugonjwa wa malaria?

(b) Baadhi ya wananchi wanadai kuwa tamko la serikali la kusema ugonjwa wa malaria haupo ni shindikizo tu la wafadhili hususan Marekani. Je, upo ukweli wa jambo hilo?

(c) Kwa nini mgonjwa anapokwenda kwenye vituo vya afya na hospitali za serikali kupima malaria huambiwa hawana malaria, lakini

wanapokwenda kwenye vituo vya afya na hospitali za binafsi huambiwa wana malaria?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 17 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, napenda kuwajuilisha Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa ugonjwa wa malaria bado upo Zanzibar na haujaondoka kabisa kama watu wengine wanavyofikiria. Taarifa sahihi ni kwamba, ugonjwa huu umeshuka sana kutoka asilimia 14 ya mwaka 2003 hadi asilimia 0.8 ya mwaka 2007. Aidha, takwimu za hivi karibuni 2009 zinaonesha kushuka kwa ugonjwa kwa asilimia 0.4 Takwimu hizi zinatoa sura ya kwamba vimelea vya ugonjwa wa malaria bado vinapatikana Zanzibar na uwezekano wa maambukizo kutoka mtu mmoja hadi mwengine inawezekana.

b) Mhe. Spika, wafadhili wa kazi za kupambana na malaria si Marekani peke yake, wapo na wengine kama Mfuko wa Fedha wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, TB na Malaria, Serikali ya Italy na wengineo na wote hawa hawajatoa shindikizo lolote kwa wizara yangu, kuwa itoe tamko la kutokuwepo kwa ugonjwa wa malaria. Takwimu zinatolewa na zinakusanywa na watendaji wa wizara yangu katika vituo vya afya na hospitali na kuhakikiwa na Kitengo cha Mfumo wa Taarifa za Afya (*Health Management Information System*).

Mhe. Spika, napenda kusisitiza kwamba ugonjwa wa malaria haujifichi wala hauwezi kufichwa sehemu yoyote ulipo utajitokeza tu, kwani mbu wanaosambaza ugonjwa bado wapo.

c) Mhe. Spika, malalamiko yapo na ningependa kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

- Uchunguzi wa vimelea vya malaria ni fani maalum na inahitaji elimu ya kutosha na uzoefu wa muda mrefu.

- Watendaji wa serikali katika vituo vya afya na hospitali hupata mafunzo ya kuwakumbusha mara

kwa mara na hivyo kuongeza umahiri wao na kuvigundua vimelea kwa kutumia darubini.

- Nafasi hii ya mafunzo mara kwa mara si aghalabu kupatikana katika sekta binafsi na kupelekea kutokuwa na taaluma husika ya maradhi haya.

- Vifaa vinavyotumika vinatakiwa viwe katika kiwango kinachotakiwa na hali hii inawezekana ikakosekana kwa baadhi ya hospitali na kliniki za sekta binafsi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia haki yangu. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwa malalamiko yote na baadhi ya watu wakienda hospitali za serikali wanaambiwa malaria hawana na katika hospitali za binafsi wanaambiwa yapo. Na kwa kuwa amesema kuwa taaluma ya serikali ni kubwa zaidi kuliko ya watu binafsi. Ni juhudi gani wizara itafanya ili vituo vyetu vya binafsi wapate elimu sawa sawa na vya serikali ili majibu kwa wagonjwa yawe yanakwenda sambamba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, wizara yangu juhudi inafanya na itaendelea kufanya. Kwa sababu kuna chombo maalum cha bodi kwa hospitali binafsi, chombo hiki ndicho kinachoshughulika na mambo ya hospitali binafsi. Kwa hivyo, tutachofanya wizara yetu kukishauri zaidi chombo hiki ili kiweze kufanya kazi zake vizuri na wawashauri hao wenye hospitali binafsi basi wale wafanyakazi wao katika sehemu zao za hospitali waweze kuwapatia taaluma ili waweze kwenda na wakati.

Mhe. Salim Abdala Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Nianze kwa kutoa pongezi kwa wizara namna inavyojitahidi kupambana na ugonjwa huu wa malaria kwa kutia madawa majumbani, kutoa vyandarua vya bure na kadhalika.

Lakini tukiangalia sisi tunatibu malaria wanaokuja majumbani, lakini mbu hawa wana sehemu zao maalum ambazo huwa wanazaana, kwenye vidimbwi na kadhalika. Na kwa sababu wanazaana itakuwa malaria haiondoki maisha, basi sijui kwa kuondoa moja kwa moja maradhi haya serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuona kuwa haya mazalio ya mbu nayo yanafanyiwa kazi ili na hawa mbu wenyewe watokomee moja kwa moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza nichukue hizi pongezi ambazo kaipongeza serikali, tunazipokea na sisi kwa mikono miwili kwa sababu ameona jitihada ya serikali katika kutokomeza

kabisa suala hili la malaria ambalo lilikuwa linawathakili wananchi wetu kwa muda mrefu.

Pili Mhe. Spika, kweli tunaelewa sote mazalio ya mbu yamo katika vidimbwi na sehemu mbali mbali kama kwenye maji yanayowekwa kwenye vifuu, vibati na maeneo mengine sote tunaelewa hilo. Kwa hivyo, jitihada ya serikali au wizara ni kutoa elimu ya kuhakikisha kuwa sisi tunafanya suala la kumaliza malaria lakini tushirikiane na wenzetu wananchi pamoja na viongozi kuelimisha suala hili liweze kumalizika kabisa. Na hili halikuanza leo Mhe. Spika, suala la elimu hii limeanza muda mrefu kuelimishwa kuwa maeneo yote yale ya vidimbwi vinavyotuama maji na maeneo mengine yote ambayo tunahisi hapa panaweza kutoka mazalio ya mbu basi jitihada zinafanyika.

Kuna baadhi ya wakati hata Mhe. Waziri wangu aliwahi kuzindua shughuli moja ya kupita kutia dawa kwenye vidimbwi. Nadhani hili suala Mwenyezi Mungu akitujalia kama uwezo utakuwepo basi tutasaidiana katika elimu pamoja na kutiwa dawa katika vidimbwi ili mazalio ya mbu yasiweze kuendelea.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kweli sote tunaunga mkono juhudi ya Wizara ya Afya kupambana na malaria, na kwa kiasi fulani tumeona kwamba mafanikio yapo tena makubwa sana. Hivi sasa upo mradi wa Maliza Malaria, lakini naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Katika wilaya 10 wilaya gani imemaliza malaria na wilaya gani bado inaongoza kuwa yapo ili juhudi na nguvu zielekezwe huko ili kuyaondoa kabisa malaria.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza na yeye nianze kuchukua pongezi zake na kutuunga mkono kabisa katika suala hili la kuwa wizara inajitahidi kwa nguvu zote. Kwa hivyo, tunamshukuru sana kwa pongezi zake.

Suala la Mradi huu wa Maliza Malaria hivi sasa ndio tunaendelea nao na umeanza Pemba halafu baadae umeendelea Kaskazini ‘A’, ‘B’ na Kusini, (Mkoa wa Kaskazini na Kusini). Kwa hivyo, hili suala sasa hivi ndio tunaendelea nalo na mradi bado unaendelea Mkoa wa Mjini Magharibi hatujafika.

Hata hivyo, hatuwezi tu sasa hivi kusema tu kwa vile shughuli hii inaendelea kuwa sasa hivi tumeshakuwa na tathmini ya wilaya gani inaongoza na wilaya gani haiongozi, suala hili bado tunaendelea nalo. Baada ya kumalizika wataalamu wetu watakaa watufanyie tathmini waone kuwa wilaya gani mpaka sasa hivi imemaliza suala hili la malaria. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 41

Ushindi wa *Zanzibar Heroes*

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu *Zanzibar Heroes* ilishiriki Mashindano ya *Challenge* ya Afrika ya Mashariki huko Kenya na kuibuka na ushindi wa tatu baada ya kuwafunga ndugu zetu wa Tanzania Bara goli moja kwa bila, katika kutafuta mshindi wa tatu na kupokelewa na Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

(a) Je, Mhe. Waziri, baada ya mapokezi makubwa, vijana wetu wamepewa tunzo gani kwa kazi nzuri waliyoifanya?

(b) Je, wizara yako ina mikakati gani ya kuiwezesha timu yetu vizuri zaidi hapo baadae?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wazima wa afya kujumuika tena katika kikao hiki leo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 41 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba kusema kwamba timu yetu ya *Zanzibar Heroes* ilisherehekea sana pale ilipoifunga timu ya Tanzania Bara na kupata ushindi wa tatu. Sherehe hizo zilikuwa kubwa hususan baada ya timu ya Tanzania Bara kutoa changamoto maalum kwa timu ya Zanzibar kuwa ni wala urojo na hawakuwa na kiwango chakufaa au kupaswa kucheza mpira huko. Na wao walisema ni wana wa brazil na sisi tumewathibitishia kwamba ni Wazanzibari.

Mhe. Spika, kama nilivyokwishajibu jana katika swali Nam. 40 pia naomba nirudie kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba:

(a) Baada ya vijana wetu kufanya vizuri kwenye mashindano ya *challenge* huko Nairobi, Kenya waliandaliwa mapokezi maalum waliporejea hapa nyumbani Zanzibar.

Mhe. Spika, serikali iliizawadia timu ya *Zanzibar Heroes* jumla ya Dola za Kimarekani 13,700 sawa na shilingi za Kitanzania milioni ishirini na tisini na sita elfu na pia timu yetu ilipata fursa maalum ya kwenda Ikulu na kula chakula rasmi cha mchana pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani Abeid Karume.

(b) Mhe. Spika, lengo na mikakati ya wizara ni kutoa fursa nzuri kwa timu zetu kujiandaa vizuri kwa kuwapa nafasi ya kufanya ziara za mafunzo nje ya nchi na kupata maandalizi mazuri ya mafunzo hapa hapa nchini kabla hawajashiriki mashindano kama hayo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, bado mimi napongeza tu timu yetu hii ya *Zanzibar Heroes* kwa shughuli nzito waliyoifanya hasa tukilinganisha kwenye utani wa jadi baina ya Timu ya Taifa ya Tanzania Bara na Timu ya Taifa ya Zanzibar.

Lakini Mhe. Spika, maandalizi ni jambo la kwanza ili kujiweka vizuri huko mbele tunakokwenda, toka kurudi timu hii hadi kufikia leo kuanzia walimu na viongozi au walimu na wachezaji, angalau wamekutana mara ngapi kuweka mkakati wa huko mbele twendako?

Pili kwakuwa hilo nililolizungumza katika swali langu la kwanza ni zito, hivyo wizara kupitia *ZFA* ina mpango gani wa makusudi kuanzisha utaratibu wa kutafuta timu kutoka nje kuja hapa kufanya majaribio au mashindano ili kuiweka vizuri timu ile kwa siku zijazo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwana kabisa nakubaliana naye juu ya utani wa jadi kati ya Timu ya Tanzania Bara na Timu ya Zanzibar, na ndio maana nikasema kwamba Zanzibar ilisherehekea sana kupata ushindi huo kutoka Tanzania Bara kama Mungu akitujaalia Yanga itakavyosherehekea Jumamosi hii inayokuja. Ingawa wenzao wameshachukua ushindi tayari, lakini naamini yanga itasherehekea zaidi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane naye kwamba timu haikukutana na sababu maalum ni kwamba timu yaani makocha pamoja na wachezaji baada ya kurudi tu walikuwa na ratiba zao za Ligi Kuu ya Zanzibar. Kwa hivyo, kila mchezaji alirudi timu yake na tunajua Hemed Moroco ana timu yake ambayo anaifundisha. Kwa hivyo, wao walikuwa na ratiba hiyo ambayo imewafanya wasikutane pamoja hadi pale ambapo *ZFA* itawaita tena pamoja kupanga mkakati mwengine utakaotokezea kama huo.

Hivi sasa timu zote, wachezaji wote, makocha wote wapo katika ratiba zao za ligi kuu na kila mmoja sasa hivi anashughulikia na timu yake ili aweze kupata ubingwa wa Zanzibar na kwenda kushiriki katika mashindano ya shirikisho pamoja na Klabu Bingwa za Afrika.

Mhe. Spika, jengine hata yule kocha tuliyempata mtaalam Ndugu Abdulfatah yeye pia aliazimwa na timu ya Miembeni akawa anaifundisha Miembeni kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Kwa hiyo, kwa ujumla hata yule kocha ambaye alikuwa anasimamia Timu ya Taifa moja kwa moja nae pia aliombwa kuazimwa na hivi sasa yupo katika ratiba ya ligi ili kutafuta vipaji. Mara tu ligi itakapomalizika au itakaposimama na mashindano hayo kuwa tayari naamini vipaji hivyo vimeshaonekana wataitwa wachezaji wote na makocha wote tena watakaa pamoja na kupanga mkakati.

Mhe. Spika, naomba kumuondoshea hofu Mhe. Mwakilishi kwamba hata *Copa Coca Cola* itakuja tena Baraza la Wawakilishi Mwenyezi Mungu akitujaalia mwaka huu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tunaipongeza sana serikali kwa juhudi yake iliyofanya ya kuipa motisha Timu ya Taifa ya Zanzibar na wachezaji kila wanapopata motisha huwa wanazidisha ari. Sasa kwa juhudi hizo pamoja na juhudi nzuri sana za Rais wa Zanzibar kuwapongeza na kuwakaribisha wakenda kula chakula cha mchana pamoja Ikulu.

Je, Mhe. Waziri atafanya vipi kuwashajiisha matajiri, makampuni na mashirika makubwa makubwa yaliyopo Zanzibar, ili na wao wawe na moyo wa kuwapa zawadi wachezaji wetu wa Zanzibar wazidi kuwa na moyo wa kufanya vizuri zaidi na kulipatia sifa taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, hivi karibuni kama siku nne zilizopita tulikuwa tunafuatilia hizi habari za michezo. Ndugu zetu kutoka Pemba wao walikuwa wanasherehekea sana hususan timu ya Jamhuri na Chipukizi kwa kuwafunga *Ocean View.*

Mhe. Spika, ningependa sana kuchukua taaluma kutoka kwa ndugu zetu Pemba kwamba waliwapa motisha gani hawa timu za Chipukizi na Jamhuri hata kuweza kushinda timu kama hiyo kubwa ambayo ina kocha kutoka Senegal hivi sasa.

Mhe. Spika, bado jitihada zitaendelea za kuwashajiisha hawa matajiri pamoja na kampuni mbali mbali kutoa motisha. Lakini ninachotaka kusema kwamba motisha hautokani na fedha tu au tajiri, unatoka kwenye moyo.

Nam. 88

Hoteli ya Bwawani

Mhe. Mkongwe Nassor Juma – Aliuliza:-

Hoteli ya Bwawani ni moja ya Taasisi za Serikali ambazo zinajitegemea lakini inawasilisha taarifa zake za mapato na matumizi Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Waziri, kwa kuwa Bwawani ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea. Kwa nini haijaundiwa Bodi kisheria itakayosimamia utendaji wake na kupokea taarifa za kiutendaji za hoteli hiyo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Hoteli ya Bwawani inawasilisha taarifa za mapato na matumizi ndani ya Idara ya Mipango na Sera kwenye Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Hii ni kutokana na kwamba Hoteli ya Bwawani ni kitengo kinachosimamiwa chini ya Idara hiyo ya Mipango na Sera. Kwa maana hiyo, Hoteli ya Bwawani si taasisi inayojitegemea.

Ili iweze kuundiwa Bodi ya Usimamizi inabidi kwanza itungiwe sheria ya kuifanya Hoteli ya Bwawani kuwa Shirika kulingana na Sheria ya Mashirika ya Kitengo cha Mitaji ya Umma.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani imejengwa miaka 38 iliyopita. Sasa hivi hoteli nyengine nyingi zimejengwa lakini bado hoteli hii ina hadhi yake na ni kubwa kuliko hoteli zote zilizojengwa hapa katika Mji wa Zanzibar.

Hizi zilikuwa ni fikra za Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Hayati Karume alikuwa na *vision* na alijua kwamba nchi hii itakwenda kwenye utalii. Pale mbele tumeweka sanamu lake kumuenzi na tumesema sisi Mzee Karume amekufa lakini fikra zake ziko pale pale na tutaendelea kuzienzi.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni hali ya hoteli ile kuwa ni mbaya sana.

(b) Haoni kwamba hoteli ile ilivyodhalilika ni kulidhalilisha jina la Hayati Mzee Abeid Amani Karume.

(c) Haoni kama hiyo enzi ndio tumeiondosha.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Hoteli ya Bwawani ina historia ndefu na ilijengwa miaka hiyo ya nyuma ya mwanzo mwanzo wa miaka ya 70. Katika kuiendeleza hoteli hii ilipitia historia ndegu kati kati hapa. Hoteli ya Bwawani imeshawahi kupewa makampuni kadhaa ili kuiendeleza kufikia kiwango kizuri kwa nia ya kuenzi jina la aliyeanzisha hoteli hii.

Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani imepita mikononi mwa kampuni za *OBEROI, Tudor Marketing* ya *Channel Islands* na Kampuni ya *Zee Hotel Management.* Lakini wote hawa hawakuikuza na kuiweka kwenye hadhi inayotakiwa mpaka mwaka 1997 Hoteli ya Bwawani ikarudi mikononi mwa serikali. Katika njia hiyo ya kuenzi jina la Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa sasa hivi serikali imehisi Hoteli ya Bwawani ibakie mikononi mwake.

Mhe. Spika, nakiri kwamba Hoteli ya Bwawani iko katika hali mbaya kwa nje, lakini Uongozi wa Hoteli unajitahidi kuitengeneza ndani kwa mtaji kidogo ambao inakusanya.

Lakini papo hapo Hoteli ya Bwawani hupangiwa viwango vya kuchangia serikalini na haijatokea hata mwaka mmoja hoteli hii kushuka chini ya kiwango kinachopangwa kuchangia.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba serikali haina nia ya kudhalilisha jina la Marehemu Mzee Abeid Amani Karume bali tunajitahidi kutunza jina lake na kutunza yale ambayo ameyaanzisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na kasoro kubwa ambazo zimo katika Hoteli ya Bwawani na hasa katika suala la usimamizi wa mapato na matumizi yake ni kuongozwa kwa muda mrefu na Kaimu Meneja kinyume na Kanuni za Utumishi *(General Orders).*

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba umeshafika wakati sasa kutafuta mtu mwenye maarifa na ndani ya Zanzibar hii wamo ambao wana uwezo wa kushughulikia hoteli hii na kumpa nafasi bila ya kuongozwa na Kaimu Meneja kwa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba ni kipindi kirefu sasa kama miaka mitatu au zaidi Hoteli ya Bwawani inaongozwa chini ya jina la Kaimu Meneja. Hii haina maana kwamba Kaimu

Meneja anayeongoza hana maarifa. Ni mtu mwenye maarifa na ndio sasa hivi anayeipeleka vizuri Hoteli ya Bwawani. Linalotukwaza ni Kanuni za Utumishi, kila tunapoomba kumthibitisha Idara ya Utumishi wanakuwa na vikwazo hivi na vile.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Wajumbe wako kwamba bajeti ijayo hakutakuwa na Kaimu Meneja kutakuwa na Meneja kamili wa Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alikuwa na mawazo ya kuwaonesha njia Wazanzibari kwa uwekezaji tofauti. Lakini baada ya kufariki yeye na tukagundua hapa kati kati hakuna mtu anayeyaendeleza yale na hivyo baada ya muda mdogo tu serikali ikatengeneza Sheria ya Mitaji ya Umma na baadhi ya mali za serikali zikabinafsishwa.

Je, kitu gani kinachozuia Hoteli ya Bwawani isibinafsishwe kama zilivyobinafsishwa mali nyengine za umma.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba mali nyingi za serikali zimebinafsishwa, lakini haina maana kwamba kubinafsisha ndiko kutakakokuza maadili ya serikali. Kama nilivyosema Hoteli ya Bwawani tuliibinafsisha mara tatu. Walipewa *OBEROI*, wakapewa *Tudor Marketing* wa *Channel Islands*, wakapewa *Zee Hotel Management* na wote hawakuifikisha pale tulipotaka. Badala yake huyu wa mwisho aliondoka na akaacha madeni ya milioni 200.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi kama nilivyojibu kwamba serikali imeamua Hoteli ya Bwawani ibakie mikononi mwake. Hoteli hii kubakia mikononi mwa serikali inasaidia serikali kwa kiasi kikubwa. Katika nchi yoyote ile lazima kunakuwa na kitu kama kile. Kunakuwa na hoteli inabaki mikononi kwa serikali kwa kazi za serikali, au kunakuwa na *Guest House* yenye hadhi ya hoteli lakini inatumika kwa kazi za serikali.

Mhe. Spika, kwa sasa hivi serikali imeamua Hoteli ya Bwawani ibakie mikononi mwake ili itumike kwa kazi mbali mbali za serikali na zetu binafsi humu ndani.

Nam. 12

Uanzishwaji wa *Offshore Banking* Zanzibar

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza:-

Katika Dira 2020 neno la *Offshore Banking* (Benki za Ufukweni) limetajwa kuwa ni miongoni mwa mikakati ya kukuza uchumi nchini. Kwa vile hivi sasa wawekezaji wameitikia wito wa kuwekeza Zanzibar hasa katika sekta ya Utalii.

(a) Je, Mhe. Waziri, serikali imefikia hatua gani katika uanzishwaji wa benki za aina hiyo.

(b) Je, uanzishwaji wa *Offshore Banking* hatutakwenda kinyume na mikataba ya *EAC* na *SADC*.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba hili neno *Offshore Banking* (Benki za Ufukweni) limetajwa kuwa ni miongoni mwa mikakati ya kukuza uchumi hapa nchini kwetu. Dira 2020 imeweka mkakati huo kwani ni imani yetu kwamba kuanzishwa kwa benki hizo hapa nchini kutaongeza pato la Taifa na ajira kwa wananchi wetu.

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba uanzishwaji wa Benki za Ufukweni unafanyika hapa nchini. Mchakato wa uanzishwaji wa huduma hizo unaendelea ambapo hivi sasa serikali inafanya mazungumzo na Kampuni ya Kimataifa ya Usajili wa Huduma za Kifedha *(Registrar International Services Ltd - RISE)* ambayo imeonesha nia ya kutaka kushirikiana na serikali katika kufanikisha suala hili kwa kutoa huduma za usajili wa makampuni ambayo yatakuwa yanafanya shughuli zake hapa Zanzibar.

b) Mhe. Spika, serikali inaelewa vyema kuwa kabla ya kuanzisha *Offshore Banking* sheria mbali mbali za Kimataifa lazima zipitiwe ili kutokwenda kinyume na mikataba ya *EAC* na *SADC*. Uanzishwaji wa *Offshore Banking* utaongozwa na Sheria za Biashara za Kimataifa.

Mhe Spika, ili kufanikisha uanzishwaji wa benki hizo kutakuwa na haja ya kuanzisha mamlaka mpya ya Biashara za Kimataifa itakayoshughulikia benki au kampuni zitakazojitokezea katika masuala hayo. Mhe. Spika, baadhi ya sheria ambazo ni muhimu zinazotarajiwa kutungwa zinahusu Mikataba na Itifaki *(Protocols)* za *EAC* na *SADC* ni kama vile *International Service Provider Act, International Business Companies Act, International Trust Act* na *The Foundation Act.*

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini hata hivyo nina swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wawekezaji siku zote hutaka usalama kwa wao wenyewe pamoja na fedha ambazo ndio hasa wanazokuja kuzitafuta. Lakini siku za karibuni tumesikia wawekezaji wetu hasa wa mahoteli sehemu za Kendwa wameibiwa, pia juzi Wilaya ya Kati katika Hoteli ya Samaki wameibiwa.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kitendo cha kucheleweshe kuwawekea taasisi za usalama wa fedha katika maeneo haya kutaviza uwekezaji.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mmwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na matukio ya wizi wa fedha katika sehemu mbali mbali za mahoteli. Serikali kwa kweli imejitahidi sana kuweka ulinzi wa Polisi na tunawashukuru sana Makamanda wetu wa Mikoa nafikiri wamejitahidi na wamefanya mpaka ulinzi jamii, ili kuwashirikisha wananchi wenyewe na mahoteli wenyewe wachangie yale masuala ya ulinzi. Wengine wamekwenda kukodi makampuni ya ulinzi yaliyopo. Nafikiri sasa kuna makampuni mbali mbali ya ulinzi yaliyopo hapa visiwani kwetu na wanafanya kazi nzuri sana za ulinzi.

Sasa cha kusisitiza tu ni mashirikiano zaidi na hasa ni elimu kwa wale wafanyakazi wenyewe. Kwa sababu mara nyingi sana kesi hizi ukizifuatilia utakuta upelelezi wa Polisi basi kwanza wanawakamata wale walinzi wa pale, hawana uhakika lakini wanawashuku kidogo. Kwa sababu wizi wenyewe unakuwa wa kiajabu ajabu unahisi hasa kwamba *clue* zinatoka pale.

Kwa hiyo, ni suala zima la kushirikiana ili tuweze kulifanikisha. Lakini kwa ujumla mashirikiano yaliyopo kati ya mahoteli yenyewe, serikali na walinzi wao ni suala la msingi sana.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, inatajwa kwamba uanzishwaji wa

Offshore Banking hurahisisha uharamia wa shughuli za biashara kwa kifedha ikiwemo *money laundering* na mambo mengine.

Je, hilo ni kweli. Ikiwa ni kweli Zanzibar katika kuelekea huko tumejitayarisha vipi kiutaalam, kiteknolojia na kiusalama kuona kwamba nchi yetu haiwi kituo muhimu cha money laundering na biashara nyengine ya fedha haramu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Said Ali Mbarouk na Waheshimiwa Wajumbe wengine wote watakubaliana na mimi kwamba sheria ile ya *Anti Money Laundering* tayari imeshawekwa sahihi na Mhe. Rais na tayari imeanza kutumika. Lakini sasa sheria ni suala moja, utekelezaji ni suala jengine. Naomba sana sote tushirikiane kwamba Zanzibar isiwe kituo hicho cha *money laundering*.

Mhe. Spika, kulikuwa na wasi wasi huo watu walikuwa wanaona kwamba kwa nini Zanzibar kuna mahoteli mengi, kiuchumi imenyanyuka haraka, mabenki. Kila mwenye benki leo anataka kuja kufungua tawi Zanzibar, haoni kwamba Zanzibar imenyanyuka kiuchumi. Wao wanashuku zaidi labda wasi wasi tu kwamba watu wanaghushi fedha na mengineyo.

Sasa hiyo si kweli, ukweli kwamba Wazanzibari wanafanya kazi na wana ubunifu wa kibiashara na ndio maana kwa kweli nchi imetutuka leo kila mmoja anataka kuja Zanzibar kutembea na anataka kuwekeza.

Mhe. Spika, Mhe. Samia Suluhu Hassan tunamshukuru sana *ZIPA* inafanya kazi vizuri kwa misingi iliyopo na yanakuja maombi mengi tu. Kama nilivyosema tuwe waangalifu kwa ardhi zetu tusiziuze bali tuwekeze na sisi wazalendo. Kwa hiyo, tutajitahidi kuhakikisha kwamba hili suala la pesa chafu lisiingie kwetu.

Hili tushirikiane sote Mhe. Said Ali Mbarouk, hasa wewe uliyekuwepo mpakani kule Gando inafaa utupigie debe zaidi.

Nam. 46

Mradi wa Kilimo cha Kumwagilia Maji

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na Kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na mambo yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muumba kwa kutupa uzima na afya njema tukaweza kukutana hii leo hapa tayari kwa kujadili Mswada wa Kufuta Sheria Nam. 8 ya Mwaka 1983 na Kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Taifa la Michezo ya Mwaka 2010.

Mhe. Spika, mswada ulioko mbeye yetu ambao ninauwasilisha hivi sasa tayari umekwishawasilishwa katika Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na ninawasilisha hivi sasa pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii Mhe. Ali Suleiman Ali (SHIHATA), Makamo Mwenyekiti Mhe. Ame Mati Wadi na Wajumbe wote wa Kamati kwa mashirikiano yao na msaada walionipa hadi kukamilisha matayarisho ya mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu ninaouwasilisha umegawika katika sehemu tano zifuatazo:

Sehemu ya Kwanza ni Jina fupi na kuanza kutumika. Sehemu ya Pili inahusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Michezo. Sehemu ya Tatu inaeleza Kuwepo Mikutano ya Wadau wa Michezo. Sehemu ya Nne inahusiana na Mambo ya Fedha, Matumizi na Ukaguzi wa Hesabu za Mapato na Matumizi na Sehemu ya Tano inahusiana na Mambo mengineyo.

Mhe. Spika, sheria iliyopo ambayo ni Sheria Nam. 8 ya Mwaka 1983 sasa ina umri wa miaka 27. Katika kipindi hicho kumetokea mabadiliko makubwa ya

shughuli za michezo. Kwa sababu hizo sheria hiyo iliyopo sasa imepitwa na wakati. Ili wizara iweze kukabiliana na mabadiliko hayo imeona ipo haja ya kuandika upya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo pamoja na kutunga kanuni zake.

Mhe. Spika, marekebisho makubwa yanayoambatana na marekebisho ya sheria hii ni haya yafuatayo:-

1. Kuongeza na kurekebisha tafsiri ya maneno kama inavyoonekana katika sura ya kwanza ya mswada huu.

2. Maelezo yanayohusu kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Michezo yanayohusu mambo yafuatayo:-

    (i) Kuundwa kwa Baraza la Taifa la Michezo chombo ambacho kinajitegemea, kinachoweza kushtaki na kushtakiwa na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.
    (ii) Maelezo kuhusu idadi ya Wajumbe wa Baraza na namna wanavyopatikana.
    (iii) Kazi na majukumu ya Baraza.
    (iv) Mamlaka na uwezo wa Baraza.
    (v) Namna ya kumpata Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti.
    (vi) Namna ya kuendesha mikutano na masharti yake.
    (vii) Uamuzi wa Baraza na masharti yanayopelekea kufikia katika maamuzi hayo.

3. Maelezo kuhusu kuwepo Mrajis wa Vyama vya Michezo, mamlaka na majukumu yake na namna ya kuunda Sekretarieti ya Baraza.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria hii utakapokubaliwa utafuta Mabaraza ya Mkoa na badala yake kuweka Mabaraza ya Wilaya. Kwa kufanya hivyo kutahatarisha utekelezaji wa shughuli za michezo na usikilizwaji wa malalamiko na rufaa na kesi za michezo.

Aidha, wadau wa michezo sasa wataunda kamati zao ambazo kazi zake zimeelezwa katika ukurasa wa 29 mpaka 30.

Mhe. Spika, Baraza sasa litakuwa na vyanzo halali vya mapato ambavyo zaidi ya ruzuku inayotolewa na serikali itakuwa na aina nyengine za mapato kama yafuatayo:-

Misaada kutoka kwa wafadhili, wahisani na kadhalika. Lengo ni kuondokana na kuwa na Baraza tegemezi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya ufafanuzi, sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wajadili mswada, waniongoze na hatimaye waukubali mswada huu ili michezo ipate kusonga mbele. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambae kwa rehema zake ameniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, nikiwa hai na afya njema, ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na Kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lina majukumu makubwa ya Kitaifa yakiwemo yale yaliyoelezwa katika kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, ambapo kifungu cha 88 (1) (a) kineleza yafuatayo:

”Baraza la Wawakilishi litakua na kazi ya kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo”.

Hivyo, ni wazi kuwa, Baraza hili ni muhimili muhimu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na majukumu hayo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa kifungu hicho cha sheria kinatoa fursa kwa Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ambapo linaweza kufanya hivyo kwa kutunga sheria mpya, kufuta sheria iliyopo na kutunga upya au kufanya marekebisho tu katika sheria fulani iliyopo ili iweze kukidhi mabadiliko ya kimazingira na wakati. Kwa kuzingatia utekelezaji wa hili, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imewasilisha mbele ya Kamati yetu Mswada wa sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na Kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Taifa la Michezo na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Kamati inatowa Shukurani za pekee kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ambaye pia ni Naibu Waziri Kiongozi Mhe. Ali Juma Shamhuna pamoja na watendaji wake wote kwa kuwasilisha Mswada huu mbele ya Kamati na kwa kuipa Kamati yetu mashirikiano makubwa wakati wa kuupitia na kuujadili Mswada wa sheria hii. Ushirikiano wao kwa kiasi kikubwa ulirahisisha upitishaji wa Mswada huu katika Kamati.

Mhe. Spika, Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa ushirikiano wao wa bega kwa bega waliouonesha kwa kuupitia kwa kina mswada huu na hatimaye kuupitisha, ingawa walikua katika mazingira magumu ya kiutendaji. Naomba niwatambulishe Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe Moh'd Ali Salim	-	Mjumbe
7.	Mhe. Haji Faki Shaali	-	Mjumbe
8.	Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	-	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
10.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
11.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
12.	Ndg. Salmin Amour Abdalla	-	Katibu
13.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Spika, kifungu cha 87 cha Katiba kinaeleza bayana kuwa lugha rasmi ya Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Kiswahili. Kifungu hicho kaneleza zaidi kuwa Kila Mswada, kila sheria inayotungwa na Baraza, kila sheria ya msingi au sheria inayopendekezwa chini ya chombo cha sheria na Baraza, na kila sheria halisi au inayopendekezwa, kusahihishwa au inayoendelea itaandikwa kwa lugha ya kiswahili na ikihitajika kwa lugha ya kiingereza.

Mhe. Spika, kifungu cha 26 cha kanuni toleo la 2009 nacho kinaeleza kuwa "majadiliano na shughuli za Baraza yataendeshwa kwa lugha ya kiswahili". Hata hivyo Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo kidogo kuhusu jambo hili. Miswada yote inaandikwa kwa kiswahili na inawasilishwa, kujadiliwa na hatimae kupitishwa katika Kamati na Baraza kwa Kiswahili. Lakini kwa bahati mbaya nakla ya sheria inayokwenda kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kupata kibali chake inatayarishwa kwa kiingereza. Hii ni kusema kwamba nakla zinazokwenda kupata saini ya rais sizo halisi zilizojadiliwa na kupitishwa katika Kamati na Baraza kwa kuwa Kamati pamoja na Baraza wamejadili na kupitisha nakla za Kiswahili.

Mhe. Spika, Kiujumla tunawaamini sana wataalamu wetu wanaokaa baadae kutafsiri kutoka Miswada ya kiswahili iliyopitishwa na kwenda katika kiingereza ili ikasainiwe. Hata hivyo, baadhi ya nyakati kumekuwa kunajitokeza tatizo ambapo baadhi ya vifungu vilivyo katika miswada ya

kiingereza ni tofauti kabisa na ile ya kiswahili ambayo ndiyo iliyojadiliwa na kupitishwa na Kamati pamoja na Baraza.

Ili kuepusha kasoro hii Mhe. Spika, Kamati yetu inashauri kuwa ama Mheshimiwa Rais apelekewe Miswada ya Kiswahili ndiyo atiye saini yake kwa kuwa ndiyo halisi iliyopitishwa na Baraza lako au basi Miswada ya Kiingereza iende sambamba katika Kamati na Baraza ambapo wajumbe wako wawe na nafasi ya kutowa maoni yao katika miswada yote miwili na wakati wa kupitishwa katika Baraza na ule Mswada wa Kiingereza uwepo upitishwe sambamba na ule wa Kiswahili. Vyenginevyo Mheshimiwa Spika anaweza kuja kutokea mwananchi mmoja na kuzipinga baadhi ya sheria za Kiingereza mahkamani kwa hoja kuwa sio iliyojadiliwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Habari na michezo katika kuendeleza nchi yetu, na kwamba ndiyo inayochochea ari ya wananchi katika kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii, hivyo inahitaji uangalifu mkubwa sana ili kuimarisha ustawi wa wananchi na kukuza vipato vyao.

Mhe. Spika, nadhani sote tutakubaliana kuwa michezo ikitumika vyema inaweza kuwa chanzo kizuri cha mapato kwa watu wetu na hivyo kupunguza umasikini wa kipato. Kwa sababu hii, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ndiyo inawasilisha Mswada huu ili, pamoja na mambo mengine, kuweza kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza na kuimarisha michezo nchini.

Mhe. Spika, Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na Kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Taifa la Michezo ya mwaka 2010, umekusudia kutowa msukumo na kufanya mageuzi makubwa ya michezo hapa Zanzibar kwa kulipa nguvu na mamlaka Baraza la Michezo, ili liweze kufanya maamuzi muhimu ya kimichezo nchini pamoja na kushirikiana na taasisi au chama chochote cha michezo kwa madhumuni hayo.

Mhe. Spika, Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii iliupokea Mswada huu na kuujadili kwa kina mnamo siku ya Jumanne ya tarehe 23/3/2010. Wakati wa kuupitia Mdwasa huu, Kamati ilipendekeza baadhi ya marekebisho yatayohitaji kufanywa katika Mswada huu kwa madhumuni ya kuuimarisha zaidi na kuufanya ulete tija inayokusudiwa. Baadhi ya marekebisho ni kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, **a**ina ya kwanza ya masahihisho yaliyofanywa na Kamati yetu yalihusu makosa yakilugha au uchapaji yaliyojitokeza katika Mswada**.** Kwa mfano, katika ukurasa wa 23 wa Mswada huu, neno ”IMETUGWA” lililo mara

baada ya kichwa kirefu cha maneno yaani ”long title” limesahihishwa na sasa kufanywa lisomeke ”IMETUNGWA”. Vile vile, kumeongezwa neno ”na” baina ya maneno ”saini” na ”rais” yaliyo katika kifungu cha 1(1) ili kukamilisha maana iliyokusudiwa ya kuwa itatiwa saini na Rais.

Mhe. Spika, makosa mengine ya kiuwandishi yaliyojitokeza katika Mswada ni kama vile katika tafsiri ya neno neno ”kuthibiti” lililo katika tafsiri ya maneno ”chama cha Taifa cha michezo”, baina ya maneno ”na” na ”michezo” limesahihishwa na kufanywa lisomeke ”kudhibiti”. Madhumuni makubwa ya kulirekebisha neno hili ni kuwa Kamati imeona kuwa kwa mujibu wa Mswada huu, Baraza la Taifa la Michezo lina majukumu ya kuendeleza na kudhibiti michezo na wala sio kuthibiti michezo.

Mhe. Spika, wakati wa uchapaji wa Mswada huu inawezekana baadhi ya nambari au tarakimu zilikosewa kwa bahati mbaya. Vifungu vingi vilivyofanyiwa marejeo (*cross reference*) katika kifungu cha tafsiri inaonekana zimekosewa na hazipo kwa usahihi. Marejeo au reference zilizofanywa katika tafsiri za maneno ”Daftari”, ”Katibu”, na ”Mwenyekiti” zote zimekosewa na hivyo Kamati imejitahidi kuonyesha usahihi wake kama ilivyozibaini wakati wa kuupitia Mswada huu. Kwa msingi huu, katika tafsiri ya neno ”daftari”, tarakimu 17(2) zinabadilishwa na badala yake zinawekwa tarakimu 19(2). Katika tafsiri ya neno ”katibu”, tarakimu 14 zinabadilishwa na badala yake zinawekwa tarakimu 16. Katika tafsiri ya neno ”mwenyekiti”, tarakimu 14 zinabadilishwa na badala yake zinawekwa tarakimu 4(a).

Mhe. Spika, Kamati yetu kwa bahati nzuri ilikuwa na nakla za Kiingereza za Mswada huu. Hivyo, baadhi ya nyakati Wajumbe waliweza kulinganisha baina ya vifungu vilivyomo katika Mswada wa Kiswahili dhidi ya vile vilivyomo katika Mswada wa Kiingereza. Ikitokezea vifungu hivyo vimetofautiana basi Kamati ilitaka maelezo kujua kipi kati ya vifungu hivyo ni sahihi na ndicho ambacho wizara inakikusudia kibakie kwenye Sheria. Kutokana na hali hii, Kamati imependekeza kurekebishwa tafsiri ya neno ”michezo” ili ilingane na ile iliyokuwa katika Mswada wa Kiingereza. Tafsiri iliyoongezwa inafafanuwa michezo kwa kujumuisha michezo mengine yote ambayo Serikali, kwa kupitia gazeti rasmi la Serikali itaitangaza kuwa ni michezo kwa madhumuni ya sheri hii.

Mhe. Spika, Kamati imependekeza marekebisho Kifungu cha 7 ambapo imeona ni vyema Mwenyekiti wa Baraza akapewa nafasi ya kutajwa katika sheria. Hapo awali kifungu hichi kilikuwa kinazungumzia nafasi na majukumu ya Makamo Mwenyekiti pekee bila ya kumgusia Mwenyekiti. Baada ya kukipitia, Kamati imeshauri kuwa ni vyema kifungu hichi kikaanzisha rasmi nafasi ya Mwenyekiti pamoja na Makamo wake na kwamba kiseme wazi kuwa

Mwenyekiti ndio ataongoza vikao vyote vya Baraza isipokuwa atakapokuwa hayupo ndiyo Makamao Mwenyekiti akamate kiti na kuongoza vikao.

Mhe. Spika, Kifungu cha 10, cha Mswada kwa namna kilivyo sasa kinasomeka kuwa ”uwamuzi wa Baraza unaweza kuchukuliwa kuwa ni sahihi”. Kamati iliona kuwa maneno ”unaweza kuchukuliwa” yaliyo katika kifungu hichi hayatowi maana nzuri kwa kuwa yanatowa mwanya kwa maamuzi hayo yasiweze kuchukuliwa kuwa ni sahihi. Hivyo ili kusawazisha kasoro hiyo Kamati imependekeza marekebisho kwa kuyaondosha maneno yanaweza kuchukuliwa na badala yake kuweka utachukuliwa kuwa ni sahihi bila ya kuweka *loophole* kwa mtu mwenye nia mbaya kuyakataa maamuzi ya Baraza kuwa si sahihi.

Mhe. Spika, Kamati imependekeza kurekebishwa kwa kifungu cha 12 ili kilingane na kifungu cha 30. Kamati iliona inawafikina zaidi na maoni kuwa kumbukumbu za mikutano ya Baraza ziwekwe katika utaratibu ulio bora na Katibu Mtendaji wa Baraza lakini ni vizuri azitie saini yake kabla ya kuthibitishwa katika mkutano unaofuata na kisha zisainiwe na Mwenyekiti wa Baraza baada yakuonekana ziko sahihi na kuthibitishwa na mkutano.

Mhe. Spika, Kamati yetu imeona kuwa Kifungu cha 14 kirekebishwe ili kuongeza sharti la kufariki dunia kuwa moja ya sababu zitazomfanya Mjumbe wa Baraza asite kuwa Mjumbe. Endapo Mjumbe atafariki hii ni wazi kuwa atakuwa hayupo na hivyo hatoweza tena kuwa Mjumbe wa Baraza kwa kuwa hataweza kuhudhuria na kushiriki katika vikao vha Baraza. Mhe. Spika, lakufurahisha ni kuwa sharti hili lilikuwa limetajwa katika Mswada wa Kiingereza lakini lilikuwa limeachwa katika Mswada wa Kiswahili.

Mhe. Spika, Hayo ni sehemu tu ya mapendekezo ya marekebisho yaliyofanywa na Kamati yetu**.** Marekebisho kamili yanapatikana katika waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho ambao natumai kila Mjumbe atakuwa amepata nakla yake.

Baada ya maelezo hayo machache, yenye ufafanuzi wa kina Mheshimiwa Spika naomba nikushukuru tena kwa niaba ya Kamati yangu, kwa kunipatia fursa hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu mswada huu.
Aidha, nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa usikivu na ustahamilivu wao wakati wote nikiwasilisha maoni ya Kamati yetu.

Mhe. Spika, Kwa kuzingatia umuhimu wa Mswada huu pamoja na maelezo yote niliyoyatoa hapo awali, nachukua fursa hii kutamka rasmi kuwa, mimi binafsi, Kamati yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani

tunaunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wauunge mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja baada ya kuujadili na kutoa maoni yao muhimu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, kwa kuwa mengi tulizungumza katika mambo mbali mbali na maswali na majibu juu ya michezo, basi naomba kabla sijawasilisha niseme machache sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi naipongeza wizara kwa kutoa nfasi hii nzuri ya kuhakikisha kwamba chombo kilichoelekezwa hapa yaani Baraza la Taifa la Michezo ni chombo ambacho kinarasimu michezo yote au kinasimamia michezo yote bila ya ubaguzi.

Lakini pia wito wangu Mhe. Spika, ningeviomba vyama vya michezo vyote, vihakikishe kwamba vinafuata taratibu zake nzuri na vinakwenda na kalenda zake, na zinatafuta ushauri mzuri kwa Baraza la Michezo pale wanapoona wamekwama.

Mimi wito wangu Mhe. Spika, hivi sasa katika mambo ya michezo hasa mpira wa miguu duniani unapigwa vita sana na vyama vya soka duniani, kuhusu mambo ya kushiriki katika migomo au mambo ya kushiriki katika mahakama zetu za nje.

Mhe. Spika, mimi naomba watumie nafasi hii kuwa huru, watumie nafasi hizi kama ni chanzo cha maendeleo katika michezo. Pia kama ilivyosema sheria hii kwamba michezo ni ajira na michezo ni mali sasa hivi.

Mhe. Spika, katika nchi yetu tuna vijana wetu wazuri wenye vipaji vya michezo mbali mbali. Ukija kwenye riadha wapo, kuogelea wapo. Kwa wachezaji wa mpira wa miguu tena ndio sitaki kusema, maana nikisema nitaambiwa mchezo huo ndio ninaupenda zaidi. Lakini michezo yote ina fani nzuri na maendeleo yake yanaonekana.

Kwa hivyo, niviombe vyama vyote vya michezo vishirikiane sana katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

La mwisho Mhe. Spika, narudia tena kauli yangu ya kwamba mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani na kwa niaba ya kamati yangu ambayo nimesoma hotuba yetu hii ya maoni, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Najma Khalfan Juma: (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, nianze kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyeumba ulimwengu huu na vilivyomo na ambaye uwezo wake usiokuwa na kikomo wala mipaka ndio uliotuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wazima kiafya – Amina

Pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Mswada nilioutaja hapo juu – nakushukuru sana.

Mhe. Spika, mswada huu umekuja wakati muafaka kulingana na haja halisi ya kukuza michezo bila ubaguzi, upendeleo au vitisho.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri pamoja na ufutwaji wa Sheria No. 8 ambayo imeonekana kuchoka au kutotekelezeka katika zama hizi, nikupongeze kwa kuona mbali, yaani nampongeza Mhe. Waziri. Lakini nikupongeze kwa kuitilia nguvu michezo na kushirikiana na wana michezo hasa wale ambao ndio wanaoleta matumaini zaidi yaani michezo ya ndani (*indoor Games*).

Mhe. Spika, wakati nikiusoma Mswada huu ilinijia picha kwamba katika Baraza la michezo kuna kusahauliwa kwa chombo hiki ambacho wajumbe wake ni wasikilizaji kesi za kimichezo zaidi tofauti na majukumu yanayowahusu. Naomba niuchangie na niudadisi Mswada huu kwa maana ya kutaka ufafanuzi wa baadhi ya vifungu vya kisheria vinavyotaka kuondoshwa na kuwekwa vipya au kama itavyojulikana kuwa ni sheria mpya ya uanzishwaji wa Baraza hilo la michezo. Kwa kuupitia basi Mswada huu namuomba Mheshimiwa aniondolee wasiwasi juu ya vifungu vifuatavyo:-

Kifungu cha 4 cha Sheria kinachohusiana na wajumbe, sioni mantiki ya kumuongezea nafasi za uteuzi Mhe. Rais, hasa tukizingatia kuwa Mhe. Waziri anaehusika na michezo alitosha kuifanya kazi hiyo. Lakini kwa hali nyengine mteule huyo wa Rais yaani Mwenyekiti wa Baraza anaweza kujijengea heshima kubwa hata katika vikao vya Baraza pale maamuzi mazito yatapotaka kutolewa hususan katika migogoro ya mara kwa mara ya michezo. Uzoefu umewahi kutuonyesha kwamba Mwenyekiti ambae sio mtendaji wa kiofisi ndani ya Baraza la Michezo anakuwa na tabia ya kuwatawala wajumbe kwa kuwa amepewa ukinara na Waziri ambae huongoza Wizara.

Mhe. Spika, katika kifungu hicho hicho ningeshauri Wizara ikazingatia kuwa na mjumbe kutoka Wizara ya Afya kwani ni muhimu kwa Wizara hiyo kuwa na taarifa na maelekezo kupitia mjumbe wake ndani ya utaratibu wa uteuzi wa Mawaziri husika, hii itathibitisha kuwa michezo ni afya.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 5 “kazi za Baraza” ningeomba Mhe. Waziri akatoa ufafanuzi wa Ibara (i) ambacho kinaonyesha uingiliaji kati wa kazi za vyama vya michezo, jee Waziri atato ufafanuzi juu ya hadhi ya Baraza letu nje ya mipaka ya Tanzania na haitakuja kuwa kujiingiza katika migongano na mashirikisho ya michezo ya Kimataifa ambayo hupinga uingiliwaji kati wa sheria za vyama wanachama ambapo Baraza halina nafasi. Pili Baraza letu la Michezo lina nafasi gani kimataifa jee linatambuliwa?.

Kifungu cha 11 kinachoelezea “uamuzi kutoathirika kwa athari za utaratibu”.

Kifungu hiki Mheshimiwa Waziri kinatia wasiwasi kwani haithibitiki suala zima la ubatilishaji pale maamuzi yatapopitishwa. Uzoefu unaonyesha jinsi baadhi ya vilabu au wanamichezo walivyokosa haki zao na wakatishiwa kufukuzwa au kusimamishwa pindi wakienda mahakami, haidhuru kwenye kifungu cha 3 Ibara (b) kinaonyesha haki ya kisheria.

Mhe. Waziri huoni kwamba Baraza lisipokuwa na Mdhibiti kabla ya ufikishaji mahakamani litaweza kuchukua nafasi ya kuonea na hasa pale nafasi ya Mwenyekiti, Katibu Mtendaji na hata baadhi ya wajumbe watapovaa kofia za kuteuliwa kutoka ngazi ya Rais na Mawaziri husika?.

Mhe. Spika, pamoja na mzigo mwengine kwa Mhe. Rais kuteua Katibu Mtendaji wa Baraza, naomba ufafanuzi juu ya sifa zilizotajwa katika fungu la 16 (2) kwani sifa hizo tatu pamoja na kukubaliana nazo, lakini suala la uajiri hapa linapaswa kuzingatiwa, jee haki hii ya uteuzi wa Rais haitazingatia uzanzibari pia kama sifa, kwani Baraza letu la michezo liliwahi kuwa na wajumbe wasio Wazanzibari miaka iliyopita.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atuwekee wazi suala la ofisi ya Mrajis na nguvu aliyopewa kwani kifungu cha 19 (iii) hakitoi uhalisia na hali tuliyonayo katika kutumia vyama au vilabu au majimbo, pale vyama vinapopokea na kuendesha mashindano ya wabunge na wawakilishi kwa utashi wa kisiasa. Sasa hapa ni kuingizwa vyama hivyo kisiasa kwa sura ya usimamizi, naomba nipate ufafanuzi, na hasa wakati tunaoukabili wa kujipatia umaarufu sisi wanasiasa kupitia viwanja vya michezo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya mwanzo katika kuchangia kijumla mswada huu uliowasilishwa hivi punde wa kufuta sheria namba 8 ya mwaka 1983 na kuweka mpya ya Baraza la Michezo ya mwaka 2010.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri na nimpongeze kwa jitihada kubwa ya kunyanyua michezo, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na maofisa wote wa wizara yake kwa jitihada kubwa wanayoichukua katika kukuza michezo.

Mhe. Spika, naomba niungane na wenzangu waliotangulia kusema kwamba michezo hivi sasa kidunia ni uchumi na nchi nyingi duniani sasa hivi zinawekeza katika michezo. Sisi tunawaita wafadhili kuja kuwekeza katika mahoteli na mambo mengine. Lakini sasa hivi wenzetu huko nje walioendelea tayari mwenye fedha zake za kutosha anawekeza kwenye michezo, kwa kununua wachezaji bora na kuunda timu na kushindanisha. Katika ushindanishi ule ndio mtu anapata kile chake na kuongeza uchumi kwenye nchi. Sasa na sisi nadhani kwa juhudi tunazofanya basi tunaweza tukafika.

Pia michezo ni ajira ambapo wenzetu wengi sasa hivi wanaajiriwa kwa madau makubwa sana, inakuwa ni kinyang'anyiro hasa, huyu anamtaka kwa bei hii na huyu anamtaka kwa bei hii. Sisi tunashukuru kuwa angalau tunafika mpaka hapo Bara watu wanatunyang'anyia, lakini nadhani tukitoka hapo tutapiga hatua zaidi.

Mhe. Spika, mswada huu umeashiria kwamba twende huko ambako tumekusudia, naopongeza na naamini kwamba mswada umekuja katika kipindi kizuri kabisa.

Mhe. Spika, nikija kwenye mswada nije na sababu na madhumuni ambayo ni sababu nzuri. Miswada mingi huwa inaleta sababu na madhumuni huwa hazifahamiki, lakini hii imeandikwa kitaalamu sana. Naomba ninukuu kidogo, kinasema hivi;

> "Madhumuni ya mswada huu ni kuweka sheria mpya yenye kuanzisha Baraza la Taifa la Michezo la Zanzibar na kufanya liwe na uwezo na mamlaka ya kusimamia na kuendeleza shughuli mbali mbali za michezo, kulingana na sera za maendeleo za michezo nchini kwa lengo la kupata wanamichezo bora na kuondoa urasimu uliopo katika sheria nambari 8 ya mwaka 1983".

Nashukuru Mhe. Spika, kwa utangulizi huo na kila mtu akisoma atajua dhamira namakusudio ya kuletwa kwa mswada huu.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo ndogo nije kwenye sheria yenyewe na mimi kubwa nitataka ufafanuzi tu ambapo ziko sehemu ambazo sijazifahamu, nitazisoma halafu niombe msaada wa Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ili aweze kunielezea.

Kwanza kabisa nije kwenye ukurasa wa 24 ambao umeanza kwenye ukurasa wa 23, hapa pana maneno ya ufafanuzi, yale maneno ambayo yametumika na yamewekwa tafsiri yake. Sasa nilikuwa naomba kuna neno moja limetumika sana humu lakini halikuwekewa ufafanuzi wake. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na wanasheria wake kupitia kwako Mhe. Spika, kama itahitajika na mawazo yangu yakiwa mazuri, basi na hili lingewekwa kwenye ufafanuzi na neno lenyewe linaitwa Wadau wa Michezo. Kwa kweli limetumika sana, lakini kwenye ufafanuzi halimo.

Nadhani kama sheria inatakiwa iwe nzuri na hao tumewazungumza sana humu, basi tungeweka maana yake na mtu yeyote angeweza kufahamu maana hiyo kwa wepesi na kujua imekusudiwa nini. Kwa maana hiyo, kama litakuwa zuri basi liandikwe kwenye ufafanuzi.

Jambo la pili nimeusoma mswada mwanzo mpaka mwisho, yaani vifungu vyote sita, lakini kuna jambo sikuliona. Sasa sijui wanasheria hili linahusika litiwe kwenye sheria au haliruhusiki na nitamuuliza Mhe. Waziri kama linaruhusika basi si vibaya nalo tukaliweka. Lakini kwa mawazo yangu nafikiri tukiliweka linaweza kusaidia sheria yetu.

Hapa Zanzibar tangu kipindi cha Mapinduzi kuna michezo ambayo ilipigwa marufuku kutokana na kwamba haileti tija wala faida isipokuwa ni hasara tu. Lakini tafsiri ya michezo hapa imezungumzwa kijumla, yaani michezo ya kujenga mwili, kufanya mazoezi, kushindana na kila kitu. Kwa kweli kuna mchezo mmoja hapa kwetu hauruhusiwi ambao ni wa ngumi, yaani *Boxing*.

Sasa sijui hii kisheria kuiweka inaruhusu au vipi, kwa sababu michezo imetafsiriwa kijumla, basi kutokana na kwamba sheria imewachwa wazi mtu anaweza kuanzisha mambo haya na baadaye tukamtia kwenye matatizo wakati sheria hakuna pahala ilipomzuia.

Kwa hivyo, hilo naliomba Mhe. Spika, kama litaruhusiwa kwa tafsiri ya michezo jambo hilo lingeepukwa na kusema isipokuwa mchezo fulani, ili mtu akienda kombo ya hili iwe sheria inamzuia. Ikiwa hilo litasaidia kuiweka uzuri sheria yetu, naomba wanasheria pamoja na Mhe. Waziri kulitilia maanani kama linafaa kuliingiza.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 25 Baraza litakuwa na kazi zifuatazo, ambazo hizi zimeandikwa nyingi, lakini zile ambazo zinanipa mashaka nataka kidogo nizizungumzie. Miongoni mwa kazi hizo za Baraza kifungu (d) Mhe. Spika, naomba ninukuu

Kifungu cha (d) kinasema hivi:-

"Kwa kushirikiana na mamlaka husika ni kusimamia na kusajili viwanja vya michezo ili kuepusha uvamizi wa viwanja hivyo".

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwamba hivi sasa sheria imeeleza hivyo. Lakini tatizo kubwa ambalo lilikuwa likizikabili timu mbali mbali ni hili la kuvamiwa viwanja vyao. Kwa kuwa nchi yetu hivi sasa ni ndogo, basi viwanja vingi ambavyo vipo karibu na mji watu huuziana na kujenga nyumba, tatizo hilo limeshatokezea kwenye eneo langu la Kihinani mwenye eka kauza kiwanja na watu wakajenga.

Sasa nadhani Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake hili wameliona kwa hiyo nawapongeza sana kulitia kwenye sheria. Lakini sheria ni kitu kimoja na usimamizi ni kitu chengine.

Kutokana na hali hiyo, naomba msaada sana hili likeshapitishwa, basi tukaanza kufuatilia eneo moja baada jengine, ili kuweza kupata udhibiti wa sheria kwa hivi viwanja kidogo tulivyonavyo na watu wasiweze kuvamia. Vyenginevyo tunaweza kuwa sheria tumeitunga vizuri, lakini bado watu wakavamia viwanja na kujenga maduka na nyumba za kuishi au wengine hivi sasa wanapigia matofali.

Kwa kweli nimefurahi sana na nadhani wanamichezo wengi watakuungeni mkono juu ya suala hili. Isipokuwa naomba lifanyiwe kazi, ili lile lengo lililokusudiwa liweze kupatikana.

Kifungu kingine cha (g) Mhe. Spika, naomba kunukuu halafu ndio nitoe mawazo yangu.

Kifungu cha (g) kinasema hivi:-

"Kuhakikisha kuwa vyama vyote vya michezo vinaunda kamati za usuluhishi na rufaa za michezo katika vyama vyao".

Kwa kweli hili ni jambo la msingi, lakini suala hili pia linataka usimamizi mzuri. Kwa sababu hivi sasa yapo Mabaraza kama haya na tayari wamejaribu kuweka vitu kama hivi isipokuwa upendeleo unakuwa mkubwa sana. Kwa hivyo, naomba na hili pengefanywa utaratibu baada ya sheria hii hao wanaotayarisha masuala ya kufanya masuluhisho pamoja na rufaa, basi wangelipata mafunzo madogo ya kuweza kukaa na kuamua na kutoa haki kwa upande mmoja unaohusu.

Lakini hivi sasa migogoro imekuwa mikubwa na watu wanakwenda katika maamuzi na baadaye viongozi wanapendelea upande mmoja. Kwa kuwa sasa tumelitia kwenye sheria, vyema kulifuatilia na kulisimami, ili kupunguza migogoro katika michezo.

Kwa kweli vijana wengi hupenda kuingia kwenye michezo, lakini huvunja moyo na usimamizi wa viongozi kutokana na kukosa haki zao za kimsingi. Kwa mfano, mtu anaweza kuingia kwenye ligi na kuingia kwenye mzunguko wa kwanza na kupita na kuingia kwenye mzunguko wa pili, lakini akajafanyiwa vikwazo katika hatua ya kumalizia.

Sasa utaona ameshagharamika kwa kiasi kikubwa, lakini kule ambako amekusudia kufika hafiki tena. Kwa hivyo, msimu mwengine huona bora mtu aache tu, isipokuwa acheze mpira kwa ajili ya kujenga mwili wake. Kwa hivyo, nadhani tukilisimamia hili litatusaidia katika kuweka suala hilo vizuri na watu wakaweza kushiriki michezo kikamilifu.

Mhe. Spika, jengine baada ya (h) namba ya Kirumi (i) naomba ninukuu

> Kifungu cha (i) ambacho kinasema hivi:-
>
> > "Kushiriki katika mikutano ya vyama vya michezo katika ngazi mbali mbali ndani ya nje ya nchi".

Nadhani ni Mjumbe wa Baraza au Baraza linaweza kutoa mtu na kushiriki mikutano mbali mbali ya hapa kwetu ndani na nje. Kwa kweli hapa sijafahamu vizuri, kwa hiyo naomba nipate ufafanuzi ili niweze kuelewa vizuri kwamba ushiriki huu utakuja kwa mualiko ama sheria moja kwa moja inampa haki huyu Mjumbe wa Baraza kushiriki au Baraza kwa jumla.

Kwa hivyo, naomba kifungu hiki nifahamishe vizuri kwamba kushiriki kwenye mikutano ya vyama vya michezo, katika ngazi mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Kwa sababu ninafahamu kwamba japo Mjumbe au Mwenyekiti wa Baraza wengine huwa wanaingia kwa cheo au mialiko, sasa hapa imekusudiwa kwa cheo au mialiko. Ikiwa mwaliko haupo na cheo chenyewe Baraza chombo kikubwa cha mkusanyiko wa watu ambao wametajwa vyeo mbali mbali. Kwa maana hiyo, kama kuna maelezo basi naomba nifahamishe vizuri, ili nipate kuelewa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, sasa niende kwenye ukurasa wa 26 na hapa pia nataka ufafanuzi tu. Kuhusu kifungu cha 11 kinachozungumzia masuala ya uamuzi, naomba kunukuu.

> Kifungu cha 11 kinasema hivi:-

"Uamuzi wa Baraza utakuwa batili iwapo utakwenda kinyume

na Katiba na Sheria hii ya Baraza".

Hapa nimefahamu kwamba batili maana yake ninaijua. Lakini nadhani kimepungua kitu, kusema tu kuwa uamuzi wa Baraza utakuwa batili iwapo utakwenda kinyume na Katiba na Sheria ya Baraza hili. Kwa mfano, Baraza limekaa na kuamua jambo fulani pengine kwenye kesi hizi na wakamaliza kikao chao. Lakini unaweza kuwa batili ikiwa hawakufuata Katiba na Sheria, hivi ni nani ambaye atawazindua juu ya suala hilo.

Nafikiri kama sentensi inaning'inia na ikiwa kuna maana ya msingi ambayo imekusudiwa basi ningepata ufafanuzi zaidi. Wakati ninapoisoma sentensi inaeleweka, lakini swali langu je hilo Baraza ni nani atakayelizindua kwamba hiyo haki uliyoifanya siyo na iwe batili, kama kuna chombo cha juu waziri au kitu chengine chochote kile. Kutokana na hali hiyo, nadhani kama sentensi haikwisha na kama iko sawa basi nikipata maelekezo sina tatizo.

Kifungu cha 14 hapo hapo naomba ninukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 14 kinasema hivi:-

"Mjumbe wa Baraza atasita kuwa mjumbe wa Baraza endapo yatatokea moja ya mambo yafuatayo:-

Niende kwenye kifungu cha (b)

(b) Iwapo atatuhumiwa kufanya kosa la jinai na kuthibitika kufanya kosa hilo".

Sasa hapa nimechanganyikiwa kidogo, huyu mjumbe ni mwananchi pengine anafanyakazi nyengine nyumbani na amebahatika kuchaguliwa kwenye Baraza hili. Kwa maana kwenye zile kazi zake za Baraza au huko mitaani, yaani hapa hakikufafanuliwa na imewacha wazi.

Kwa mfano, mimi ni mfanyabiashara kwa bahati Mhe. Waziri kupitia sifa zangu ameniteua nimekuwa Mjumbe wa Baraza, lakini naambiwa kwamba nitatolewa Mjumbe wa Baraza kama nitafanya kosa la jinai. Je, kwenye kazi zangu za kibiashara ambazo ni binafsi au zile za Baraza, hapa haikuainishwa. Kwa hivyo, hilo pia naomba kama kutakuwa na maelezo zaidi nipewe ili niweze kufahamu.

Lakini kazi nyengine zote nimezikubali nafikiri moja imeachwa na kama ipo haja ya kuongezwa na ikiwa hapo basi mtaniambia. Vile vile mtu anaweza kuwa si mjumbe iwapo atakufa inakuwa amejitoa kwenye ule ujumbe. Kwa

hivyo, kama hii nayo itakubali kuwekwa basi ni vyema ndio mchango wangu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nikiendelea ukurasa wa 26 kifungu cha 16 katika eneo hilo naomba kunukuu.

Kifungu cha 16 (1) kinachosema hivi:-

" (1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Baraza ambaye atateuliwa na Rais,

2. Mtu hataweza kuteuliwa Katibu Mtendaji mpaka awe na sifa zifutazo:-

(a) Awe na stashahada kutoka chuo kinachotambulika;

(b) Awe uzoefu katika masuala ya michezo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano".

Wasi wasi wangu ni kwamba michezo ni kitu kikubwa sana, sasa tukisema mtu awe na uzoefu wa michezo tu nafikiri kila mtu, lakini kumtilia na vikwanzo mpaka atimize miaka mitano mpaka kumi. Nadhani hili tungelipunguza na kusema tu awe na sifa na uzoefu katika michezo mbali mbali itakuwa imetosha. Lakini tukisema atimize miaka mitano pengine mtu ni mzuri utampima vipi kama ametimiza miaka mitano au kumi wakati mtu huyo uraiani.

Kwa hivyo, na hili pia lingeangaliwa kisheria tusijekuacha watu wazuri kwa kuwa hawakufika miaka mitano katika kushiriki michezo na mchezo unaweza kutizama Mao-Tse-Tung tu hapo mpira siku mbili au tatu mpaka nne na wala si lazima ucheze.

Mhe. Spika, nadhani kuna mambo ambayo tunayafunga kwa kuwakosesha watu riski. Kwa sababu naamini kwamba ukusema awe na uzoefu wa masuala ya michezo, nafikiri imetosha na hii ya muda tungeipunguza kwa mawazo yangu, kama itawezekana Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wako wazo langu ndio hilo.

Nikiendelea kwenye kifungu cha 17 kuhusu majukumu ya Katibu Mtendaji namba (2) Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 17(2) kinasema hivi:-

"(2) Pamoja na majukumu aliyonayo Katibu Mtendaji ambayo yametajwa hapo juu vile vile:-

Kuna nambari za Kirumi (i), (ii), (iii) na wasi wasi wangu kwenye namba (iv) kwa hivyo naomba ninukuu na halafu nitoe wasi wasi wangu.

Kifungu cha 17 (2) (iv) kinasema hivi:-

> "atadhibiti taarifa za wajumbe wa Baraza".

Mhe. Spika, hii kudhibiti imenipitikia kidogo naona haileti maana. Nadhani tungesema atahifadhi taarifa za Wajumbe wa Baraza. Kwa sababu kudhibiti ni kitu labda unataka asifanye kitu fulani unamdhibiti asikifanye, lakini nilivyofahamu mimi kama kuna taarifa za mjumbe wako wa Baraza unataka kumuhifadhia.

Sasa sijui imekusudiwa nini hapa kidogo sikuifahamu kwamba huyu Katibu Mtendaji atadhibiti taarifa za Wajumbe wa Baraza, kama vile vikao asitoe siri. Kwa hivyo, kama kuna maelezo zaidi ni vyema kuyapata kwa ajili ya kufahamu vizuri, lakini naona kama imekaa kinyume kidogo.

Sehemu hiyo kifungu cha 8 kuhusu Mrajis wa Vyama vya Michezo na hapa kidogo ninayo mashaka naomba nipatiwe ufafanuzi kidogo. Kwa hivyo, naomba kunukuu na baadaye ndio niseme hilo ambalo nimelikusudia.

Kifungu 18 (1) kinasema hivi:-

> "Waziri kwa kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali, atamteua Mrajis wa Vyama vya Taifa vya Michezo, Vyama vya Wilaya na Vilabu kufanya kazi kwa kutumia uwezo waliopewa kwa mujibu wa sheria hii na kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii, pia anaweza kuteua Msaidizi Mrajis ambaye atapokea maelezo kutoka kwa Mrajis".

Sasa huyu Mrajis anateuliwa na Waziri ilivyokusudiwa hapa, lakini huku tunaambiwa atateua Msaidizi Mrajis ni huyu Mrajis mwenyewe au ni yule Waziri mwenyewe atapeleka pendekezo achague wote wawili. Kwa hivyo, hapa nataka ufafanuzi, ili niweze kufahamu kwamba huyu Mrajis mwenyewe akeshakuteuliwa na Waziri tena yeye ateue Msaidizi wake ama Waziri atateua wote wawili.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye kuzungumzia suala zima la mswada huu niende kwenye ukurasa wa 28 kwenye kifungu cha 3(d) naomba ninukuu na hapo ndio nitapata maana yote na halafu nije hapo nilipokusudia.

Kifungu cha 3(d) kinasema hivi:-

> "Kusitisha uanachama wa chama au *club* yoyote ya michezo iwapo itatokezea mambo yafuatayo:-".

Hali hii imekusudiwa kwa hizi timu au chama ambacho kimeshasajiliwa kitasita uwanachama wake kwa mambo yafuatayo:-

(i) iwapo kwa makusudi kinakwenda kinyume na Katiba na Kanuni zake; Hilo sina tatizo nalo,
(ii) iwapo kinatumiliwa katika kufanya vitendo ambavyo vinakwenda kinyume na Sera ya Michezo ya Zanzibar; Vile vile hilo sina tatizo nalo,
(iii) iwapo kinajishughulisha na mambo ya siasa.

Sasa hapa nataka ufafanuzi kidogo, kwa sababu sitegemei kwamba watu wote hawana vyama vya siasa, kwa kweli watu wote wanavyo, isipokuwa kila mtu ndani ya roho yake. Kwa hivyo, tukiweka hapa naona kama tutainyima haki ya timu pamoja na vyama vya michezo.

Mhe. Spika, hapa ningeomba ufafanuzi zaidi labda mtu siasa hiyo atashiriki vipi kwa kushika bendera, kwenye mikutano, atachangia hoja, ili mtu tusimnyime haki katika suala la michezo. Kwa hiyo, naomba hapa nipate ufafanuzi imekusudiwa nini, ili nami niridhike na wala sina matatizo na mswada huu *(Makofi)*.

Nikiendelea niende ukurasa wa 30 sehemu ya nne kuhusu masuala ya fedha, matumizi pamoja na ukaguzi wa mahesabu mapato ya Baraza, naomba kunukuu.

Kifungu cha 31(c) kinasema hivi:

> "Fedha zilizolipwa kwenye Baraza kwa njia ya michango, ruzuku, kodi, ada na riba".

Kwa hivyo, nataka nijue hiyo riba itatokana na nini au itakuja vipi, yaani riba pia ni pato. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi ili niweze kufahamu.

Lakini mwisho kabisa kiujumla ningependa kushukuru wizara na ningeomba kutokana na sheria yetu nzuri basi tuisimamie vizuri kiutekelezaji. Vile vile kuna jambo moja la jumla ambalo halimo kwenye mswada ambalo nataka nilisisitize kwenye wizara na limeshawahi kutokezea mara nyingi, basi ningeomba na hili wakalitafutia dawa, ili kuweza kuendeleza michezo yetu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hivi sasa timu nyingi za mikoa kwa vile Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Unguja wanabahatika kuingia kwenye Daraja la Kwanza na kuchukua nafasi tatu kubwa. Kwa mfano, kipindi kimoja hapa Mundu ilikuwa *Club* Bingwa au Mshindi wa Pili, sasa timu kama hizi huwa

kuna ligi fulani, lazima timu isafiri, yaani iende nchi hii na ile sasa *Clubs* zetu zinakuwa changa kwenda nje.

Kwa hivyo, ilifika mpaka kwenda wa mabasi sijui nchi gani ile na walipofika wamechoka sana na baada ya kucheza mechi walifungwa magoli mengi. Lakini walipokuja hapa kumbe wale wanaowagharamia wachezaji kukawa na madeni hapa hoteli mmoja mjini tena muda mrefu na baadhi ya wapenzi au wadau wakazuiliwa gari zao mpaka deni likalipwa.

Kutokana na hali hiyo, naomba timu zetu kama hizi za shamba wakati zinapokuja mjini hali zao si nzuri, basi wizara ingeweka fungu maalum kwa ajili ya kuwasaidia kwa lengo lile la kukuza michezo pamoja na kuendeleza vipaji.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono mswada huu nawaomba wenzangu tuuchangie.

Nashukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nilifikiria kuna orodha ndefu ya wachangiaji, lakini kila nikisubiri mtu ainuke simuoni. Kwa hivyo, nami nataka kuchangia kidogo tu.

Nikianza na mchango wangu kwenye ukurasa wa 28 nadhani Mhe. Ali Abdalla Ali amekiona, kwa sababu nimekitia alama kuhusu masuala ya shughuli za Mrajis atakuwa na Mamlaka na majukumu yafuatayo; (a), (b) (c), naomba kunukuu.

> Kifungu cha 19 (d) kinasema hivi:-
>
> "Kusitisha uanachama wa chama au kabla yoyote ya michezo iwapo itatokezea mambo yafuatayo:-".

Hiyo hapo itawezekana na kile cha tatu nimekiogopa kidogo. Kwa hivyo, kile cha (iii) ndicho ninachokiogopa kidogo, iwapo kinajishughulisha na mambo ya siasa.

Naogopa tena nimeandika hii ni fitna, kwa sababu Mhe. Spika sisi walimu kuna kitu nadhani wengi humu tunakiita *value judgment*, yaani naweza kumsomesha Mhe. Samia Suluhu Hassan kuna vitu navitia point kwamba hiki nitakipa 1 na hiki 2 na hiki 3. Lakini kuna ile *judgment* tu ninavyomuona Mhe. Samia Suluhu Hassan nikasema hiki mm! Sasa hii *personal discretion* ya mawazo ina hatari sana *(Makofi)*.

Mhe. Spika, unaweza kuja kuambia huko kwamba hiki kinafanya hivi na vile na hayo yamo na yameshatokea huko mitaani. Kwa mfano, ukaambiwa hiki kinajishughulisha na siasa, basi kikakosa bahati tu kwa sababu ya tafsiri ya mtu ambaye pengine amefungwa magoli mengi au ameingia hana viatu na mwenzie amepewa viatu na jezi.

Lakini tatizo langu dogo nimekuwa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary yupo hapa, kwenye ukurasa 24 unasema Mhe. Spika naomba kunukuu.

> Ukurasa wa 24 unaosema kwamba:
>
> "Baraza litakuwa na Wajumbe wafuatao:-".

Wametajwa pale na masahihisho mengine yameelezwa. Sasa hili ni Baraza inapokuja mkutano wa wadau ukusara wa 29 naomba kunukuu Mhe. Spika

> Ukurasa wa 29 unasema kwamba:
>
> "Kutakuwa na Mkutano wa Wadau wa Michezo ambao utakuwa na wajumbe wafuatao:-".

Mhe. Spika, takriban wote wale waliomo kwenye Baraza wametajwa tena. Nadhani wangetajwa kwamba ni wajumbe wa Baraza na halafu na wengine. Sasa niliposoma huku na kule nikasema je hawa waliotajwa hapa ndio wa huku au wengine, kwa sababu wote wametajwa tena.

Halafu kwenye huo mkutano wa wadau kifungu cha (b) kuhusu Katibu Mtendaji. Nafikiri ni vizuri ikataja Katibu Mtendaji wa Baraza, kwa sababu Katibu Mtendaji wako wengi wanaweza kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Wilaya.

Kidogo nimechanganyikiwa nilikuwa nikimuuliza Mhe. Haji Faki Shaali hapa kifungu (i) na (j) nimeshindwa kuelewa naomba nisaidiwe, naomba kunukuu Mhe. Spika.

> Kifungu cha 26(i) kinasema hivi:-
>
> "Wawakilishi wanne kutoka vyama vya taifa vya michezo ambao watachaguliwa na Mkutano wa Wadau wa Michezo miongoni mwao wawili wawe wanawake".
>
> Kifungu cha (j) kinasema hivi:-
>
> "Mwakilishi mmoja kutoka kila chama cha michezo …".

Sasa nilikuwa nikijiuliza chama cha michezo na vyama vya taifa vya michezo vimetofautishwaje, kwa kweli nimeshindwa kujua tofauti yake na nimejaribu

kwenda kusema labda hebu nitizame *definition* ya chama cha taifa cha michezo, kimeelezwa kwenye utangulizi chama cha taifa cha michezo. Lakini nilipokitizama chama cha michezo hakipo kwa hivyo nikashindwa kutofautisha kati ya vitu viwili hivi.

Kwa maana hiyo, naomba tusahihishe maana yule atakayekuwa anasimamia mambo haya, ndio hayo aliyosema mmoja wetu hapa kwamba mimi sihusiki simo humo, kwa sababu mimi ni chama cha michezo. Mhe. Spika, nilikuwa nikijiuliza labda chama cha Taifa cha Michezo ni wale wanaohusika na michezo ya *Football*, na chama cha taifa ni ile timu ya Mwembeladu.

Kwa kweli sijafahamu Mhe. Waziri na wala sikutaka kueleza maelezo mengi zaidi kwa sababu mengine tayari yameshazungumzwa na wenzangu.

Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo na naunga mkono mswada huu *(Makofi)*.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nakushukuru nami kunipa nafasi nikaweza kutoa mchango wangu mdogo tu. Lakini nataka nichukue nafasi hii kuipongeza wizara kupitia Mhe. Waziri mwenyewe, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote, baada ya kuona kwamba sheria iliyokuwa ikitumika katika Baraza la Michezo imepitwa na wakati na kuweza kuleta sheria mpya ambayo itaweza kusaidia katika kukuza michezo kwenye taifa letu.

Mhe. Spika, kwanza nitakuwa na maswali na halafu nitakuwa na ushauri. Kwa sababu nakumbuka Rais wa Kwanza wa Zanzibar alikataza mambo ya kupigana ngumi Boxing na tulikwenda nayo hiyo kwa muda mrefu sana. Lakini hivi sasa tunacho Chama cha Judo, *Kickboxing*, ambayo nafikiri mchezo wa *Kickboxing* ni hatari zaidi kuliko hiyo *Boxing* yenyewe, kwa sababu *Kickboxing* unapigana kwa migumu pia.

Sasa swali langu kwa Mhe. Waziri je kama watajitokeza vijana na kutaka kuanzisha hiki Chama cha *Boxing* itaruhusiwa na lile wazo la Rais wa Kwanza wa Zanzibar itakuwa tumeliondoa na kama haitoruhusiwa hii *Kickboxing* ni hatari zaidi kuliko hiyo *Boxing* yenyewe.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika mswada huu ambao nimeupitia wote sikuona pahala ambapo umesema kwamba Baraza litashajihisha vijana kuanzisha vyama vya michezo. Nadhani hili linalo umuhimu wake.

Kwa sababu hivi sasa katika mitaa yetu sehemu nyingi ukipita utaona vijana wamejikusanya na kucheza *Pool*, *Keram* na hata *Draft*. Lakini vijana hawa wameji-*keep busy* pale wenyewe. Ikiwa Baraza litaweza kuwashajihisha na

kuanzisha vyama hivi na kuingia kwenye mashindano, basi nafikiri inaweza kusaidia sana.

Mhe. Spika, michezo hii pamoja na kwamba wakati mwengine inakera, maana unaweza kuwakuta vijana wanacheza kuanzia asubuhi mpaka usiku, lakini kwa upande wa pili inasaidia. Kwa sababu ni bora hawa vijana kujishughulisha na hii michezo kuliko kuingia kwenye mambo mengine. Kwa kuwa kijana akikaa tu kichwa kitupu basi inakuwa ni nyumba ya shetani, sasa nyumba ikiwa ya shetani kwenye kichwa yanaweza kuingia ulevi, ulaji wa unga, bangi, mapenzi ya utotoni pamoja na mambo mengine mbali mbali.

Kwa kutokana na hali hiyo ya hawa vijana kujishughulisha na hii michezo, nafikiri ipo haja katika mswada huu kwenye shughuli za Baraza basi kuwe na kipengele kinachosema kushajihisha vijana kuanzisha vyama vya michezo. Hali hii itatusaidia kuwa na vyama vingi na vijana wengi.

Vile vile tusiafute vipaji kwenye *football* tu, pia tunaweza kupata vipaji kwenye *pool*, keram, draft na michezo mengine. Kwa hivyo, ningelimuomba sana Mhe. Waziri katika kazi hizi za Baraza basi kuwe na kipengele cha kushajihisha vijana kuanzisha vyama vya michezo. Pia wanaweza wakawapata wakipita katika mitaa na kuona wanavyocheza.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba tuna tatizo la vyama vyetu vya michezo kupata ufadhili. Ufadhili unakuwa mgumu sana na nataka nikiri kwamba kuna vyama vyengine vya michezo, viongozi wa vyama hivyo pengine hawana uzoefu wa kuomba kufadhiliwa michezo hiyo. Kwa kuwa hawana uwezo wa kuomba kufadhiliwa mchezo ule mara nyingi utakuta mzigo unawaangukia wizara na zaidi Mhe. Mahmoud Thabit Kombo nimemuona mara nyingi sana akihangaika kutafuta wafadhili wa kufadhili michezo.

Mhe. Spika, nafikiri ni vizuri katika mswada huu kungelikuwa na kitu kusaidiana na vyama vya michezo ili kutafuta ufadhili. Kwa sababu wenzetu Baraza hili la Michezo lina uwezo mkubwa zaidi kuliko hivi vyama na wanaweza wakawasaidia. Kwa hivyo, ningelimuomba sana Mhe. Waziri akaliangalia hilo.

Mhe. Spika, sisi hapa sera yetu ni kwamba ufadhili wa pombe tumepiga marufuku hatuutaki. Lakini kitu ambacho mimi kinanipa mashaka ukenda **Gymkhana** pale bahati nzuri nimeshakwenda na Mhe. Waziri kwenye fainali za Kombe la Afrika katika mchezo wa *netball* hapa panachezwa *netball* hapa panauzwa pombe. Lakini ukenda katika Uwanja wa Amani kabla haujafanyiwa ukarabati huku vijana wanacheza *football*, huku vijana wanacheza judo pembeni kuna hoteli pana baa.

Mimi suala ambalo huwa najiuliza kuuzwa pombe katika viwanja na kuvaa nembo ya pombe kwenye shati ukacheza mpira ni kipi chenye athari zaidi? Nafikiri kama tunasema ufadhili wa pombe hatuutaki basin a pombe kwenye viwanja tukataze, kwa sababu watu wakishakunywa pombe kwenye viwanja vya mpira basi chochote kinaweza kutokea. Kwa hivyo, ni vyema tukaliangalia suala la unywaji wa pombe kwenye viwanja na uvaaji wa fulana ya pombe.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mswada huu ni mzuri, umepangwa vizuri zile kasoro ndogo ndogo ambazo nimeziona bahati na kamati wameziona na wamezifanyia marekebisho naomba waheshimiwa wauchangie na watizame zile *points* ambazo zimekosekana hapa basi waweze kuziongeza ili tuufanye mswada huu uwe bora zaidi na iweze kufanya kazi kwa ajili ya kuwaendeleza vijana wetu pamoja na wazee. Mhe. Spika, ukenda kwenye pool unawakuta mpaka wazee wanacheza, ukenda kwenye keram pia unawakuta mpaka wazee wanacheza. Kwa hivyo, hii inamfanya mtu kama Mjumbe wa Baraza hapa amekaa kutwa ameumiza kichwa chake ikiwa anataka apumzike basi anakwenda kujipumzisha kwenye michezo hii. Mhe. Spika, hii inasaidia sana katika kutengeneza mawazo ya mtu na kusahau baadhi ya kero.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nimesema mswada huu ni mzuri nasema naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru hasa kwa kutaja watu wawili maana yake mimi nina mchango mdogo sana.

Mhe. Spika, kwanza mimi napenda nitoe pongezi zangu kwa wizara hii kwa vile wameona kwamba kuna kasoro na wakajaribu kuweka utaratibu mpya ili waweze kurekebisha hiyo kasoro. Mhe. Spika, jambo langu la mwanzo nataka kusema kuhusu hili taifa, hili linaitwa Baraza la Michezo la Taifa sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri tunayo haki ya kutumia taifa sisi hapa kwa sababu sisi ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano taifa ni moja. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa anaunda Baraza la Michezo la Taifa mimi namuuliza tu kwa mujibu wa katiba tunayo haki hiyo.

Mhe. Spika, baada ya suala hilo napenda niseme kwamba kwanza mkutano mkuu wa wadau. Mhe. Spika, unajua hili neno wadau linatumika lakini huu sio mkutano mkuu wa wadau, huu ni mkutano wa Baraza walioalikwa wadau. Maana yake Baraza lote lakini wadau ni wanne tu tena wakuchaguliwa. Mhe. Spika, lakini kuna madai mengi ambayo yanatoka katika visiwa hivi viwili, Zanzibar ina visiwa viwili vikubwa Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, kadri ya marekebisho ambayo tunayafanya basi yanatakiwa yende sambamba na ile hali halisi inayokwenda katika visiwa hivi viwili. Mhe. Spika,

katika sheria yote sijaona *consideration* iliyofanywa kwamba kuna visiwa viwili na vinatakiwa vifanyiwe haki. Kwa sababu suala la michezo ni suala ghali ambalo linahitaji fedha nyingi na matokeo yake hayaji katika fomu ya mapato, yanakuja katika ile *performance* itakayotokea na pengine kujenga afya na mustakabal wa vijana wetu.

Mhe. Spika, unapokuwa unasema Baraza la Michezo la Taifa lakini huoneshi dalili kama kuna visiwa viwili hiyo inakuwa haieleweki. Kwa mfano, hakuna pahali iliposemwa kwamba huo mkutano wa wadau vyama vingapi vitoke Pemba na vyama vingapi vya michezo vitoke Unguja. Mhe. Spika, ni kwamba maendeleo ya michezo katika visiwa viwili Unguja na Pemba na utayaona kwamba hayako *parallel* yako tofauti kabisa.

Mhe. Spika, suala la tatu ni kwamba kwa hapa Zanzibar pamoja na kuwepo baadhi ya vilabu na mambo mengine. Lakini tukizungumza mchezo zaidi unaotiliwa mkazo ni *football* lakini riadha na michezo mengine mingi ambayo duniani sasa hivi ukenda utaona kama sisi labda ni *as-hab-lkaafy* ikiwa tutawachukua vijana wetu tuwapeleke huko duniani basi huenda wakajikuta ni *as-hab-lkaafy* ni wale waliolala miaka mia tatu, halafu wakashtuliwa wakenda kule wakaona yale yaliopo.

Mimi hutizama katika TV za wenzetu naona sisi hasa hili suala la michezo niliwahi kusema siku moja sijui tuliache maana yake ukifikiria hao watu wanaoogelea sasa hivi hawaogelei moja kwa moja, hujirusha juu mtu akageuka mara nane hapa sisi hata ile kuogelea hatujui. Kwa hivyo, ukitutizama sisi hapa Zanzibar na ukitizama ulimwengu ulivyo ni kama watu waliolala miaka mia tatu halafu wakaamshwa wakenda kuona watu wanavyocheza michezo.

Mhe. Spika, pia nina ushahidi mwengine huwauliza vijana kwa nini mnaandika mpaka mabango timu za nje zikicheza. Mhe. Spika, ile *speed* ya mpira inavyokwenda kule Ulaya basi wanaacha kutizama timu za hapa wanatizama timu za Ulaya. Kwa sababu ya ile *speed* ya mpira na ule mpira wenyewe ulivyo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kuonesha hiyo michezo sisi hatuitilii maanani na haya yanayozungumzwa yana matatizo ni kuhusu suala la sherehe zetu. Hivi karibuni tumepata sherehe mbili mfululizo kule Pemba, sherehe kubwa za Mapinduzi basi sijasikia hata siku moja katika sherehe zile zaidi ya gwaride lile kama kuna michezo kama mashindani ya mipira na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa ufupi mchango wangu mimi nasema kwamba tusiandike maandishi ambayo hayana *application*, hayana ufuatiliaji wa kina. Ikiwa vijana wetu tunataka kwa kuondoka katika sheria iliyopita na kuingia katika sheria

mpya ya Baraza la Michezo moja ni ku-*improve* michezo hapa basi tuwe makini katika uwanja huo.

Mhe. Spika, la mwisho kama nilivyosema kwamba mimi sina mchango mkubwa ni kuwa sekeretariati itakuwa na majukumu yafuatayo.

Mhe. Spika, kifungu cha 22 kuhusu kusimamia kupanga na kuratibu shughuli zote za kila siku za Baraza, kufanya kazi nyengine kama itakavyoamriwa na Baraza.

Mhe. Spika, hii itakuwa haina kazi kwa sababu haina kazi hata moja ya ufuatiliaji inakaa inasubiri kufanya kazi za kila siku na kufanya kazi za kupangiwa, hakuna kazi za kufuatilia. Mhe. Spika, pia hakuna sekeretariati labla hili jina sekeretariati ndio lina mashaka kwa sababu *secretary* anakaa ndani juu ya meza ikawa hana ufuatiliaji. Mhe. Spika, kazi za michezo ni kwamba zinataka ufuatiliaji kwa sababu hakuna mchezo wowote unaofanywa ndani ya chumba. Mhe. Spika, michezo yote ifanywa ndani ya holi na ndio maana ikaitwa *indoor games*. Kwa hivyo, wale waliona ni ya afisi halafu ikawa sekeretariati kazi yao ni kukaa tu. Mhe. Spika, naomba irekebishwe, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, mimi nakushukuru sana kwanza naunga mkono hoja kwa sababu nimepata fursa nzuri sana ya kujadili mswada huu pamoja na wenzangu kama alivyotaja Mhe. Waziri na Mwenyekiti wa Kamati. Lakini sasa katika kuubariki na nikaonekana kwamba ni mdau wa mswada huu basi haitakuwa vizuri tukawaachia wale wajima wakalima sisi wenye shamba tukaa kivulini ikawa tunawatazama tu. Kwa maana hiyo na mimi mwenye shamba lazima sasa nijitokeze nikamate jembe nilime.

Mhe. Spika, mimi masahihisho nitakuwa sina maana yake yote nimeyataja katika kamati, lakini nataka nije katika fikra zangu ambazo pengine pale sikuzitoa ilikuwa hazijaja kichwani wakati ule au hata kama zingekuja simuhtadha wake kuzitoa pale.

Mhe. Spika, kwanza nataka nije kwenye suala la kuundwa kwa Baraza. Mhe. Spika, mswada unatamka kwamba kutakuwa na Baraza la Michezo ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea ambacho kitakuwa huru na kitakuwa na nembo na muhuri wake. Kwa maana hiyo ikiwa Baraza linalosimamia michezo lenyewe litakuwa linajitegemea kwa misingi hiyo hiyo na vyama hivi vya kitaifa na vya wilaya huko chini panapaswa vile vile vijitegemee. Mhe. Spika, ikiwa baba anatakiwa ajitegemee na watoto hivyo hivyo basi watalazimika wajitegemee. Kwa maana hiyo kwa mswada huu itabidi sasa *ZFA* tuwatafutie namna ya kujitegemea kwani tumewabeba vya kutosha na muda mrefu

wanaendeshwa kwa ruzuku ya serikali jambo ambalo sasa hivi halitakiwi na *FIFA* vyama vya michezo kuwa katika mfuko wa serikali.
FIFA hawataki mambo hayo kuendeshwa na serikali lakini sisi tulikuwa tunafanya kienyeji enyeji na kwa sababu walikuwa masikini tungewaachia wangekuwa hawana namna. Lakini sasa nafikiri tuwatafutie mtaji au tuwatafutie namna ya kuwasaidia ilimradi wajitegemee kama inavyotaka *FIFA* na kama inavyotaka sheria hii. Mtu tena akishakuwa na uwezo wa kushtakiwa, uwezo wa kujitafutia mapato, mihuri yake tena huyo anaachishwa maziwa anatakiwa ajitegemee mwenyewe.

Mhe. Spika, nije katika sheria kwenye kifungu cha 5 ambacho kimetaja kazi za Baraza, lakini kazi ambazo nataka kuzitilia mkazo ni mbili ambayo inasema kwa kushirikiana na mamlaka husika kusimamia na kusajili viwanja vya michezo ili kuepusha uvamizi wa viwanja hivyo. Mhe. Spika, bahati mzuri waziri anayeshughulika na ardhi yupo.

Mhe. Spika, hili ni tatizo letu kwani mheshimiwa unakuta kuna baadhi ya miji mengine inakuwa ina ufinyu sana wa viwanja kwa sababu watu wanajenga wanavyotaka. Kuna skuli nyingi hazina viwanja vya michezo na watu wamejenga mpaka wamesahau kwamba pahala pakiwa na skuli lazima pawe na viwanja vya michezo. Jambo hili zamani lilikuwa linatiliwa sana mkazo leo utakuta skuli inajengwa hata pale pahala pa kuwekea paredi hapana. Kwa hivyo, hili ni tatizo kubwa ukiacha humo mijini kama Hamamni humu inaeleweka lakini kama humo vijijini skuli inatakiwa iwe na kiwanja cha michezo. Hili Mhe. Waziri tungemuomba akakaa na Mhe. Waziri anayehusika na ardhi kwamba kila penye skuli basi atusaidie kupata ardhi kwa ajili ya michezo.

Mhe. Spika, vile vile akishatupatia basi tupatiwe na hatimiliki ili visije kuibiwa hivyo viwanja, kwani siku hizi viwanja vinaibiwa watu wanachukua wanavyotaka wanajenga, wengine wanafanyia shughuli zao za kibinafsi. Hili nalo linaua michezo.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumze kwa haraka haraka ni kuhusu suala la Kamati za Usuluhishi na Rufaa za Michezo. Mhe. Spika, Zanzibar pamoja na majirani zetu Bara michezo hasa ya mpira mara nyingi unakubwa na migogoro, mizozo isiyokwisha na ukitafuta sababu nyingi zinazouwa michezo basi ni hii mizozo na migogoro isiyokwisha. Mhe. Spika, sheria imetaja uwezo huo wa kuunda kamati za usuluhishi na rufaa, lakini mimi nadhani hata katika *level* yetu sisi kati ya Bara na Zanzibar nadhani ipo haja ya kuliangalia hili, tusiangalie katika vyama vyetu vya Zanzibar tu.

Lakini hata sisi kati ya *ZFA* na *TFF* kuna haja ya kuwa na kamati ya usuluhishi ya migogoro kwa sababu mara kwa mara inatokezea. Mimi naona sio jambo la busara kila wakati Mhe. Waziri akakae na Waziri mwenzake kushughulikia mambo ya mpira kwani wana mambo mengi ya kushughulikia. Mhe. Spika, kwa nini kusiwe na kamati za usuluhishi za aina hii katika ile *level* ya kitaifa.

Mhe. Spika, jengine ambalo limetajwa ni kuhusu mambo ya kushughulikia nidhamu. Nataka nimnukuu Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete) sijui katika shughuli gani lakini sio muda mfupi uliopita alisema kwamba: "Vyama vya Michezo Tanzania vina sifa kubwa kwa kuadhibu wana michezo". Mhe. Spika, alisema kosa dogo mtu atafungiwa miaka miwili au mitatu alisema wenzetu hili hawafanyi hivyo, zile adhabu kwa wana michezo zinakuwa ndogo, lakini hapa kosa dogo mtu anapigwa miaka miwili au mitatu.

Mhe. Spika, nafikiri katika hili suala la mabaraza kufikiria adhabu huu ni utamaduni wetu Wazanzibari kosa dogo tu mchezaji akifanya anafungiwa miaka miwili au mitatu, hivyo inakuwa tunauwa vipaji vya wachezaji. Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba huu wito wa Mhe. Rais wa kufikiria kwamba hizi adhabu kwa wana michezo kuzipunguza kidogo makali. Mhe. Spika, kwa kweli tungekuwa na utaratibu wa kufikiria hizi adhabu kuzilegeza sikusudii kuachia kabisa wakakosa nidhamu, lakini angalau kuzipunguza kwa sababu tunaua vipaji vya wana michezo wetu.

Mhe. Spika, jengine katika ule muundo wa Baraza wametajwa watu wengi mle ambao ni wajumbe. Lakini bahati mbaya sana katika Baraza hili hatukuwataja wale makatibu wa vyama, tumesema kuna uwakilishi wa vyama. Mhe. Spika, wawakilishi wanne kutoka Chama cha Taifa cha Michezo ambao watachaguliwa na mkutano mkuu wa wadau humu wametajwa.

Mimi nilikuwa nafikiria kitu kimoja kama wale makatibu wa vyama vya michezo tungekuwa tunao pale nahisi ingekuwa ni jambo zuri sana. Itakuwa tumepoteza sana kuwakosa makatibu wetu wa vyama hivi vya kitaifa vya michezo ama katika hili Baraza la Michezo au katika ule mkutano wa wadau. Kwa sababu ukitoa mwanya wa jumla kama ukisema chama cha kitaifa kitaleta mjumbe mmoja katika mkutano wa wadau, mimi nadhani bora tungekuwa specific tukawataka pale aje katibu kwa sababu katibu ndiye mtendaji mkuu wa kile chama.

Kwa hivyo, nadhani kuja yeye kuna uzito zaidi kuliko kuteuliwa tu mjumbe akaambiwa nenda wewe. Hili mimi nafikiri anapokwenda Katibu wa *ZFA* katika Baraza la Michezo nadhani kuna nguvu zaidi kuliko mtu mwengine aliyechaguliwa hivi hivi tu pengine uwezo wake ni mdogo.

Mhe. Spika, sasa hivi zaidi Zanzibar mchezo tunaoshughulikia sana ni mpira wa mguu na kidogo *netball* michezo mengine sote tunavyoshuhudia ni kuwa imefifia. Mhe. Spika, hapa Maisara pana sehemu panaitwa Gofu lakini ukiwauliza vijana wengi hawajui maana yake kwa nini pakaitwa Gofu. Kwa sababu huo mchezo wenyewe wa Gofu hawaujui wala hawajauona. Mhe. Spika, mimi naona bora mchezo wa gofu ufufuliwe, watu kama Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis, Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim ndio michezo yao.

Mhe. Spika, ile ndio michezo mizuri kwa hiyo ipo haja ya kuifufua michezo hiyo, kwani michezo ya gofu inachezwa na watu waliokuwa magwiji kidogo au waliokuwa watu wazima. Lakini leo ukimuliza mtu kwa nini pakaitwa gofu anaweza akafikiri kwa kuwa pana majumba mabovu. Hiyo sio maana yake hapaitwi Gofu kwa sababu ya majumba mabovu ule ni mchezo. Michezo kama hiyo ilikuwepo zamani lakini imekufa muda mrefu.

Mhe. Spika, mwishoni mwa miaka ya 80 Wizara ya Elimu Zanzibar ilianzisha diploma ya michezo hapo Beit-rass na nakumbuka palikuwa na walimu wawili walikuwa wanashughulikia mmoja akiitwa Lizbart na mmoja Mr. Vant. Kwa kweli hawa waliibua sana vibaji vya wana michezo kwa sababu pale palikuwa panafundishwa mpira wa miguu, tena huo mpira wa miguu pakifundishwa mpaka ukocha, wakifundisha netball kwa kweli palikuwa panafundishwa michezo isiyopungua kumi. Mhe. Spika, watu walikuwa wanafanya diploma haya masomo ya kawaida lakini ilikuwa muda wao mwingi wanaupoteza kwenye haya mambo ya michezo. Lakini naona tena ile programu ikafa, lakini iliibua vijana wengi sana na ilileta msisimko mkubwa sana.

Mhe. Spika, hili Mhe. Waziri labda anaweza akakaa na Mhe. Waziri wa Elimu mkatafuta uwezekano wa kulifufua kwa sababu michezo hasa inaanzia maskulini. Lakini hata ukisema unajenga *academia* za michezo utajenga ngapi? Utajenga moja ya Dole wakati Pemba haipo basi itakuwa haina faida yoyote itasaidia watu wachache. Mhe. Spika, nadhani tukiwa na programu kama ile ya kuanza maskulini basi tunaweza tukaibua michezo mengi.
Mhe. Spika, mimi nakumbuka wakati nasoma kulikuwa kuna michezo mingi kama kwenda mbio ukifika unakula andazi, basi ilikuwa hata na mimi sishindwi katika michezo kama hiyo kwani nilikuwa nafuatilia lile andazi. Lakini leo yote hii haipo kulikuwa na michezo ya magunia, kufukuza kuku yote hiyo imepotea. Kwa hivyo, mheshimiwa kwa sababu ya muda mimi nilisimama kwa sababu naona watu kidogo kipindi hiki wamechoka kusoma miswada, wengi wamechoka lakini kwa sababu mimi sijachoka nikaona nichukue nafasi hii angalau niimalizie hii robo saa iliyobakia, jioni nina imani utapokea maombi yasiyopungua 20 ya wachangiaji.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

(Saa 6:00 Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kwa jioni ya leo *Yaumul-Jumaa* kunipa nafasi hii ya awali ili na mimi nitie mchango wangu kidogo katika mswada huu adhimu.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye anapaswa kushukuriwa, basi naona sitakuwa na mengi ya kuzungumza. Ingawaje kwa sababu huu mswada ni wangu, nimeupitia kwenye kamati vizuri, tumeurekebisha palipostahiki kurekebishwa, lakini isingekuwa jambo la busara kuwa nisitie hata ubani kidogo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, usije ukashangaa kuwa nitazungumza mambo machache ukaona labda leo sikupata cha mchana kizuri, aa. Sasa hivi hapa niko pomoni.

Mhe. Spika, nataka nianze katika mswada huu kwenye ukurasa wa 24 kifungu cha 3 kinachozungumzia kuundwa kwa Baraza. Hapa tunaambiwa kuwa kutakuwa na Baraza la Michezo ambalo litakuwa na sifa zake hapo zimetolewa Baraza hili litakavyokuwa.

Mhe. Spika, kuundwa kwa Baraza la Michezo ni jambo zuri, tena zuri sana. Kwa sababu kuundwa kwa Baraza hili kutakuwa na maana ya kwanza kama michezo ni mnyama itakuwa ina mchungaji, lakini la pili mchungaji huwa ana wajibu katika uchunga wake kutafuta malisho, kutafuta pahala pa kuwalaza ng'ombe wake. Kwa hivyo, na hili Baraza nalo linatakiwa madhali linaundwa tunatarajia kuwa litakuwa ni mchungaji wa vyama vya michezo katika hali zote zinazostahiki.

Mhe. Spika, nikitoka hapo labda nije katika kazi za Baraza. Baraza hili limepewa kazi kadhaa wa kadhaa sina haja ya kuzisoma, kwa sababu tayari zipo katika mswada. Labda ninalotaka kulizungumzia dogo tu katika hizi kazi za Baraza. Ni kwamba mtu anapopewa kazi basi anapaswa aifanye ile kazi aliyopewa, kama haiwezi basi aseme mimi kazi hii siiwezi. Kwa hivyo, tunatarajia Baraza tumelipangia kazi, kazi hizi ni nzito kwa kiasi fulani kwa sababu zinahusiana na shughuli za michezo na michezo ni mingi sana, na michezo ina mambo mengi sana inayotaka. Kwa hivyo, kazi hizi za Baraza kama zitafanywa vizuri ni mategemeo yetu kuwa michezo itakua na itatuletea licha ya jina la Zanzibar lakini pia uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mswada huu kuna mamlaka na uwezo wa Baraza, Baraza limepewa mamlaka yake na uwezo, sasa hili ni jambo moja kidogo lina hatari ndani yake. Kwa sababu unapopewa mamlaka na uwezo kuna mambo mawili, ama utayatumia vizuri madaraka yako na uwezo uliopewa au utatumia ubinafsi wako kwa kutumia uwezo uliopewa. Sasa endapo Baraza hili litatumia uwezo liliopewa vizuri tunatarajia matokeo mazuri, lakini endapo uwezo huu waliopewa wataanza kuweka ubinafsi mbele hatutafika pahali.

Kwa hivyo, kwa mawazo yangu kwa sababu huwa mara nyingi napenda kutoa nasaha katika Baraza hili na nasihi Baraza hili litakapoundwa basi ubinafsi uwekwe mbali. Watu wasije wakatumia uwezo waliopewa kwa kukandamiza timu ambazo wao hawazipendi, au kwa sababu Wajumbe wa Baraza kwa sababu hawakukatazwa pahali kuwa na wao wako katika timu. Sasa kwa kuwa na wao watakuwa na timu zao hawa Wajumbe wa Baraza uwezo huu tunaowapa wasije wakautumia vibaya katika kutetea timu zao. Hili nalo ni jambo muhimu sana ambalo lingefaa lizingatiwe.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 26 katika kifungu cha Mikutano ya Baraza. Baraza tumeliambia kuwa likutane angalau mara moja kila miezi mitatu kwa mikutano ya kawaida, ya dharura tena yoyote ile itakayotokea madhali ni dharua itakuwa ni ya dharura.

Uzoefu Mhe. Spika, unavyoonesha mara nyingi Mabaraza mengi yanayopangiwa ndani ya sheria muda wa kukutana huwa hayakutani katika muda uliopangwa. Kutokana na hilo, ile azma nzuri ya sheria inayotungwa hufisidika, kwa sababu huwa Baraza linapokutana linapanga mipango mbali mbali. Sasa ikiwa halikukutana kama lilivyopangiwa mipango ile inakuwa haiwezi kupangika kwa sababu Baraza hawezi kuwa mmoja kakaa kwake na mwengine akakaa huko wakapigiana simu, haya leo tufanye nini, tufanye vipi, lazima wakutane na ndio maana ikawekwa hii kuwa ni mikutano ya Baraza iwe angalau mara moja katika kila miezi mitatu.

Lakini pia Mhe. Spika, katika mikutano hiyo kutakuwa nauamuzi kama kinavyosema kifungu cha 10, uamuzi huu lazima uwe uamuzi unaofaa. Lazima hawa wajumbe wa Baraza watakaoteuliwa wawe watu makini ili uamnuzi wowote watakaoutoa usije ukaturudisha nyuma badala ya kutupeleka mbele.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika kifungu cha kumbu kumbu za mikutano ya Baraza. Katibu Mtendaji kapewa kazi ya kutunza kumbukumbu, kadiri ninavyoelewa kumbukumbu ni siri ya kikao. Mara nyengine Mhe. Spika, makatibu au watu mbali mbali wanakuwa na marafiki, wanaamua kitu kwenye kikao kabla ya kutendeka kitu kile tayari watu nje wanakizungumza. Hii maana yake kumbukumbu hazikudhibitiwa vizuri.

Sasa hili lina pande mbili, upande mmoja wa huyu mtunza kumbukumbu, lakini upande mmoja wa hawa wajumbe. Kwa sababu mjumbe anaweza akatoa taarifa ya kikao kinyume na utaratibu. Lakini pia katibu mtendaji kwa sababu ndiye anayezitunza kumbukumbu inawezekana zimeshapita hata mwaka mzima lakini kuna kitu akaja akakitoa ambacho kilikuwa hakistahiki kutolewa katika pahali pale alipokitoa. Kwa hivyo, pia nashauri hapa kuwa kumbukumbu katibu mtendaji azitunze vizuri na azifuate taratibu zile zilizokusudiwa labda katika muda wa uongozi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 15 tumesema hapa kuwa muda wa uongozi Mjumbe wa Baraza ukiacha wale ambao wataingia kwa nyazifa zao. Akakaa katika uongozi kwa kipindi cha miaka mitatu na pia anaweza kuchaguliwa kwa kipindi chengine. Nilivyofahamu vipindi vya mwisho vya uwezo wa kukaa katika Baraza ni viwili, kwa sababu ataweza kuchaguliwa kipindi chengine kimoja na kile cha mwanzo itakuwa vipindi viwili. Lakini je, kama mtu huyu bado ule ujuzi wake alionao na umuhimu wake unahitajika bado ndani ya Baraza, iwe basi tena hivi vipindi viwili asichaguliwe tena?

Sasa sijui hili tutalifanyaje? Kwa sababu anaweza akatokea mtu ikawa utaalamu wake na ujuzi wake unasaidia sana ndani ya Baraza na ikaonekana kama huyu bora angeendelea kubaki kuwa mjumbe wa Baraza, lakini tumeshamuwekea vikwazo kuwa vikimaliza vipindi viwili basi. Je, huyu nae hatuoni kama tutajikosesha hapa kidogo jambo zuri?

Nafikiri hili lingefikiriwa na likatafutiwa utaratibu labda wa kuwa ikiwa kuna mtu anayeonekana kutokana na vitendo vyake michezo inakua basi bado apewe nafasi zaidi azidi kukuza na wakati huo huo atayarishwe mtu mwengine wa kuja kukama ile nafasi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika Mrajis wa Vyama vya Michezo kifungu cha 18. Katika kifungu hiki Mhe. Spika, tumeambiwa kuwa waziri atamteua mrajis na mrajis atatunza orodha hizo za vyama vya michezo vilivyosajiliwa. Hapa nina wazo moja, huyu mrajis kwa inavyoelekea hapa atafanya kazi ya kitaifa, atarajis vyama vyote lakini katika ngazi ya taifa.

Nilifikiria kuwa mrajis angekuwa na wasaidizi wake katika wilaya, ili kila wilaya ikawa kuna urajis wa wilaya halafu ndio kukawa na urajis wa pamoja wa wote. Kwa sababu wasi wasi wangu ni kuwa pengine si vyama vyote vitakuwa na uwezo wa kufika kwenda kujirajis kwa mrajis mkuu, lakini wanaweza wakajirajis katika wilaya na wilaya wakisharajis wao wakapeleka kwa mrajis mkuu. Hili nafikiri ni moja katika pendekezo nililolifikiria baada ya kukaa na kuangalia vizuri huu mswada wetu.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 23 kwamba Baraza linaweza kuanzisha kamati ndogo ndogo kwa madhumuni ya kutekeleza kazi maalum kwa kadiri itakavyohitajika. Kamati hizi zinaonekana ni kamati za kuwa na kutokuwa, yaani ni kamati za muda, kukitokea jambo basi inaundwa kamati inafanya kazi likimalizika kamati ile tayari kazi yake imekwisha wanarudi katika shughuli zao za kawaida.

Sasa katika uundaji wa kamati hizi ndogo ndogo, kuna kanuni zitakazowekwa jinsi ya kuunda kamati hizo au ndio hii sheria imetosha kutoa mwanya wa kuunda kamati ndogo ndogo? Kwa sababu bila shaka kamati ndogo ndogo itabidi ziwe na utaratibu wake, udogo wake uwe kiasi gain? Ukubwa wake uwe kiasi gain? Ziundwe vipi? Zifanye kazi vipi? Nafikiri katika kanuni vitu kama hivi vinahitajika viweko ili mambo yaweze kwenda vizuri zaidi.

Halafu hapo hapo kwenye mabaraza ya michezo ya wilaya, kwa kweli ni jambo zuri kufanya haya mabaraza ya wilaya. Lakini pia nataka nitoe indhari kuwa Baraza la Taifa la Michezo liwe likitupa jicho sana katika Mabaraza ya Wilaya. Kwa sababu ninajua kuna timu nyingi zimekufa kutokana na uongozi wa michezo wa wilaya.

Kwa hivyo, hapa lazima tuwe na hadhari kubwa katika suala hili la Mabaraza ya Wilaya. Pamoja na kuwa tumeambiwa hawa watafanya kazi chini ya Mkuu wa Wilaya, lakini Mkuu wa Wilaya pia ni binadamu kama binadamu mwengine. Kwa hivyo, lazima tuchukue hatua za kufaa katika kuona kuwa hayo Mabaraza ya Wilaya yanafanya kazi vizuri.
Mhe. Spika, labda niuache kidogo huu mswada nije katika baadhi ya mambo mengine. Unajua Mhe. Spika, wengi hawajui kama mimi nilikuwa mwanamichezo, wanafikiria nilikuwa shekhe na mpaka hivi leo ndio naonekana hivi nilivyo.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa mwanamichezo, haizuru kwenye *foot ball* nikipiga mbio na watu tu, maana yake kuna mcheza mpira na mpiga mbio na watu, mimi nilikuwa mpiga mbio na watu. Lakini kwenye uongozi wa michezo basi nilikuwa hodari, usije ukashangaa kuwa nilikuwa mwenyekiti wa *net ball* wa Pemba nzima elimu.

Mhe. Spika, usishangae pia ukisikia nilikuwa kocha wa net ball, lakini usishangae pia kuwa mimi na Maalim Abdalla Rajab Haji tulianzisha timu mbili kila mmoja timu yake pale Mkoani. Timu yangu ilikuwa ikiitwa Mapinduzi na yake yeye ilikuwa ikiitwa *National*, ya watoto wadogo. Na tukaichukua mpaka wakawa watu wazima na walikuwa wakicheza mpira mkubwa sana kwa wakati huo.

Sasa uzoefu mdogo ninao katika mambo haya ya michezo na ndio maana nikasema kuwa nahitaji nitoe kidogo ule uzoefu wangu nilionao pengine unaweza ukasaidia.

Kwanza labda nizungumzie kuhusu michezo mbali mbali. Michezo Mhe. Spika, kama walivyosema wengine iko mingi sana, kila mchezo una uzuri wake, kila mchezo una sheria zake, kila mchezo una uongozi wake. Sasa Baraza hili moja katika kazi zake ni kuhakikisha michezo yote iliyopo basi inashughulikiwa, inakua na inafuata taratibu zile zinazotakiwa. Kuna michezo mingi hivi sasa haishughulikiwi watu hujifanyia tu wenyewe. Labda siku ya sherehe inaweza ikaletwa kama sehemu ya sherehe tu, lakini haiendelezwi kama sehemu ya mchezo.

Kwa mfano, kuna siku utasikia kuna mechi ya bao, utasikia kuna mechi ya karata kwenye sherehe, lakini katika hali halisi hazitajwi karata wala bao. Baraza linashughulikia michezo miwili tu kwa sana iko ne mingine kidogo lakini mingine haishughulikiwi kabisa inajishughulikia wenyewe. Kwa sababu "Isiyo na mkami hujikamua". Kwa hivyo, kuna mengine hujikama wenyewe kwa sababu haina mkami.

Mimi nilikuwa muamuzi wa michezo ya riadha na cheti ninacho, nilikuwa hodari zaidi kwa michezo ya *field, long jump, triple jump* na mingineyo. Nimeshaamua michezo kama hiyo katika UMISETA, UMISAMA. Kwa hivyoi, michezo hii ya riadha kwa mfano, inahitaji nayo kushughulikiwa hata kama hakuna mashindani mbele yetu, iwe ni kitu cha kawaida ushughulikiaji wa hii michezo. Tusingoje mpaka mwezi ujao kuna mashindani ya *Common Wealth* tukaanza kuweka watu kambini leo tunatayarisha eti wakashindane *Common Wealth,* hapo tutakuwa hatujafanya kitu cha maana.

Lakini hili ni jambo la kila siku, kama tunavyokula kila siku, tunavyokwenda haja kila siku, basi na michezo yote inatakiwa iendelezwe kila siku. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani hilo ni moja katika mambo muhimu ya kufanya kutokana na Baraza hili ambalo tunaliunda.

Mhe. Spika, moja katika mambo muhimu katika michezo ni nidhamu. Ni kawaida ya wachezaji wanaojiona wao mahodari kutokuwa na nidhamu nzuri, hii ni kawaida, wale wenzangu mimi wale wanakuwa na nidhamu mia kwa mia. Kwa bahati mbaya katika baadhi ya vilabu wale mahodari waliokuwa hawana nidhamu ndio wanaoshughulikiwa zaidi, si kwa nidhamu, wanashughulikiwa zaidi kama kuna mechi, nini, hakuna adabu kwao aa, tusije tukamkera akaja akatukosesha magoli. Sasa hili nalo ni jambo ambalo lazima lisimamiwe kwa nguvu zote ili wachezaji wetu wawe na nidhamu.

Kwa sababu watakapokuwa na nidhamu kwanza watakuza jina la nchi yetu, watakapokwenda nje kucheza na timu nyengine wakaonesha nidhamu basi jina la nchi yetu linakuja juu. Halafu wakaonesha na mchezo mzuri hapo tena ndio aa humaliza tu mambo. Kwa hivyo, nidhamu ni kitu muhimu.

Kwa wale wenye nidhamu aende pale mwalimu ambaye wao wanaona kuwa hajui lakini watamfuata atakavyofundisha. Lakini wale wanaojua waliokuwa hawana nidhamu akenda mwalimu kwanza wanamtizama mwalimu huyu ana ujuzi gani, wakiona ujuzi wake mdogo hafuatwi tena huyo. Lakini huwezi kujua ujuzi wa mtu anao mwenyewe ndani ya nafsi yake, ngojea kwanza akufundishe umfuate aliyokufundisha ata usishinde hapo tena ndio utasema kumbe bwana huyu hatufai.

Kwa hivyo, suala la nidhamu kwa wachezaji ni moja lakini pia suala la nidhamu kwa viongozi wa timu na viongozi wa michezo kwa jumla ni jambo jengine ambalo nalo lina umuhimu wake.

Mhe. Spika, jambo jengine muhimu katika michezo ni uadilifu, uadilifu ni muhimu sana katika michezo, uadilifu wa wachezaji, uadilifu wa viongozi wa timu, uadilifu wa mabaraza. Huu ni kitu muhimu sana. mara nyingi utasikia ah! bwana wale wamekula pesa bwana wamefungwa, wamewaachia, ni kitu gani? Ni ukosefu wa uadilifu. Kama kuna uadilifu humuachii mtu hata siku moja.

Nashukuru kuwa safari hii timu yetu imekuwa adilifu sana, haikuwaachia wenzetu wa Tanzania Bara, piga vitu basi. Ule ndio uadilifu unaotakiwa, sio mtu achukue pesa halafu afungishe, hatwendi namna hiyo. Lakini kwa kweli nashukuru sana kuwa hilo limefanyika vizuri.

Mhe. Spika, michezo inahitaji nyezo, nyezo za michezo ziko za aina nyingi kwa sababu kila mchezo una nyezo zake. Lakini pamoja na nyezo zote hizo michezo inahitaji viwanja vya kuchezea.

Kuna timu ambazo zina viwanja vyao hivi sasa, kuna timu ambazo hazina viwanja huwa wananyang'anyiana hicho hicho kiwanja kimoja kilichopo timu mbali mbali. Lakini pia kuna timu ambazo tayari wana viwanja, tayari wameshalipa pesa katika wizara inayohusikana na ardhi lakini bado hatimiliki hawajapata, wakiuliza wanaambiwa bado hazijarudi kwa Mhe. Waziri. Naomba watu kama hawa mkiwajua basi muwachochelee moto kule angalau zile ahadi zitoke upesi.
Moja katika timu hizo ni timu ya *Shooting Star* ya Mkoani. Imeshalipa katika wizara inayohusika na ardhi kupatiwa hatimiliki ya kiwanja cha Mpika tango. Naomba muwachochelee moto wapate warka, kwa sababu vyenginevyo kile kiwanja kitavamiwa kwa sababu itakuwa hakuna hatimiliki na kikivamiwa ni

tatizo. Kwa hivyo, naomba hili nalo muchochee chochee huko jikoni ili wapate huu waraka wao usichelewe sana.

La mwisho Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza kwa saa hizi ni lile suala la vyama kujihusisha na siasa. Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu na haya ni yangu, ni kuwa vyama vya siasa vingetakiwa vianzishe michezo, vingetakiwa vianzishe timu na timu zile zikishindana ingelikuwa ni ushindani wa hali ya juu na michezo ingekua mara moja. kwa hivyo, mimi lile wazo la kuwa timu zisijishughulishe na siasa siliwafiki kikamilifu, naona vyama vya siasa vingetakiwa vianzishe timu zao ili timu zile nazo ziwe zinakuza michezo.

Mhe. Spika, Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Ali Salim, Alhaji, Mwenyekiti Mstaafu wa *Net ball*. (*Kicheko*)

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii, yeye kaweka ubani na mimi naweka udi kidogo harufu ipate kuwa nzuri, angalau na sisi tuweke baraka zetu katika mswada huu.

Mhe. Spika, nitangulie kusema kwamba naunga mkono huu mswada. Lakini pia nitoe maoni yangu machache ambayo katika kupitia pitia huku na kule nimeviona, sasa huenda vikawa vinakubalika vikaweza kusaidia.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake, pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya mpaka leo mswada huu uko mbele yetu.
Mhe. Spika, nataka nianze mchango wangu katika mswada huu sehemu ya pili kifungu cha 3. Maneno yote yaliyokuwepo hapa nakubaliana nayo lakini nahisi kimepungua kitu kimoja kidogo lakini kikubwa.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu na nitapenda nikinukuu kifungu cha 3 © kama ifuatavyo. “Baraza litakuwa na uwezo wa kumiliki, kutoa, kununua au kumiliki mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake”.

Sasa mimi nimeona kumepungua kitu cha kupokea, basi watakuwa wanatoa tu hawa hawapokei. Kwa hiyo, ningeomba Baraza lipokee basi kama kuna kitu mtu kaamua analeta, pengine Mhe. Juma Duni Haji au Mhe. Nassor Ahmed Mazrui katoka alikotoka kaja na mzigo wake kwa mfano jezi au kitu kingine chochote, basi Baraza liwe lina uwezo wa kupokea vile vile.

Mhe. Spika, niingie kifungu cha 19 kinachohusiana na mambo ya Mrajis. Kifungu cha 19(d) (iii) kama kilivyo na nadhani hiki ndio mwenzangu alipomalizia katika kipengele kile kile cha kwamba "Iwapo kinajishughulisha na mambo ya siasa" itakuwa chama cha mchezo.

Mimi naona kama hakuna haja ya hiki kifungu cha 3 kuwepo na sababu zangu ni kama zile Mhe. Mwakilishi hapa amemalizia. Unapoweka kitu kama hiki tayari unakereketa kitu katika nafsi. Mimi nadhani tuangalie zaidi kuendeleza michezo katika hali ya kuweka uzalendo mbele.

Sasa tukitanguliza uzalendo Mhe. Spika, basi nafikiri tutakuwa kama Waingereza. Muingereza hata kama ana timu yake Chelsea au Manchester lakini ikicheza timu ya kwao England pahala popote na ndio maana wanaambiwa watu wakorofi, lakini ni ile hamasa ya uzalendo wa kuona kwamba wanataka timu yao waishangilie waone kwamba ule ushindi unapatikana. Kwa kweli hii inakuwa inasababisha mambo mengi mazuri katika nchi.

Sasa nadhani kwa hali zetu sisi hususan nazungumzia uzoefu katika nchi yetu na mambo ya siasa hili linapelekea kuturejesha nyuma sana. Kwa sababu mtu anaweza kumtazama fulani kwamba huyu kwa alivyo ni jambo kadhaa, kwa hiyo tunakuwa tayari tunaanza kuona huyu anafaa, huyu hafai. Mimi nadhani mtu aachwe apendelee anapopendelea ile ni nafsi yake na ni haki yake ya kikatiba, ni uamuzi wake.

Lakini katika suala kama tunalolilenga mahsusi na hapa tunazungumza michezo, basi nadhani suala la siasa tusilitazame kabisa, mtu aachwe na ushabiki wake wa kisiasa, mikutano, zahma, tukija kwenye michezo sote tunakuwa kitu kimoja na hapo tutaona mafanikio na ufanisi wa michezo utakavyokuwa.

Mhe. Spika, katika hapa mimi nilikuwa nadhani sana na hasa kwa kuwa tumo kwenye maridhiano tuone tunakwenda *step forward*, badala ya kwamba tunarudi nyuma basi tusirudi nyuma tuendelee mbele. Twende katika kuona kwamba michezo ni suala la Zanzibar na Wazanzibari wenyewe, pamoja na timu tofauti zilizokuwepo lakini tunaposimamia timu kama *Zanzibar Heroes* basi iwe sote tunajisikia kwamba ni yetu. Tusije tukaitazama kama labda hii timu inaonekana ya CCM au inaonekana ni ya CUF tutakuwa tunapunguza ladha ya michezo katika nchi yetu lakini pia tutapunguza ari na hamasa.

Mhe. Spika, nadhani mengi yameshasemwa na wenzangu kuhusu hili na mimi nilikuwa napenda tu niliongezee ili kuonesha ile msisitizo kwamba siasa kwa

namna moja au nyengine inachafua, tukiingiza pahala popote itatuchafulia. Kwa hiyo, ningependa sana hiki kifungu kingeondoshwa kabisa kisiwepo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nakwenda sehemu ya tatu na hapa nimeguswa na tafsiri tu au pengine Uswahili. Sehemu ya tatu inasema "Mkutano wa Wadau", sasa mimi niko hapa kwa wadau ni kina nani hawa hasa waliokusudiwa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nafikiri ungelikuwa ni mkutano wa wanachama, maana yake kwa vyovyote wadau waliokusudiwa hapa ni wahusika wanaoshughulika na mambo ya michezo. Kwa hiyo, wale wanachama wa michezo ambao nitaendelea zaidi kuelezea mbele hapa kwamba kuna vitu havijirudii lakini mimi nadhani kama vyengine vingekuwa havina haja kwa sababu tayari tuna Baraza, tayari kuna sekretarieti. Halafu na huu mkutano wa wadau kwa jinsi ulivyoelezwa ni chombo kingine kinachofanana na hivi viwili vilivyotangulia.

Mhe. Spika, kwa mimi nilikuwa nadhani kwamba ungelikuwa ni mkutano mkuu wa wanachama wote. Wanamichezo tunaelewa tukizungumza hivvyo, kuna watu ni wanachama wa kadi hasa. Sasa tuchukulie suala la aina hiyo kwamba hiki chombo ni chetu sote kwa hiyo hapo hakutakuwa huyu hivi, huyu vile. Ni mwanachama wa michezo kwa hiyo kile ni chombo changu na ningependekeza kwamba kuwe kuna uwanachama wa kadi. Ukiwepo uwanachama wa kadi sasa hapa tutakuwa na mkutano mkuu wa wadau wote utakaokuwa unafanyika mwaka mara moja.
Hilo likikubalika basi litaambuza na katika kifungu cha 31 sehemu ya nne ambayo inazungumzia mambo ya fedha, matumizi na ukaguzi wa hesabu. Ikikubalika hivyo, kifungu cha 31 kuna (a), (b), (c), (d) na (e) ningeomba iongezwe na (f) iwe ni ada za wanachama kwamba hicho kiwe ni chanzo vile vile cha kupatia fedha. Sasa tutakapokuwa na vyanzo vingi zaidi vya kupatia fedha na katika chanzo muhimu zaidi ni kile cha mwanachama mwenyewe anataka chombo chake kiwepo na kwa sababu kaja kwa hiari yake kachukua kadi kawa mwanachama sidhani kama kutakuwa na matatizo ya kuwa analipa ada yake.

Sasa hizi ada Mhe. Spika, zitasaidia kwa namna pana zaidi kuliko kusubiri ruzuku ambazo tunajua utaratibu wake unavyokwenda leo zipo kesho hazipo, kumetokea hili na lile. Lakini pia kukaa tukamsubiri mfadhili ana hiari yake na wakati wake kuja. Sasa hii inakuwa ni chanzo ambacho hakina mjadala, ni chanzo ambacho kwa kweli tunaweza hata kukikopea, kukipangia mahesabu na kila kitu, lakini huwezi kukaa ukapanga mipango yako kwa pesa unayotarajia tu fulani atakugaia. Pengine mwaka huu kaamua hakugaii wewe anamgaia mtu mwengine.

Mhe. Spika, kwa kawaida ya mambo haya tunaambiwa nyongeza huenda kwenye fungu, haiendi pahala hapana kitu utaongeza nini. Sasa nadhani shike shike na mwenyewe nyuma. Hiki chombo ikiwa sisi wenyewe tayari tunaonekana tunajitutumua basi hata wale wanaotusaidia wataona haja na hoja ya kwamba watusaidie kwa sababu wenyewe masikini wanajitahidi lakini ndio watu wenyewe uwezo wao mdogo kwa hiyo angalau tutie hiki. Lakini wakiona mmekaa tu mnasubiri ruzuku, mnasubiri wafadhili, kila mtu ataona aaa hawa bwana hawawezi hata kula yao. Mhe. Spika, si kweli japo uji tutakoroga, sasa tena mtu akileta pishori yake itakuwa mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, sikuwa na mchango mkubwa sana. Kama nilivyotangulia kusema kwamba naunga mkono mia kwa mia lakini ilikuwa kwa ile hamu ya uanamichezo ambayo ninayo na nadhani kwa Zanzibar hili ni kitu sare. Wazanzibari mimi nasema takriban sote Mhe. Spika, ni watu ambao tunapenda sana michezo na ndio maana aliyekuwa si Manchester basi Liverpool, maana yake hao ndio waasisi zaidi, tena imeingia Arsenal na Chelesea wamepandia pandia tu hawa wamekuja juzi juzi.

Mhe. Spika, kwa nini tunapenda Liverpool na Manchester? Sasa hivi na vitu vyengine sijui vinaingia Barcelona na nani, ni kwa sababu kwetu sisi michezo bado hatujaipa ile nafasi yake. Inakosa nafasi kwa sababu tunaiachia siasa ikae juu ya michezo. Inakaa vipi, ndio kama hivyo. Aaaa maana yake akionekana ana siasa siasa mtoe. Hivyo Zanzibar hii nani si mwanasiasa. Mhe. Spika, mimi mpaka mtoto wangu wa miaka miwili wanasiasa wote, wananyonya wako kwenye ziwa wanasiasa. Hii maana yake haina mjadala wala haitaki tochi.

Sasa nasema tukiweka kipengele kile, imebidi nirudie Mhe. Spika, kwa msisitizo, tutakuwa tunajiharibia. Mimi nataka ile ari na sherehe kubwa tunazofanyiwa Michenzani pale, watu wanapiga misere usiku wa kucha hatulali wanasherehekea Manchester, ukiuliza nini, Manchester. Mhe. Spika, sisi tunataka washerehekee *Zanzibar Heroes.* Hatukatai mtu anaweza kupenda kitu kingine lakini tuwarudishe watu katika kujiona wazalendo wanapenda chao.

Katika maneno ya hekma ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitwambia japo mimi sikuwepo alipokuwa akisema lakini nilisikia kama kayasema hayo kwamba “Tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako”. Sasa namna ya kutukuza ndio hiyo tuondoshe mambo mengine haya madogo madogo ambayo kwa kweli tukiyapa nafasi yanatuharibia. Jambo lolote ambalo tunataka tupate ufanisi na mafanikio siasa tuiwekeni pembeni tusiipe nafasi kabisa tusubiri kampeni, mimi napitia upande huu basi nitakuwa hivi, mimi napitia upande huu nitakuwa hivi.

Lakini katika mambo yetu likiwemo hili la michezo na mengine, Mhe. Spika, wewe mwenyewe na wajumbe wako katika Baraza hili mashahidi, tunasimama sote kama Wazanzibari basi lazima tutafanikiwa. Maana yake hiyo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu siilazimishi kwamba nasema mimi aaa. Anasema mkiungana yeye yuko pamoja na nyinyi.

Kwa hiyo Mhe. Spika, pamoja na Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu nakunasihini sana kwamba hiki kipengele kinachozungumza harufu ya siasa hapa kiondoke. Kuna watu wana uwezo mzuri sana lakini huna vya kumfanya atoke kwenye chama chake tutamkosa, tukimkosa ufanisi umepungua. Sasa sisi hatutaki ufanisi upungue, tutakapokaa kwenye michezo tutafanya michezo, tukiondoka hapo mtu atafanya shughuli zake nyengine. Vyenginevyo itabidi tuongeze vipengele vingi ambavyo mwisho wake mswada huu utakuwa hauna haja ya kuwepo itabidi urudi.

Kwa sababu utakuja utasema asije akaonekana mlevi mlevi. Haya! Wachezaji kama Roone au kuna mchezaji mmoja akiiitwa Kim, yule kwa chupa hatari lakini ni mchezaji mzuri. Sasa Mhe. Spika, ukim-*judge* mtu kwa vitu vidogo vidogo tunaweza kukosa mambo mengi mazuri mazuri ambayo yatatupelekea kupata ufanisi siku za usoni zijazo na zijazo.

Sasa ningeomba sana katika masuala ya michezo na jambo jengine lolote ambalo tunataka kulianzisha katika nchi yetu, basi ufanisi wake utapatikana kwa sote kuwa kitu kimoja tofauti tukaziacha kwa wakati wake. Maana yake kila jambo Mhe. Spika, lina wakati wake. Nilikuwa naomba sana kifungu hiki kingeondoka ili tupate ufanisi huo.

Lakini pia ningemuomba sana Mhe. Waziri katika kile kipengele kinachozungumza wadau basi iwe ni mkutano wa wanachama wote na neno wadau liondoke. Lakini tuongeze kifungu kingine ambacho kitatukusanyia mapato. Kuwe na ada za wanachama ambazo zitaweza kuliendeleza Baraza letu na litaweza kuendeleza michezo katika nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuchangia Mswada wa Baraza la Taifa la Michezo. Mhe. Spika, awali ya yote nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake katika wizara hii kwa kutuletea mswada huu ili kupata kuujadili na kuupitisha.

Mhe. Spika, ukurasa wa 25 kifungu cha 6 “Mamlaka na uwezo wa Baraza”. Katika kupanga na kushawishi Mabaraza ya Michezo ya Wilaya, hii ya kuanzisha Mabaraza ya Wilaya ya Michezo italeta matumaini mazuri kwa wanamichezo wetu. Kama inavyoeleweka baadhi ya wilaya nyingi zina

wanamichezo wazuri tu ambao wanaweza kuimarisha timu kama za mipira au za michezo mingine na tukapatiwa sifa katika nchi yetu.

Kuna haja Mabaraza haya ya Wilaya kuanzishwa ili wakawa na kazi kubwa ya kutafuta na kutazama wanamichezo gani wazuri tukawa nao na kuwaimarisha katika timu moja au mbili katika nchi yetu.

Kwa sababu hapo zamani tulikuwa tukivuma sana Zanzibar kwa wanamichezo wengi tu wakiwemo wa mipira. Ilikuwa timu zinazotoka Zanzibar zilikuwa zinaleta matumaini makubwa ya ushindi. Lakini utakuta kipindi hiki kuna timu moja tu ndio inayonguruma *Zanzibar Heroes* ambayo utakuta wachezaji wake wengi wamewapata kutoka kijijini. Kwa hiyo, utakuta hata Mabaraza ya Michezo yataanzishwa vijijini inawezekana tukapata wachezaji wazuri na timu zetu zikawa imara.

Kwa sababu sasa hivi hapa mjini baadhi ya timu nyingi zimetawaliwa na wachezaji ambao baadhi yao hawana nguvu ya kucheza mpira wa kutegemewa, wameshawishika na vikundi vya ulevi wa unga na bangi.

Kwa hiyo, kama tutawatafuta hasa vijijini tutawapata wanamichezo waliokomaa kwa vyakula vyenye virutubisho ambao waliokuwa makini kwa kutuletea matumaini. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri akaangalia sana hapa ili tukapata wachezaji waliokuwa imara na kutuletea ushindi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kama walivyoeleza baadhi ya wajumbe wengi hapa kuwa michezo ni kitu kinacholeta faida kwa wananchi na hata kwa yule mwanamichezo mwenyewe. Kama mwili wako utaufanya ni wa michezo basi alimradi mambo mengi ya maradhi yatakuepuka. Mhe. Spika, ningeomba tuliangalie sana suala hili la michezo na Mabaraza ya Michezo kupelekwa Wilayani.

Mhe. Spika, ukurasa wa 26 kifungu cha 15 “Muda wa Uongozi”. Kukaa kwa mjumbe kwa kipindi cha miaka mitatu. Mhe. Spika, timu zetu nyingi baadhi ya wajumbe wanakuwa wanaziendesha vizuri. Lakini tatizo linalovunja moyo baadhi ya wale viongozi wanaoendesha michezo yao vizuri, basi baada ya muda mfupi tu wanabadilishwa kupelekwa sehemu nyengine kabla ya kufika ule muda uliopangwa, au wanabadilishwa kwa utashi wa mtu tu. Kiongozi yule hata wale wanamichezo wanakuwa wanampenda kulingana na vile anavyowaongoza.
Kwa utaratibu huu wa kuweka kipindi cha miaka mitatu wakati kiongozi mtekelezaji mzuri utakuta tunawavunja moyo wanamichezo inakuwa haiimariki. Ningeomba Mhe. Waziri akaliangalia suala hili, kama kiongozi hakuleta maadili mabovu, hakuleta maharibiko yoyote iwe anaendelea angalau

kwa ukosefu miaka mitano ili kupata kuimarisha ile timu, halafu hapo ufanyike uchaguzi wa kuchaguliwa yeye au kiongozi mwengine.

Mhe. Spika, ukurasa wa 24 kifungu cha 3 “Kuundwa kwa Baraza la Michezo”. Kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Michezo ni muhimu sana. Lakini mimi kitu kinachonitia kigugumizi hapa kidogo katika sentensi hii “Kuanzishwa Baraza la Taifa la Michezo”, la wapi. Kwa kweli hapa kama utaweka Taifa tu hii nahisi kama itakuja kuleta utata baada ya kuwa Mabaraza haya yanaendelea kuja kufanywa ya Muungano.

Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri ni vyema hii sentensi kwa muono wangu irekebishwe na iwe Kuanzishwa Baraza la Taifa la Michezo la Zanzibar. Ikiwekwa hivyo hata wale viongozi watakuwa na nguvu na moyo wa kuhisi wamekuwa na uwezo wa kusimamia Baraza hili wao wenyewe. Lakini kama itakuwa haijarekebishwa hapo wanaweza kuja viongozi wengine ili wakafanya hili la shirikisho kwa wale waliokuwa wameanzisha wakawa hawana nguvu ya kuliendeleza Baraza lile. Ningeomba hapa pakaangaliwa kama pana haja ya kufanyiwa masawazisho basi yakafanywa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 27 kifungu cha 17 “Majukumu ya Katibu Mtendaji”. Katibu Mtendaji atakuwa ndie Mtendaji Mkuu wa Baraza ambaye atahusika na maamuzi mbali mbali katika Baraza la Michezo. Kwa kuwa Mabaraza haya yanategemewa kuwa katika wilaya mbali mbali, kwa hiyo mimi ningependa hapa ufafanuzi wa Katibu Mtendaji huyu akaeleweka kama atakuwepo kwa kila wilaya katika Mabaraza yale ya Michezo au atakuwepo Makao Makuu tu ya Baraza hili la Michezo ili kuja kuondosha mvutano. Katibu Mtendaji wa Wilaya ya Kati akaamua vyake, wa Wilaya ya Kusini akaamua vyake na Katibu Mtendaji Mkuu wa Makao Makuu akaamua vyake, kwa hiyo kukawa kuna mgongano. Sasa ningeomba hapa Mhe. Waziri akija anitolee ufafanuzi ili nikafahamu vya kutosha.

Mhe. Spika, kwa kweli kwa kuanzisha chombo hiki cha Baraza la Michezo kwa hapa Zanzibar kitaleta matumaini mazuri kwa wanamichezo wetu na watakuwa na kipaji kama kilichokuwepo hapo nyuma. Kitu muhimu tu kwa wale viongozi wawe waadilifu na wawe wakweli. Yule aliyekuwa mwanamichezo kweli basi wamthibitishe kweli wasichukulie upendeleo tu kama huyu kwa kuwa maarufu tunamjua hivi wakampa nafasi, wakamuacha yule mwenye fani na sifa ya utekelezaji wa michezo.

Mhe. Spika, kama Baraza hili litakaa kwa kina na kuchunguza zaidi kwa suala la michezo kwa hapa Unguja tuna michezo mingi tu ya kizamani iliyokuwa ikichezwa hapa, lakini kwa ukosefu wa wasimamizi baadhi ya michezo ile mingi imekufa na mingine haikuendelezwa. Lakini kama litaamua Baraza hili

kuichunguza na kuitafuta ipo michezo mbali mbali ambayo ikiimarishwa italeta matumaini mazuri katika nchi yetu.

Kuna michezo ya wasanii ambao wanaigiza michezo mbali mbali na kuleta burudani kwa wananchi. Kulikuwa na resi za baiskeli ambazo mara nyingi zilikuwa zinaleta matumaini, mtu akisikia kuna resi za baiskeli basi siku ile anavunja kazi anakwenda kufuatilia na kusikiliza. Lakini utakuta kipindi hiki muda mrefu hatujawa na usimamizi mzuri kwa hiyo hazina mpangilio mzuri ule wa kupangiwa na kufanyiwa michezo yake.

Kwa sasa hivi kumefufuliwa michezo mbali mbali ya resi za punda, hili kwa kweli limefurahisha sana kwa wananchi wetu, pindipo siku inayoanzishwa tu basi watu wote wanatoka majumbani wanakaa barabarani kwa kuangalia. Kwa hiyo, kuanzishwa Baraza hili litaleta changamoto mpya ya Wazanzibari ili kupata burudani na kupata kutembelea sehemu mbali mbali za michezo hiyo.

Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu mia kwa mia na nawaomba wajumbe wenzangu tuupitishe ili ulete maslahi kwa wananchi wetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru na nichukue muda mfupi kuchangia mswada huu kwa sababu mengi nilikuwanayo wajumbe wenzangu wameyachangia.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia mswada huu naomba nimkumbuke, nimtaje na nimuombee dua mchezaji mmoja wa timu ya vijana ya Mkanyageni ambaye alifariki kiwanjani kwa ajili ya *league* ya mpira wa ya miguu. Mwenyezi Mungu amjaalie kijana huyu amlaze pahala pema peponi. Amin.

Mhe. Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye tafsiri ya maneno. Nianze kwenye tafsiri ya neno michezo ambayo tumeiona hapa, lakini imenipa wasi wasi kwamba tafsiri inasema mchezo utakuwa mchezo pale ambapo sheria na kanuni ya mchezo huo inatambulika. Watumbatu wenzangu wana mchezo wa ngumi ni mchezo mkubwa sana na wana uthamini kuliko michezo mingine ambayo imo kwenye katiba. Sasa sijui michezo kama ile ya ngumi na ngwara kule Micheweni itakuwa ni michezo na tunaweza tukaiundia chama kama. Kama itakuwa ni michezo na tunaweza tukaiundia chama, basi niweze kuwaambia wenzangu wa Tumbatu tufanye vyama hivi.

Mhe. Spika, nikitoka hapa niende kwenye Baraza la Michezo ambalo limetoa ujumbe wake hapa, lakini nimesikitika sana kwamba nadhani mjumbe mmoja tumemsahau, kwa sababu hakuna ufanisi wa michezo kama hatukuwashirikisha waamuzi kwenye mabaraza haya, hata tupange vipi na vilabu vijitahidi vipi ikiwa waamuzi wataachwa pembeni, basi jitihada ya mabaraza haya na vyama

hivi vya michezo basi vitafujika, kwa sababu waamuzi wana sehemu kubwa ya kufuja michezo yetu au kuendeleza.

Mhe. Spika, ningeomba kusema kwamba mjumbe mmoja kutoka chama cha waamuzi Zanzibar, awe ni mjumbe wa Baraza la Michezo Zanzibar ili yale ambayo yatazungumzwa na kupangwa waweze kuyajua, kuliko kuwekwa pembeni halafu ikawa ni uchafuzi wa michezo.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 26 kifungu cha 11, kuna uamuzi kutoathirika kwa athari za utaratibu. Mhe. Spika, kifungu hicho kinasema kwamba uwamuzi wa baraza utakuwa batili iwapo utakwenda kinyume na katiba na sheria ya baraza. Sasa *marginal note* huku inasema kutoathirika, lakini huku kwenye maandishi inasema utakuwa batili. Nadhani kuna ukosefu kidogo wa lugha. Kwa hivyo, wanasheria naomba waangalie ili waweze kutusaidia.

Kwenye kifungu cha 14(b) Mhe. Spika, kinasema kwamba

Kifungu cha 14(b)

> “iwapo atatuhumiwa kufanya kosa la jinai na kuthibitika kufanya kosa hilo”.

Mhe. Spika, yaani mtu huyo hatokuwa mjumbe wa baraza. Sasa ningeomba nijuwe kwamba kosa hilo lina ukubwa gani na adhabu yake itakuwa ni nini. Kwa sababu kwa mfano mtu hatoweza kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi iwapo amehukumiwa kosa la jinai na kufungwa miezi sita zaidi. Sasa ikiwa Mjumbe wa Baraza kosa lake la jinai limethibitika ni kiwango gani ukubwa gani adhabu yake.

Mhe. Spika, kwa sababu matusi ni kosa la jinai. Kwa hivyo, mtu anaweza akawa katukana huko lakini bila kuadhibiwa tusijuwe kwamba kapewa adhabu gani na bado akaendelea kuwa Mjumbe wa Baraza. Sasa Mhe. Spika, ningeomba tukajua ni kiwango gani cha adhabu hii ya kosa la jinai kile ambacho kinaweza kumtoa Mjumbe huyo wa Baraza.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeomba nipate ufafanuzi ni uteuzi wa Katibu Mtendaji. Hapa tumeambiwa sifa ya kwanza ni kwamba awe ba Stashahada kutoka chuo kinachotambulikana. Mhe. Spika, Stashahada hii nataka nijuwe iwe ni ya fani ya michezo au pengine uwongozi na kadhalika. Kwa sababu wasi wasi wangu ni kwamba unaweza ukamuweka katibu mtendaji lakini akawa hana sifa ya shughuli za michezo na mambo yakaenda upande. Kwa hivyo, nataka nijuwe Stashahada hii ni ya fani gani ya michezo au fani nyengine ambayo mswada huu umetaja.

Kwa mfano sifa za Mrajis wa Michezo imewekwa wazi hapa kwamba lazima awe na elimu ya kuanzia Stashahada ya Kwanza katika fani ya sheria, hii imetajwa lakini kwa Katibu Mtendaji haikutajwa. Kwa hivyo ningeomba nijuwe ni sifa ya Stashahada fani gani.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 19 kwenye mamlaka na majukumu ya mrajis ukiangalia kwenye kifungu cha 19(d)(i) hadi (v) nadhani kazi zake zimefanana, kwa hivyo nafikiri ingekuwa ni kifungu kimoja kuliko kuwa vifungu viwili. Kwa sababu kifungu cha (i) kinasema;

Kifungu cha 19(d)(i)

"Iwapo kwa makusudi kinakwenda kinyume na katiba au kanuni zake";

Kifungu cha 19(d)(v)

"Iwapo uongozi wake umepatikana kwa namna nyengine kinyume na ilivyoelezwa katika katiba au kanuni zake";

Mhe. Spika, zote hizi ni maana moja, kwa hivyo ningeomba iwe ni kifungu kimoja badala ya viwili.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa kuchangia ni katika kifungu cha 27(c) kinachozungumzia wajibu na majukumu ya mkutano wa wadau wa michezo ni;

Kifungu cha 27(c)

"kupokea na kujadili utekelezaji wa ripoti za mabaraza ya michezo ya Wilaya na vyama vya michezo vya taifa".

Mhe. Spika, mimi naona hapa kidogo maandishi yamekwenda kombo, iwe ni ripoti ya utekelezaji. Kwa sababu utekelezaji wa ripoti nadhani ni kinyume. Lakini iwe ni ripoti ya utekelezaji.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka nisisitize ni kifungu cha 35 kuhusu hesabu na ukaguzi. Tumeambiwa kwenye mswada huu baraza litaweka hesabu zake na kutoa ripoti yake kwa Mhe. Waziri na kifungu cha 2 kinasema kwamba hesabu hizo za baraza zitakaguliwa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali. Hii ina maana kwamba ikiwa CAG atazikagua maana yake na PAC itafika. Kwa hivyo, hatuwezi kumuachia majukumu katibu mtendaji atoe ripoti bila ya kuwa na mkaguzi wa ndani wa mahesabu.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, ningesisitiza kwamba lazima tuwe na *internal control* ya baraza kwa ajili ya kumbukumbu sahihi, vyenginevyo tukimwachia katiba na baraza lake bila ya kuweka wataalamu wa fedha, maana yake kila

siku *query* za baraza zitakua zipo na itakuwa baraza linaendelea katika uchafuzi wa mahesabu ya serikali.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba naunga mkono hoja na marekebisho Mhe. Waziri ayazingatie. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza kabisa naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwepo hapa, mimi naomba kutoa mchango wangu na baadhi ya maelezo ambayo wajumbe wengi wamechangia juu ya mswada huu ambao tumeambiwa umekuja wakati muafaka. Kama miswada mingi mingi ambayo imekuja hapa nayo imekuja kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, kwanza kabisa katika mchango wangu nitagusia hiki kipengele cha siasa ambacho kimetajwa na vipi tumekifahamu sisi au tulivyokitafsiri. Mhe. Spika, kule kwenye jimbo langu la Mpendae tuna timu ya mpira, ambayo inaitwa Mpendae United. Timu hii tumeiunda kwa kutumia chama cha siasa CCM, ni timu yetu ya CCM. Kuna siku moja nilikwenda pale nikakuta vijana wanapigana, kuna ugomvi. Kuna kijana mmoja kamwita mwenzake bunju miba au vyovyote vile, lakini kamwita bunju na ndio ugomvi ukawepo hapo. Sasa sisi tulijaribu kuwaamua ule ugomvi.

Kwa hivyo, ninachotaka ni kwamba katika ile timu mchezaji anaweza kuchaza mchezaji yeyote na ndio ilivyokusudiwa hapa, kwamba isiingizwe ile siasa kwa kuwabagua wale wachezaji wenyewe. Kwa mfano aah! Wewe usicheze katika timu hii. Kwa hivyo, katika timu ya Mpendae United ni timu ya CCM, lakini tuna wachezaji wa CCM, wako vijana kutoka CUF tunawajua ambao wanakaa maeneo yale ya Bitiamrani wanacheza katika timu hiyo hiyo na wazee wao wengine ni viongozi kabisa. Lakini wanapocheza mpira pale tunakuwa tumeshughulika na jambo moja tu. Tunaposhangiria, inakuwa tunashangiria bendera yetu hivyo hivyo, bendera ya timu pamoja na ya siasa. Lakini katika kucheza sote tunacheza pamoja. Siasa inayokatazwa hapa ni ile kuibagua timu, haya yameshatokezea mara nyingi.

Mhe. Spika, kuna kesi moja iliwahi kutokezea hapa kwa kupitia BAZA na UBA. BAZA ni chama cha *basket ball* cha Zanzibar na UBA ni chama cha *basket ball* cha Wilaya ya Mjini, kesi yao ilikwenda mpaka mahakamani na wakili alikuwa ni ndugu Mbwezeleni, ambaye alikuwa anashughulikia kesi hiyo. Timu moja ambayo ilikuwa imebaguliwa Wilaya ya Mjini ilikuwa ni *Stone Town* wakati huo, ambao walikuwa wamechukua ushindi, lakini wakanyimwa ule ushindi kutokana na kwamba wamepewa jina tu la CUF, lakini muna vijana wazuri sana katika timu ya *Stone Town* wa CCM ndani yake na mimi nawafahamu wengi wao. Kwa hivyo, siasa iliyozungumziwa hapa ni

kuibagua mantiki ya mchezo na timu yenyewe kutokana na ile siasa. Nadhani hilo limeeleweka.

Mhe. Spika, mchango wangu katika ukurasa wa 26 uteuzi huu wa katibu mtendaji. Wajumbe wengi wameligusia hili. Katika marekebisho yake kifungu cha 16(2)(a) kinasema;

Kifungu cha 16(2)(a)

"Awe na angalau Stashahada kutoka chuo kinachotambulika".

Neno 'angalau' limeongezeka pale, ambapo mwenyekiti wa kamati ya ustawi wa jamii alitoa katika marekebisho. Angalau Stashahada kutoka chuo kinachotambulika. Sasa katika michezo Stashahada hapa imetajwa sio lazima uwe na Stashahada ya michezo. Wale wapenzi wa timu hii maarufu ya *Arsenal* watakuwa wanamjua kocha wao Arson Wenga, hana shahada ya michezo ila ana shahada ya uchumi, digrii yake ni ya uchumi na leo ameiongoza ile timu kwa miaka kadhaa, inafanya vizuri na imezalisha mamilioni, mamia ya mamilioni ya *pound* kule Uingereza. Kwa hivyo, hapa Stashahada inayotakiwa awe na kiwango hicho cha elimu, lakini sio lazima katika fani ya michezo, ndio maana hilo halikuwekwa hapa.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alichangia pia kuhusu chama cha waamuzi. Chama cha waamuzi katika michezo yote hakiko peke yake, yaani hakijitegemei kwamba hiki ni chama cha waamuzi. Chama cha waamuzi mara nyingi kinakuwa katika chama cha ule mchezo husika.

Kwa mfano, chama cha waamuzi wa mpira wa miguu kiko pamoja na chama kikuu chake ZFA chini ya chama hicho. Chama cha waamuzi wa mpira wa basket ball kiko chini ya BAZA. Kwa hivyo, chama cha waamuzi maisha hakikai peke yake kwamba kijitegemee, lakini ninachotaka kueleza kwamba hapa katika hizi nafasi, kwenye ukurasa wa 24 kifungu cha 4(h) kinasema;

Kifungu 4(h)

> "Kutakuwa na wawakilishi wanne kutoka chama cha taifa cha michezo ambao watachaguliwa na mkutano wa wadau wa michezo miongoni mwao wawili wawe wanawake".

Mhe. Spika, mimi huwa napenda mara nyingi kuwaita wahusika wakuu hawa. Kwa hivyo, wale wote waliochangia neno hili na mimi binafsi napenda kutumia neno wahusika wakuu, kwa sababu neno hili mara nyingi huwa tunalipiga vita. Hata Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo neno hili huwa halipendi kulitumia, hata kwenye kamati tulizungumzia neno hili. Kwa hivyo, wahusika

na nina amini kuna wataalamu wa lugha ambao sheria hii ikishatoka, basi naamini na wao watatumia busara zao za kuweka sawa hili.

Mhe. Spika, katika mkutano huu chama cha waamuzi kinaweza kuingia moja kwa moja. Kuna Mhe. Mjumbe mmoja alichangia akasema kwamba mbona hakuna mwakilishi yeyote kutoka Pemba. Hapa pia hajatajwa mwakilishi yeyote kutoka Unguja. Kwa hivyo, kwa nafasi hizi, mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mhe. Rais anaweza akatokea Pemba anaweza akatokea Unguja, mkurugenzi wa michezo, katibu mtendaji, mrajis wa vyama, mjumbe mmoja atakayeteuliwa na waziri, anaweza waziri akatumia busara zake akamteua mjumbe huyo kutoka Pemba, mwakilishi wa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kadhalika.

Kwenye vyama vya michezo wenyewe, sio baraza. Vyama vya michezo kwa sababu wana ngazi za wilaya ambazo zina sehemu zinazotokea. Kwa mfano Pemba, katika katiba ya ZFA ukiangalia kuna mwenyekiti ambaye anaweza kutokea upande wowote, lakini kuna makamu wenyeviti wawili, mmoja lazima atokee hapa Unguja na makamu wa pili wa mwenyekiti wa ZFA lazima atokee Pemba. Hiyo ni katiba yao ambayo imepanga hivyo na vyama vingi vya michezo katiba zake ziko kwa mantiki hiyo.

Mhe. Spika, katika michezo mara nyingi huwa tunazungumzia masuala mbali mbali ya maendeleo. Mimi naomba nimshukuru sana mtu ambaye amekuwa akinishauri mara nyingi na kuniongoza na kunipa maoni yake, ambaye naweza kusema kwa hapa Zanzibar ana *qualification* za aina tatu peke yake, nitamtaja. Yeye ana *qualification* ya *sports management* yaani uongozi katika michezo, ana *qualification* ya *stadium management* ya kuendeleza vile viwanja vya michezo pamoja na *qualification* ya *sports development* yaani kuendeleza michezo. *Management, development na stadium management.* Naye ni Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis, katika *qualification* hizo naweza kusema amefika mbali sana. Kwa sababu alifika mpaka kule makao makuu ya FA Uingereza na kuifanya Zanzibar iwe mjumbe.

Mhe. Spika, mantiki ya kuongea haya ni nini? Inategemea kile chombo chenyewe baraza kitakuwa kiasi gani yaani wepesi wake, vipi kitakuwa. Kwa mfano yule mwenyekiti uwezo wake, mrajis uwezo wake na kadhalika. Ni vipi wao wataweza kukifikisha kile chombo nje ya Zanzibar.

Mhe. Waziri Kivuli aliongelea juu ya kwamba hili baraza litakuwa kwa hapa au litakwenda nje zaidi ya Zanzibar. Matatizo mengi tumeyaona, matatizo ya FIFA tumeyaona ambayo TFF na ZFA zilikuwa hazipati haki sawa na tumewatetea ZFA kiasi tulichoweza na hivi sasa matatizo hayo yametatuka. Kuna matatizo ya CHANETA na CHANEZA. Mara nyingi matatizo haya huja

kwa michezo ya nje ya Zanzibar, ambapo ushiriki kwa bendera moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mara nyingi mialiko hiyo inapokuja basi huja kwenye afisi moja nayo huishia pale Dar es Salaam kwa wenzetu. Sasa inategemea mahusiano mmejenga vipi.

Kwa mfano Baraza hili la Wawakilishi sasa hivi lipo mstari wa mbele sana katika masuala ya CPA. Siku moja nilikuwa nasoma hili gazeti la CPA, nikaona Mhe. Abass Juma Muhunzi ameandika *article* nzuri sana katika gazeti lile. Hii inategemea vipi sisi wenyewe tutakavyokuwa mstari wa mbele katika masuala haya.

Kwa hivyo, ninachotaka kueleza hapa ni kwamba baraza la taifa la michezo hapa Zanzibar, itategemea pia na uongozi wake vipi utachukua kwenda nje. Lakini lina ruksa na lina majukumu ya kwenda nje ya Zanzibar bila ya wasi wasi wowote, kwa sababu katika michezo hatuko katika Muungano, kila mmoja anajitegemea. Ndio maana mpaka leo tunaendelea kugombania haki yetu kutoka FIFA kupitia kwa ZFA.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali alichangia mambo mengi sana, ninaweza kusema katika mtu mwengine ambaye tunatakiwa tumwite mwanamichezo maarufu ni yeye mmoja wapo. Kwa sababu yeye kwenye michezo hakosi na yote aliyoyachangia leo nadhani ametugusa karibu kila sehemu.

Pia alizungumzia kuhusu michezo kiuchumi, wawekezaji waje kwenye masuala ya michezo. Napenda kumjulisha kuwa sasa hivi wafanyabiashara wengi wameshaanza kujiingiza kwenye michezo, wameshaanza kujiingiza kwenye kufadhili timu. Mifano michache ni *Ocean View* timu ya Malindi bado ina wafanyabiashara na wao wanajiingiza zaidi.

Vile vile alizungumzia kuhusu masuala ya utaalamu pamoja na mchezo huu wa *boxing*. Wakati mimi naomba ushauri kutoka kwa wazee walionipita kwa umri, juu ya mchezo huu wa *boxing* na tafsiri iliyotolewa hapa ya michezo nikaulizwa na mzee mmoja wakati namuuliza kwamba, kwa nini huu mchezo wa *boxing* sasa hivi tusicheze?. Aliniuliza swali moja yule mzee. Je, utamruhusu mwanao aende akacheze *boxing* wewe? Aliniuliza swali hilo na kwa kweli likawa zito, kweli simruhusu mwanangu kwenda kucheza *boxing*, kwa sababu najua hatari zake. Tunamuona Mohamed Ali, *clashers scley* walikuwa wakimwita wakati huo jinsi alivyo leo, maisha yake yanavyokwenda, mambo aliyopoteza, fedha zote anazo duniani lakini afya hana.

Kwa hivyo, kwa kweli mimi naomba kuungana na kauli ya Rais wa kwanza wa Zanzibar marehemu Mzee Abeid Aman Karume aliyoitoa kupiga marufuku mchezo huu. Kwa hivyo, tafsiri ya neno michezo litabaki pale pale, lakini

mchezo huu wa *boxing* bado hatujawa tayari, pamoja na michezo mingine yote inayohusiana na *boxing. Kickboxing, fly boxing* na mingineyo. Kwa hivyo, hii yote bado Zanzibar haijawa tayari, ingawa vijana wanacheza, lakini wanacheza katika mazingira yaliyokuwepo nje ya Zanzibar, wanapata zawadi nje ya Zanzibar lakini sisi hapa hatujaruhusu. Kwa hivyo, tutashindwa hata kwenda kuwapokea wakirudi na medali zitakuwa ni medali za kwao, kwa sababu bado hiyo michezo haijakubalika hapa Zanzibar.

Kulinda viwanja vya michezo kama sheria inavyotamka. Suala hili inabidi litiliwe mkazo. Mara nyingi Baraza la Michezo hili lililopita lilikuwa ni kama mahakama, halikuwa na nafasi kabisa ya kuendeleza ile michezo yenyewe. Ilikuwa baada ya *league* zinakuja kesi Baraza la Michezo na zinakuja rufaa kisha mzunguko unakuwa ndio huo huo kila siku, kwa hivyo ikawa haiwezi kuendeleza ile michezo yenyewe. Lakini sasa hivi kwa sheria hii mpya basi kazi hizo nazo zitakuwa zimepunguzwa ili Baraza la Michezo liweze kupanga mipango ya maendeleo ambayo yataweza kufanywa kila muda unapofika.

Mhe. Spika, kuna kifungu hiki cha baraza kuweza kushtakiwa na kushtaki. Hiyo ni haki ya kikatiba ya mtu au chama cha michezo. Naamini mwisho kabisa wanapokuwa hawajaweza kufikia muafaka basi haki hiyo inaweza ikatumika na ndio maana kifungu hicho kikawepo kwamba baraza lina uwezo wa kushtaki au kushtakiwa.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu kudhibiti taarifa za wajumbe. Mimi nakubaliana na mheshimiwa kwamba atahifadhi iwe ndio neno zuri zaidi, yaani kama siri. Sasa hili wataalamu wa lugha nao wanaweza kutusaidia, lakini ni kuhifadhi. Kwa sababu katika baraza mara nyingi timu zetu hizi za majimboni wakati zinapokuwa na kesi, basi hata mwakilishi huwa anaingilia, sasa unapoingilia unataka kujua mule ndani ya baraza nani aliyesimama na kazungumza nini. Sasa ili ile siri ihifadhike mtu anaweza kukuambia aah! Mimi nimekutetea bwana nimekusaidia, lakini kumbe hajazungumza hivyo, ili siri ile ihifadhike basi hilo nalo tunataka lihifadhike kupitia sheria hii.

Vile vile Mhe. Spika, liligusiwa suala la vileo au pombe au vilevi au jina lolote jengine kama kuwa wafadhili. Suala hili sio hapa tu hata nchini Ufaransa ambapo vitu hivyo navyo hutumika sana kuliko hapa, wao wamepiga marufuku kutangaza kwa kutumia ulevi ama sigara, wao wamepiga marufuku kabisa katika michezo yao yote hawatangazi. Hii ni kutokana na mila na silka ya Zanzibar basi na sisi bado.

Mhe. Spika, liliwahi kuulizwa swali moja hapa kwamba kwa nini Mafunzo walifungwa sita bila walipokwenda kuvaa jezi ya kileo na nilijibu sababu zake. Juzi tu hapa Mhe. Spika, umesoma taarifa ambayo wajumbe iliwasikitisha

kidogo walipoambiwa wamevaa jezi za aina hiyo. Kwa hivyo, hilo bado tunaendelea nalo.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman aligusia juu ya kasoro nyengine zilizokuweko, kama kero za TFF, ZFA, CHANETA, CHANEZA nimezielezea na sio kero hizo tu kuna na kwenye masuala ya riadha nayo tumeyaelezea. Akatoa mfano wa mchezo wa kuogelea. Hilo naomba nimthibitishie kwamba sasa hivi nalo tunalishughulikia, na hivi karibuni tu tunatarajia mambo yatakuwa mazuri. Michezo katika elimu kama sera ya elimu inavyosema imo nayo ni sisi na wao tunaendelea kushirikiana zaidi ili tuweze kwenda mbele.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, mimi naomba kuunga mkono pamoja na hoja zote zilizotolewa ambazo tumejitahidi kuweka sawa na naamini wataalamu wa lugha nao watatusaidia kuweka sawa kwa yote. Baada ya hayo yote Mhe. Spika, naomba kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kuendelea kutupa uhai na uzima na tukadiriki hapa tulipo na kusikiliza michango mbali mbali ya wajumbe.

Mhe. Spika, na wewe nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho. Sitofanya majumuisho ya jumla kwa kuokoa wakati, nitafanya majumuisho ya waheshimiwa 10 waliochangia, naomba niwataje;

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	Mwenyekiti
2.	Mhe. Najma Khalfan Juma	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Juma Duni Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	Mjumbe
5.	Mhe. Haji Faki Shaali	Mjumbe
6.	Mhe. Moh'd Ali Salim	Mjumbe
7.	Mhe. Zakiya Omar Juma	Mjumbe
8.	Mhe. Ali Denge Makame	Mjumbe
9.	Mhe. Hija Hassan Hija	Mjumbe
10.	Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Mjumbe

Mhe. Spika, nawashukuru wote waliochangia wengine wametushauri, wengine wametusaidia kutoa ufafanuzi wa hapa na pale, wengine wametuelekeza. Kwa jumla michango ilikuwa mizuri *constructive*, hatuna sababu kwa nini tusithamini na tusiipokee na pale palipotolewa ushauri tuondoshe hiki na tuweke hiki, nataka niahidi kwamba tutapaangalia na wakati wa kuandika mswada wa mwisho tutashirikiana na Mwanasheria Mkuu kuweka yale ambayo

nyinyi mmeshauri. Kwa bahati nzuri katibu wetu yuko hapa kwanye Baraza kwa hivyo kasikia yale ambayo yaliyoshauriwa tutayazingatia.

Mhe. Spika, nianze na Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana umetupongeza, umetoa ufafanuzi kwa mambo mbali mbali, umejitahidi sana kutoa ufafanuzi ule ambao marekebisho tuliyazungumza kwenye kamati, umetusaidia sana. Mwisho ukatoa nasaha na kutoa wito kwa vyama vyetu vya michezo vishirikiane na Baraza la Michezo la Taifa.

Mhe. Waziri Kivuli wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Najma Khalfan Juma, kwanza umetupongeza na halafu ukaendelea kutuelekeza hapa na pale. Maeneo mengine nakubaliana na wewe na maeneo mengine naomba kutoa ufafanuzi kidogo.

Kwa mfano, uliuliza kuna haja ya Mhe. Mwenyekiti ateuliwe na Rais. Lakini kwenye ukurasa wa pili umetupatia jibu katika hii hoja yako na ukasema huyu anayeteuliwa na Rais anapata hisia kwamba kateuliwa na Rais, anakua zaidi mwangalifu na kadhalika. Nakubaliana na mawazo hayo, lakini zaidi nasema *tradition* inatuelekeza hivyo kwamba takriban wenyeviti wote wa Mabaraza mazito kama haya, maana Baraza la Michezo tusidhani kwamba kazi yake ni kucheza tu. Isipokuwa Baraza la Michezo lina uzito maalum wa kuendeleza michezo kama ilivyoelezwa kwenye kazi zake.
Kwa hivyo, nadhani tukubaliane kwamba mwenyekiti kuchaguliwa na Rais ni bora, maana huyu atakuwa muadilifu akikumbuka kwamba pale amepata *confidence* ya Rais kumchagua kwa ajili ya kufanya ile kazi.

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia kwenye kifungu cha 3(b) kuhusiana na masuala ya haki, sheria na kadhalika. Kwa hivyo, nataka niuthibitishie ukumbi huu, kwamba lengo la kuandikwa upya sheria hii ni kuondosha zote zilizokuwepo hapo mwanzo.

Kwa hiyo, nashukuru wengi waliochangia wameelekeza michango pamoja na ushauri wao huko. Kwa maana hiyo, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba asiwe na wasi wasi Baraza hili litakuwa adilifu vya kutosha.

Mhe. Spika, pia aligusia suala la vyama visiende Mahakamani ni kuzuia uhuru wa wanamichezo na kadhalika. Nataka nilieleze Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba uamuzi wa michezo kutokwenda Mahakamani ni uamuzi wa *FIFA*. Kwa hivyo, *FIFA* inasema matatizo yote ya michezo yaelekezwe kwenye Mabaraza ya Michezo pamoja na Vyombo vya Michezo vya Rufaa.

Lakini bado wapo watu wamekwenda Mahakamani, kwa ajili ya matatizo ya michezo. Kwa kweli Baraza la Michezo halikuzuia ingawa sheria yake inakataza, huo ni uhuru wa mtu mwenyewe.

Mhe. Spika, kwa mfano Waislamu wameshauriwa kwenye matatizo yao ya ndoa waende kwa Kadhi. Lakini tunao ushahidi Waislamu wengine wanapenda kwenda Mahakamani, ambapo Sheria za Kadhi hazina nguvu sana na pengine anaweza kwenda mpaka Mahakama ya Rufaa. Kwa hivyo, akiamua kufanya hivyo kwamba ndoa yake ichezewe na Mahakama hizo za kawaida sawa, lakini akiamua ndoa yake izingatiwe na Maulamaa katika nafasi ya Kadhi pia ni sawa.

Uadilifu tunasema kwamba watu wasiende Mahakamani, watakapokwenda Mahakamani basi wanakwenda kwa hiari yao na kama sheria zetu zinamgusa zitaendelea kumgusa.

Nikiendelea pia Mhe. Mjumbe ametushauri kwamba suala la Wazanzibari lizingatiwe sana katika shughuli zetu za michezo na hilo limethibitika hivi karibuni. Wakati timu zetu za riadha, *football*, *netball* na huo ni ushahidi kamili kwa wale waliozungumza kwamba Baraza linashughulikia *football* peke yake na hiyo si sahihi.

Kwa kweli tunashughulikia michezo mingi na mingine imeanza kupamba moto na kushinda mashindano mbali mbali. Kwa hivyo, suala la Uzanzibari tunalizingatia katika kila eneo ambalo lazima kumtaja na kumjumuisha Mzanzibari.

Lakini katika maeneo mengine Mtanzania anayo nafasi kushiriki basi atashirikishwa. Kwa mfano, tunazo timu ambazo zimeajiri wachezaji kutoka Ulaya, Tanzania Bara na hawa wanashirikishwa na wakifika hapa wanafuata Sheria zetu za Michezo za Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiendelea na hoja za Waheshimiwa Wajumbe, sasa niende kwa Mhe. Ali Abdalla Ali kama alivyomwita Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwamba huyu ni mtaalamu mzuri sana wa michezo tena anafuatilia sana michezo na michezo yake mara nyingi inakuwa *very constructive (Makofi)*.

Nataka nimthibitishie kwamba yale ambayo ametushauri tutayazingatia. Vile vile alitaka ufafanuzi kuhusu suala la wadau maana yake nini. Kwa kweli suala hili bado linaweza kuulizwa, kujadiliwa na kadhalika. Isipokuwa tumeliweka kwa sababu ni neno ambalo linatumika tena linafahamika sana na karibu sasa ni

universal, yaani ni neno linalokubalika kila pahala ambapo Lugha ya Kiswahili inazungumzwa.

Kwa hivyo, tumeupokea ushauri na tutatafuta ushauri mwengine kama ni kuridhiana. Lakini ninachosema kwamba Lugha ya Kiswahili inakua na kubadilika, tunao Wajumbe katika Baraza la Kiswahili la Tanzania, ambao wanahudhuria mikutano na kudadisi pamoja na kuuliza maneno na wanapoyathibitisha basi tunayo haki ya kuyatumia.

Nadhani tujiulize tunafanya Mtihani wa Taifa wa Kiswahili, mtihani ambao hatutungi sisi, tukikataa kulitambua neno wadau, limekuja kwenye mtihani wadau maana yake nini na tunatakiwa tujibu, ili tupasi. Kwa hivyo, ndio maana nimesema suala hili ni *debatable* bado tunayo nafasi ya kukubaliana na kulichambua *(Makofi)*.

Kwa maana hiyo, turudi kwa wataalamu wetu wa Kiswahili akina Mhe. Mohammed Ali Salim, Mhe. Zakiya Omar Juma, Bi Khadija Juma watupe ufafanuzi na wakisema linafaa kutumika, basi tusione tabu kulitumia kwa sababu ndio kuendeleza Kiswahili chenyewe. Lakini kujifungia katika chumba cha kuta nne na kusema hili ndio sahihi na yaliyobakia yote si sahihi basi hatukiendelezi Kiswahili.

Kazi za Baraza zimezungumzwa sana na wachangiaji wengi. Kwa hivyo, nakubali waliyoyakubali na ninakubali waliyoyapendekeza tutayafanyia kazi.

Mhe. Mjumbe amezungumza karibu *points* 18 kwenye michango yake na kama nilivyosema mwanzo kulinda wakati. Kwa hiyo, namshukuru na kumpongeza na tumezichukua *points* zake na tutazifanyia kazi, pale ambapo tutalazimika kubadilisha basi tutabadilisha.

Vile vile alitaka ufafanuzi wa riba katika vianzio vya mapato tumetaja riba. Kwa kweli riba labda Baraza limeweka akiba pengine Benki ya Watu wa Zanzibar ni moja katika benki ambazo zinatoa riba, mwisho wa kipindi imepata riba ya asilimia sita au saba, basi ile ni haki ya Baraza ni chanzo cha mapato ya Baraza. Ndio maana tumetaja miongoni mwa vyanzo vya mapato riba tumeitaja na wala hatukuwa na haja ya kuificha.

Kutokana na hali hiyo, mkitushauri mapato ya Baraza yawekwe kwenye Benki za Kiislamu ambazo hazina riba basi tutafanya hivyo. Lakini hapa tunazungumzia benki za kawaida ambazo zote zinatoa riba.

Pia Mhe. Mjumbe ametushauri Baraza liweke kifungu maalum cha kusaidia timu zinazotoka kwenye mikoa ambazo hali yao ya kiuchumi ni dhaifu. Wakati

sasa tunaenza Baraza mpaka katika wilaya basi kuna haja ya kuangalia uwezekano kuweka vifungu maalum kwa timu za mkoa zinazoshiriki kitaifa.

Nafikiri hivyo, ndivyo alivyokusudia ndio maana ameitaja Timu ya Mundu. Kwa hivyo, tutalizingatia suala hilo kwa sababu ni kweli Mundu walilazimika kwenda Zimbabwe nadhani kwa usafiri wa basi na walipofika Zimbabwe miguu imevimba na siku ya pili mashindano na walifungwa magoli mengi sana, lakini Timu ya Mundu si mbaya sana kiasi hicho.

Natumai michango ya Mhe. Mjumbe nimeikalimisha pamoja na majibu mengine yaliyotoka kwa Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wakati alipokuwa akifanya majumuisho.

Mhe. Juma Duni Haji yeye amelizungumzia sana suala ambalo wachangiaji wengi wamelizungumza la kushirikisha michezo kwenye siasa. Namshukuru Mhe. Naibu Waziri amelitolea ufafanuzi mzuri sana na nafikiri tumefahamu tulivyokusudia.

Sasa kama kuna haja ya kukisoma tena kifungu hiki kwa maana ya yale yaliyokusudiwa yajulikane kwa haraka kuliko kukiacha hivi kilivyo, basi tutaifanya kazi hiyo. Lakini nafikiri alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri basi asingetokea mwengine kulizungumza vizuri zaidi kuliko alivyolizungumza kwa hiyo sina haja ya kuliongezea.

Vile vile Mhe. Mjumbe amezungumzia suala la wadau ambalo tayari nimeshalitolea ufafanuzi. Isipokuwa naendelea kusema kwamba bado ni *debatable* turudi kwa wataalamu wa Kiswahili na wao ndio walioturuhusu tulitumie, maana tulikuwa tumeshalitoa, lakini wameturuhusu na kutuambia hilo ni *universal.* Lakini tutarudi kwa ajili ya kukidhi haja kama itakuwa ni lazima *(Makofi).*

Mhe. Spika, pia aliuliza Katibu Mtendaji huyu ni yupi, yaani wa Baraza Kuu au Mabaraza ya Wilaya. Katibu Mtendaji tunayemzungumza hapa ni wa Baraza Kuu.

Nikiendelea na majumuisho ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe, sasa niende kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, alitoa pongezi na pia aliuliza swali la *Kickboxing* na sijui kama tukimuweka uwanjani anaweza ku-*box* na ku-*kick*, lakini hili nalo Mhe. Naibu Waziri amelitolea ufafanuzi mzuri na wala sina haja ya kulirejea.

Pia Mhe. Mjumbe alitaka Baraza lisaidie kuwatafutia wafadhili vyama vya michezo. Kwa kweli nakubali kwamba ni kazi ya Baraza la Taifa la Michezo,

lakini tukubali kwamba kazi hiyo itakuwa ni kubwa, kwa sababu vyama vya michezo ni vingi sana. Baraza likiachiwa ndio libebe hilo jukumu nadhani tutalitwika mzigo na Baraza litakuwa halina kazi nyengine za kufanya za kuendeleza michezo, badala yake litakuwa linafanyakazi ya kutafuta wafadhili ingawa wafadhili nao ni sehemu ya kuendeleza michezo.

Lakini nataka nitoe indhari kutafuta wafadhili na mfadhili ni kitu kimoja kumpata mfadhili ambaye atakubali kuchangia ni kitu cha pili. Isipokuwa jambo la msingi ukeshafadhiliwa kile ulichofadhiliwa unakitumia vipi kwa manufaa ya timu au wako mwenyewe.

Kwa bahati mbaya sana timu, zetu nyengine zilikuwa zimepata ufadhili, wafadhili wamejitoa baada ya biashara zao kuharibika. Lakini vilabu au taasisi nyengine zimepata ufadhili na tukapata moyo sana kwamba sasa taasisi zinaitikia ule wito wetu wa kutegemea ufadhili wa pombe na wanakwenda kwenye ule ambao sahihi tunaoukubali na muda si mrefu mfadhili amejitoa. Sababu amebebeshwa mzigo ambao si kiasi chake.

Kwa hivyo, hilo nalo tuliangalie, yaani hili suala la kufadhiliwa ni pande zote mbili, yaani mwenyekufadhili na kufadhiliwa. Kwa maana hiyo, ushauri wako au Baraza ama Wizara kwa jumla ni kwamba watu wajenge imani kwa wanaowafadhili tena wawe waadilifu sana kwa kile walichofadhiliwa, tuukifanya hivyo, ufadhili utakuwepo tena utadumu.

Kwa bahati nzuri tunawaona sasa wafanyabiashara wazuri aghalabu hawa wa simu hivi sasa wako mbioni wanashindana katika kutufadhili, basi na sisi tunatakiwa tuwe *very careful* katika kuupokea kufadhili na kuutunza na matumizi yake yawe ya wazi sana. Nadhani tukifanya hivyo tutafaidika na tutafadhiliwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman naye ametupa hadith ya As-hab-llkahafy, yaani wamekaa miaka 300 na walipotoka nje wameona kama wamekaa juzi na jana na kisa hiki ni kikubwa. Lakini Mhe. Mjumbe kwa kutupa vionjo ndio kawaida yake.

Katika michango yake anaonekana kwamba hayuko makini katika kufuatilia shughuli zetu za michezo na bado amejifungia kwenye bango lake liliopo pale Ziwani. Kwa mfano, anasema mchezo wa kuogelea haupo, taasisi cha Mchezo wa Kuogelea haipo, vile vile tunalazimika kukuza michezo mingi.

Kweli michezo mingi sana ambayo ilikuwa tayari imeshakufa basi tumeifufua ukiwemo huo wa kuogelea. Mhe. Naibu Waziri ametaja resi za punda watu walicheka, lakini siku punda walipofanya resi zao kutoka Amani mpaka Mao-

Tse-Tung watu walijazana sehemu zote mbili za *stree* kwa ajili ya kushangiria punda wanavyoshinda. Kwa hivyo, kutokana na watu wengi kuupenda huo mchezo, basi tunaukuza na tunauendeleza *(Makofi)*.

Vile vile baskeli zipo. Leo *coincidentally* tunajadili habari hizi za kukuza michezo wakati wiki moja iliyopita tuliwaita wanamichezo wa *Golf* na tuliwaambia wakatafute eneo na serikali italiendeleza kwa ajili ya kurejesha mchezo wa *Golf* hapa Zanzibar.

Kwa nini tukafanya hivyo, kwa sababu ya moja yale aliyozungumza Mhe. Juma Duni Haji, aliposema wale wazee sasa waliokwisha kufanya vitumbo, kwa vile Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini na alitaja na mwengine nimemsahau. Kwa hivyo, hawa ndio watengenezewe taratibu za kwenda kushiriki na kwenda kunyoosha mikono na miguu kwenye viwanja vya *Golf*.

Mchezo huu wa *Golf* unachezwa Zanzibar kwa bahati nzuri jinsi unavyopenda haukufa hata kama pakuchezea hatuna, lakini watu wanacheza mchezo huu. Isipokuwa tumeshtuka tulipomuona kijana mmoja ametokea wa mwanzo Tanzania kwa mashindano ya Golf na kupata kikombe.

Tulipowaita vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* kwa Rais basi na huyu jamaa tulimwita na kuja na kupeana mikono na Mhe. Rais na kumwambia mimi ndiye bingwa wa *Golf* katika nchi hii ya Tanzania, alimuuliza unacheza wapi *Golf*, alimwambia hapo Maisara kuna vishimo vitatu ndio tunacheza *Golf*. Kwa sababu *Golf* sheria zake ni vishimo 18 na huyu anacheza *Golf* kwenye vishimo vitatu na kutokea bingwa wa Tanzania. Kwa hivyo, tukasema wakati sasa umefika tufufue *(Makofi)*.

Kutokana na hali hiyo tumewashauri waunde kamati yao vizuri. Mhe. Spika, leo wamekwenda kuangalia hilo eneo ambalo tumewapa na wamesema linafaa. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwenye bajeti michezo ijayo mtuunge mkono, kwa bajeti ya milioni 100 hata mkituambia tufanye nini tutashindwa. Lakini mkituongezea kidogo basi tutaipeleka kwenye *Golf* na *Indoor Stadium* kwa kile mtakachotuongezea na itakuwa mambo mawili hayo tumeyafanya vizuri.

Mhe. Spika, tumefufua mchezo wa *Cricket* umetushinda kwa sababu kiwanja kimeharibika. Kwa kuwa mchezo ni wa wizara, lakini kiwanja cha Manispaa. Nadhani kama hatukushauriana na Manispaa waka-*takeover* kukirejesha katika hali yake, basi *Cricket* itashindikana, pengine itabidi tutafute sehemu nyengine kwa ajili ya mchezo huo kama tutafanikiwa kupapata.

Kwa hivyo, haya yote namuelekezea Mhe. Mjumbe kwamba michezo mingi imefufuliwa na inachezwa tena tunashinda na wala sio tunacheza kwa kushiriki isipokuwa tunacheza kwa kushinda na tunashinda.

Katika mkutano wa juzi nilipowaita hawa wana-*Golf* hata huyu jamaa alikuja tena na alifungua mkoba na kunionesha kikombe cha pili alichoshinda tena kwenye mashindano ya Tanzania. Kwa kweli tunakwenda mbele na tunachokiomba zaidi ni mashirikiano yetu kama mlivyotuonesha hivi leo wakati wa kujadili mswada huu.

Mhe. Haji Faki Shaali yeye alisema kama Baraza litafanyakazi vizuri na vyama vya michezo vitafanyakazi vizuri ni sahihi kabisa. Ametupa ushauri, lakini sikumfahamu aliposema Kamati Suluhishi au Usuluhishi isiishie Zanzibar, yaani ivuke bahari na kwenda Bara. Sikumfahamu kwa sababu katika usuluhishi tunaofanya baina sisi na wenzetu wa Bara tunafanyakazi kwa pamoja.

Kwa kweli tunafanya hivyo zaidi, kwa sababu wizara hizi mbili zinafanyakazi na hata kama si wizara za muungano. Lakini mambo au shughuli ama majukumu yetu ni ya kimuungano, maana huwezi kuweka mipaka ya bahari ifike hapa na huko uizuie isifike au utamaduni ufike hapa huko uzuie usifike, yaani huwezi kufanya hivyo.

Kwa hivyo, kwa makusudi tumeamua kushirikiana na kufanyakazi kwa pamoja na wala hatufanyi kazi kwa kusawazisha matatizo ya michezo peke yake hapana. Kwa mfano, juzi tulikuwa na mkutano wa pamoja katika ajenda saba basi ajenda moja tu ndio ya michezo na nyengine zote zilikuwa zikihusiana na habari na utamaduni.

Kwa maana hiyo, hatufanyi kazi ya michezo peke yake, lakini pale tunapogusa na michezo. Kwa mfano, juzi tulizungumza habari ya CHANEZA na CHANETA na wala hatukuzungumza hapa ya *TFF* na *ZFA*, kwa sababu suala la *TFF* na *ZFA* tulimaliza katika mkutano uliopita.

Mhe. Spika, tuliagiza CHANEZA na CHANETA wajirekebishe wameshindwa. Sasa tumewapa *ultimatum* ikifika wakati fulani wajirekebishe vyenginevyo hatua za kinidham zitachukuliwa na hilo. Mimi ni raia na mwenzangu yeye ni mwanajeshi, yaani amestaafu akiwa na cheo cha *Captain* na alitamka pale, kwamba nitachukua U-*captain* wangu nitautumia kwa kutoa adhabu kwa wale ambao hawataki kuliweka suala hili sawa.

Kwa hivyo, nataka kuthibitisha kwamba mashirikiano ya kimichezo, masuluhisho, nidhamu zinafuata pande zote mbili na tunashirikiana. Ingawa

hakuna kitengo kilichoundwa cha pamoja maana hizi kazi kila mtu na zake, kwa sababu tunashirikiana basi tunazifanya kwa pamoja.

Vile vile Mhe. Mjumbe amezungumza mambo mengine ya jumla na kuutaja mchezo wa Golf, ambao tayari nimeshautolea ufafanuzi kwa bahati nzuri kama unanisikia nje tunaufufua na tunaufufua kweli wala sio mchezo *(Makofi)*.

Pia amezungumza kuanzisha na kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kutoa Diploma za Michezo na kadhalika. Kwa kweli tutakaa pamoja na kulizungumza hili. Lakini hata muundo wetu wa Baraza tumesema Mjumbe mmoja atatoa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu Wizara ya Elimu ndiko kwenye chimbuko la michezo.

Sera yetu inazungumzia kutafuta vipaji na kuvikuza na tunazungumzia vipaji vya chini ya umri wa miaka 15, 17 19 na 20 na hao wapo maskulini. Mhe. Spika, hawa wapo tena wanashirikishwa kwenye *Bonanza*, *Academies* na kadhalika. Ndio maana *Zanzibar Heroes* safari hii wakafikia walipofika, kwa sababu ya *product* ya yule mwalimu tuliyomleta kutoka Cairo.

Kwa hiyo, hapa natoa jibu lile kwa nini lazima tupate mwalimu kutoka Cairo au nje. Nadhani tukubaliane kwamba bado kuna haja ya kuwasomesha makocha wetu kwa ajili ya kufika viwango vinavyotakiwa. Jukumu hilo tunalibeba na tunalifanya *(Makofi)*.

Lakini Moroco hawawezi kutupelekea timu ikapiga kambi Cairo kwa muda wa mwezi mmoja kila mwaka, yaani hawezi. Kwa maana hiyo, tumeichagua sisi Cairo kwa sababu hatukutaka kwenda Ulaya ambako ni mbali, lakini tumetafuta ndani ya Bara la Afrika kwamba timu gani yenye uwezo mzuri na sifa nzuri na tumeona ni Cairo. Kwa sababu ni mabingwa wetu wa Bara la Afrika miaka mitatu mfululizo na ukienda kwao utakuta *facilities* za michezo ni nyingi na tena uwezo wa mkubwa wa kufundisha.

Kwa hiyo, tutafanya yote mawili, bado tutaendelea kuagiza makocha kutoka nje waje watufundishe walimu wetu na pia watoe mafunzo kwa wanamichezo wetu. Kwa mfano, riadha tumeshapata makocha wawili wa *Field Events* na *Track*. Isipokuwa tumewazuia kusubiri *National Stadium* yetu imalizike na tukimaliza watakuja hawa lengo ni kufundisha wachezaji, lakini pia ni kuzalisha makocha wetu wa michezo. Kwa hivyo, mengi mliotwambia tunayafanya pengine labda tunafanya kikasa tunacheza chini chini gamba limetuzonga, na namna ya kuliondosha hili gamba hatuna. Kwa hivyo, mkubali tunayoyasema kwamba tunachukua juhudi kubwa sana na tuko makini katika kuongoza michezo.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Ali Salim amezungumza kuundwa kwa Baraza la Michezo, umezungumza kazi za Baraza la Michezo, umezungumza mikutano inayofanywa kwenye Baraza la Michezo, Katibu Mtendaji, muda wa uongozi. Haya yote umeyazungumza katika nia ya kutupa ushauri. Mhe. Spika, alisema muda wa kiongozi wa michezo wa miaka mitatu ni mdogo tuweke miaka labda mitano au tuweke nafasi yule tunayemuona anafanya vizuri tumuongezee muda. Hapa tumesema tutamuongezea mara moja kwa hivyo mitatu na mitatu inakuwa ni sita, lakini kama tutunge sheria *specifically* kwa wanaofanya vizuri aendelee kuwa daima kidogo itakuwa haina ladha, itakuwa ni sheria mahsusiya na hakuna sheria ya aina hiyo. Kwa hivyo, namuomba atukubalie.

Mhe. Spika, sheria ya mwanzo ilikuwa ni miaka miwili na mimi nilipokuja kwenye madaraka haya nilikuwa napata tabu sana. Kwa mfano, Mwenyekiti wa Baraza akimaliza kesho kutwa itabidi aondoke *unless* hii sheria imetiwa saini haraka haraka kabla hajamaliza muda wake, ndio sasa atabakia na mwaka mmoja zaidi. Kwa hivyo, itakuwa ni miaka miwili, tumesema hapana miaka miwili haitoshi hata ukiwa na programu ya muda mfupi basi mwenyekiti na kamati yake hata kuwe na muda wa kuitekeleza. Kwa hivyo ndio tumeweka miaka mitatu.

Mhe. Spika, namuomba atustahamilie na tutaendelea kufanya observation tutakwenda katika minne, mitano na kadhalika. Lakini kutunga sheria kwa kumtungia mtu atakayefanya vizuri hiyo itakuwa sio sheria nzuri na wanasheria wataikataa maana hizi sheria tunazozitunga hapa zikifika huko inaweza kuwa sheria batili Mahakama akaikataa na hayo yametokea. Mhe. Spika, mengine mengi aliyoyazungumza yalikuwa ni ya ujumla, ya kutushauri, kutuaidhi na kadhalika. Kwa hivyo, tumeyasikiliza na tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

Mhe. Spika, pia amelizungumza suala la Timu ya Shooting Star ya Mkoani-Pemba. Hili sio la Shooting Star peke yake, hili ni kero la Zanzibar nzima ndio maana tukaweka kifungu hapa cha sheria kitakachotuwezesha kusajili maeneo ya michezo ili sasa yasivamiwe na tukishasajili wapewe hatimiliki. Hivi sasa tunaelekea huko na tutafanya mazungumzo karibu na Waziri wa Ardhi tumeshaanza ku-*select* baadhi ya maeneo na tuna lengo la kuchagua *ground* mbili katika kila Mkoa tuzifanye kwamba hizi ni ground, tutaanza na football kwanza kwamba hizi ni ground zenye hadhi kidogo ya kitaifa na nyengine tutaziendeleza kidogo kidogo. Kwa hivyo, adhma hiyo ya kusajili na kutoa waraka tunayo.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma hoja yake ni nzito imechukua muda mrefu ilikuwa ni kuchanganya michezo na siasa, umeyasema mengi, umetupa tahadhari yote tumeyakubali. Lakini nina hakika ufafanuzi wa Mhe. Naibu Waziri umeusikia. Mhe. Spika, tunakataa kuchanganyisha kwa kubagua wewe

mchezaji katika timu yangu madamu CUF wewe usicheze katika timu yangu, na wewe refarii madamu CCM usichezeshe. Mhe. Spika, nimesema pengine labda maandishi hayakuwa vizuri ndio maana haikufahamika vizuri, ninasema tutai-*recast* ili ifahamike vizuri adhma yetu. Lakini hatuko katika adhma ya kuogopa na wala hatuogopi kwa sababu hatuwezi kuepukika kama ni CUF au kama ni CCM akiingia michezoni awe anatawaliwa na sheria moja ya michezo. Kwa hivyo, tutamdhibiti katika sheria hiyo.

Mhe. Ali Denge Makame ametoa pongezi na wewe umezungumza mjumbe kukaa miaka mitatu ni muda mfupi, jibu lake nashauri utuachie kidogo tuangalie huko mbele. Pia amependekeza tuongeze iwe miaka mitano, hiyo ni mapema kidogo. Mhe. Spika, mengi aliyoyazungumza yalikuwa ni ya ushauri yote tumeyapokea.

Mhe. Hija Hassan Hija amewasifu sana vijana wa Mkanyageni lakini umetutaka tumuombee malazi pema peponi kijana wako wa Mkanyageni aliyefariki akiwa uwanjani. Tumepokea na hata kama ni kimya kimya tumeshafanya hivyo, na wengine wataendelea kufanya hivyo, Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema mchezaji wetu huko aliko. Amina.

Mhe. Spika, kuhusu ngumi na ngwara nasema tunafuata wasia wa Rais wetu wa kwanza, ni kwamba ngumi bado lakini ngwara zinaelekea kwenye hizo ngumi hazijatafautiana na ile *kick boxing* Mhe. Mulla ananikubalia hivyo. Kwa hivyo, kama kuna hatari kwenye *boxing* Rais wetu wa awali Marehemu Amani Abeid Karume amesema kwamba tusipigane, sasa kwa nini tutiane ngwara na tuendelee kupigana. Kama tunacheza nje ya Tanzania tunapigana wenyewe kwa wenyewe vichochoroni basi na tupigane, lakini *official* kuisajili, kuitangaza hilo bado. Kama ilivyo kukutaa ufadhili wa pombe basi na hili tunaendelea kulikataa.

Mhe. Spika, naomba nitoe taarifa juzi kuna gazeti moja la Al-nour kuna mtu swahibu yangu mmoja alinipigia simu akaniambia mzee hebu tafuta gazeti la nour limekupongezeni sana wewe na Waziri wa Elimu kwa misimamo yenu ya kukataa ulevi usiingizwe katika michezo. Basi nililitafuta lile gazeti kulikuwa kuna makala tatu moja sitaki kuizungumza imeandikwa vipi na nyinyi nakuombeni litafuteni kwa sababu hili gazeti linatoka siku ya Alhamis. Lakini kama gazeti sasa linaanza kutambua umuhimu wa kukataza mambo haya nakutupongeza mimi nashukuru sana namwambia waziri mwenzangu alitafute hilo gazeti aone alivyoandikwa na yeye ameandikwa vizuri sana katika kuzuia ulevi usitangazwe kupitia michezo.

Mhe. Spika, nataka nimalizie mchango wako kwa kutoa ufafanuzi wa kosa kiwango chake ni kosa lipo ambalo linamfanya mtu sasa afukuzwe katika

chama. Mhe. Spika, sisi tumesema kosa likithibiti kama halikuthibiti basi sio kosa, lakini likithibiti hata kama ametozwa faini ya shilingi 20, 30, kenda jela mwezi mmoja, miaka mitano au sita ikiwa kosa limethibiti. Kwa hivyo, huyo ni mkosa wa jinai na kama ni mkosa wa jinai huyo hatufai katika Baraza la Michezo. Huo ndio ufafanuzi ambao naweza nikautoa, hatukuweka kiwango kwa sababu makosa yanapishana.

Mhe. Spika, pia ametukosoa kuandika ripoti ya utekelezaji unasema tungeandika utekelezaji wa ripoti. Mhe. Spika, sijui kipi kilichokuwa ni sahihi mimi nadhani chetu sisi tulichokiandika ni sahihi, lakini tutaangalia kasoro hiyo na tutarekebisha kile kinacholazimika.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri ametoa ufafanuzi mzuri sana hasa katika ile michango iliyojirejerejea ya udau na kadhalika. Mhe. Naibu Waziri amenisaidia sana na ameisaidia sana wizara yetu katika kutoa ufafanuzi alioutoa, namshukuru sana. Mhe. Spika, baada ya ufafanuzi huo sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo ya Mwaka 2010

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 2	Tafsiri pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Kifungu cha 3	Kuundwa kwa Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4	Wajumbe wa Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 5	Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6	Mamlaka na uwezo wa Baraza.
Kifungu cha 7	Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 8	Mikutano ya Baraza.
Kifungu cha 9	Akidi.
Kifungu cha 10	Uamuzi wa Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11	Uamuzi kutoathirika kwa athari za utaratibu.
Kifungu cha 12	Kumbukumbu za mikutano ya Baraza pamja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13	Posho la Wajumbe wa Baraza.
Kifungu cha 14	Kusita kwa Mjumbe wa Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 15	Muda wa uongozi.
Kifungu cha 16	Uteuzi wa Katibu Mtendaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 17	Majukumu ya Katibu Mtendaji.
Kifungu cha 18	Mrajis wa Vyama vya Michezo.
Kifungu cha 19	Mamlaka na majukumu ya Mrajis.
Kifungu cha 20	Wafanyakazi wa Baraza.
Kifungu cha 21	Sekreteriati ya Baraza.
Kifungu cha 22	Majukumu ya Sekreteriati.
Kifungu cha 23	Kamati ndogo ndogo za Baraza.
Kifungu cha 24	Baraza ya Michezo ya Wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25	Kazi za Mabaraza ya Wilaya.

SEHEMU YA TATU
MKUTANO WA WADAU

Kifungu cha 26	Mkutano wa wadau pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 27	Wajibu na majukumu ya Mkutano wa Wadau wa Michezo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 28	Mkutano wa Wadau wa Michezo.
Kifungu cha 29	Akidi.
Kifungu cha 30	Kumbukumbu za Wadau wa Michezo.

SEHEMU YA NNE
FEDHA, MATUMIZI NA UKAGUZI WA HESABU

Kifungu cha 31

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sikusikia katika ufafanuzi wa Mhe. Waziri kuhusiana na lile pendekezo nililozungumza la wale wanachama ambao ni wadau kupitia vile vilabu vyao kwamba tuongeze chanzo cha mapato kupitia ada za wanachama, kwa sababu kila *club* huwa ina wanachama wake. Kwa hivyo, nilikuwa nimependekeza suala hilo na sikupata ufafanuzi wake.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakubali mheshimiwa alilizungumza suala hilo na sikulitolea ufafanuzi namuomba mheshimiwa arudi kwenye sehemu ya nne fedha, matumizi, ukaguzi wa hesabu aangalie kifungu cha © kama hakuridhika basi nakubali tutakiingiza kwa namna alivyopendekeza. Naomba nikisome. Fedha zinazolipwa kwenye Baraza kwa njia ya mchango, ruzuku, kodi, ada na riba.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni itakapoandikwa itapanga ule undani zaidi hizi pesa zitapatikana vipi na kadhalika. Kwa hivyo, nilisahau kumjibu lakini kwa kweli hoja yake imeingizwa katika kifungu cha ©.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi unanifanya niridhike kwamba hili neno ada hapa litapata ufafanuzi vizuri kwenye kanuni, tuendelee.

Kifungu cha 31 Mapato ya Baraza.
Kifungu cha 32 Akaunti ya Baraza.
Kifungu cha 33 Matumizi ya fedha za Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 34 Ripoti za Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 35 Hesabu na ukaguzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 36 Utekelezaji wa nyaraka pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI MENGINEYO

Kifungu cha 37 Ukabidhishaji wa rasilimali.
Kifungu cha 38 Uwezo wa kutunga kanuni.
Kifungu cha 39 Kufuta na kuweka sheria pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo ya Mwaka 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo ya Mwaka 2010 usomwe kwa mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu usomwe kwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru tena kwa mashirikiano makubwa kutimiza wajibu wetu katika Baraza hili la wananchi.

(Saa 1:20 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 29/03/2010 saa 3:00 asubuhi)